

**MAUDHUI YA UKOLONI MAMBOLEO KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA
KISWAHILI**

**NA
IKUATHU SILAS THURANIRA**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA
KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

2017

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Ikuathu Silas Thurania

(Mtahiniwa)

TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Prof. Mwenda Mbatiah

(Msimamizi)

TAREHE

Dkt. Evans Mbutia

(Msimamizi)

TAREHE

TABARUKU

Kazi hii naitabarukukia mke wangu mpendwa, Mary Ngithi, kwa kunipa moyo wa kuendeleza masomo yangu hadi kufikia kiwango hiki pamoja na watoto wangu wapendawa Caleb Kaume na Boaz Murithi kwa kuvumilia upweke mwingi nilipokuwa masomoni.

SHUKRANI

Kwanza namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijaalia baraka lukuki tangu mwanzo mwa kuzihii hadi kufikia sasa. Nakiri kwamba pasingekuwa na uwezo huo nisingekamilisha kazi hii. Mungu atukuzwe milele.

Pili, ningependa kutoa shukrani zangu za dhiti kwa wasimamizi wangu, Profesa Mwenda Mbatiah na Daktari Evans Mbuthia kwa sababu ya mwongozo wenu wa hekima. Kwa muda wenu mliotumia kuifanyia kazi hii marekebisho pamoja na kutoa ushauri mwafaka Mungu ambariki. Kupitia ushauri wenu wa mara kwa mara, msaada wa vitabu na mawazo ulinifaa sana. Bila shaka kazi hii haingepiga hatua yoyote mbele pasi na maelekezo yenu. Mlinisaidia kuipanga kazi na kunionyesha mengi ambayo nisingeyafahamu. Asanteni.

Wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili walionifundisha wanastahili shukrani za kipekee kwa maarifa waliyonipa kupitia mijadala na mawaidha yao darasani. Wamenifaa mno pia wakati wa mradi huu kupitia mapendekezo na maelekezo ya kina. Katika muktadha huu nawashukuru Prof. Iribe Mwangi, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof John Habwe, Prof. Rayya Timammy, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. K.W. Wamitila, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Mukhwana Ayub, Mwalimu Sanja Leo na Mwalimu Mary Ndung'u.

Wanafunzi wenzangu pia nawashukuru kwa mchango wenu hasa majadiliano tuliyofanya ndani na nje ya darasa. Mlinipa moyo wakati kazi ilipozidi. Hawa ni George Oiro, Kithinji Nicholus, Florence Wambui, Raymond Owala, Peter Nyamburi, Nina Naisimoi, Kelvin Okello, Lillian Nzambi, Musamali Steve, Rose Munyao, Claris Uchi Chaniro, Victor, Veronica, Pauline na Domenic.

Familia yangu naipa kongole kwa kunifaa kwa njia mbalimbali wakati nilipokuwa katika masomo haya. Kwa mke wangu, Mary, nasema asante kwa msaada wako wa kifedha, maombi na kunihimiza kumaliza kozi. Watoto wangu Caleb na Boaz pongezi kwa kuvumilia upweke nilipokuwa chuoni.

Kwa marafiki zangu hasa walionitangulia katika masomo ya uzamili mlinitia hamu ya kusoma nikijaribu kuwafikia. Kwa mwalimu mwenzangu, Morris Gitiye, ulinifaa sana kwa vitabu ulivyonipa pamoja na maoni kuhusu mwelekeo wa kazi hii.

FASILI ZA ISTILAHU MUHIMU ZILIZOTUMIWA KATIKA UCHUNGUZI

Nchi za ulimwengu wa tatuNchi zilizobaki nyuma kimaendeleo
Mataifa machanganchi zilizobaki nyuma kimaendeleo
Mataifa yaliyoendeleaNchi zenye maendeleo makubwa ya kiuchumi
Washenzi..... Waliokosa ustaarabu
Ukoloni maradufuudhalilishwaji changamano unaowaathiri wanajamii kwa njia tofauti
Wingine Utengwaji wa mataifa machanga
Utamaduni mahuluti.....Mchanganyo wa tamaduni mbili au zaidi

VIFUPISHO

D.O. . District Officer
EC European Commission
IMF International Monetary Fund
LEGCO Legislative Council
MDGs Millenium Development Goals
W.T.O World Trade Organization

IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia maudhui ya ukoloni mamboleo na uwasilishaji wake katika tamthilia mbili za Kiswahili. Tamthilia zilizohakikiwa ni *Mstahiki Meya* (2009) na *Kijiba cha Moyo* (2009) za Timothy Arege. Uchunguzi wetu ulinua kuchunguza vipengele mbalimbali vya ukoloni mamboleo kama vinavyojitokeza katika tamthilia hizo mbili.

Nadharia ya ubaada-ukoloni imetumika katika utafiti huu. Mihimili yake iliyotufaa ni kama vile, utengwaji wa kimataifa, ukandamizwaji wa utamaduni wa mataifa machanga pamoja na uibukaji wa utamaduni mseto kwa mataifa yaliyotawaliwa. Pia tumetumia baadhi ya vipengele vya nadharia ya elimu-mitindo katika kuchambua jinsi mtindo ulivyofanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Mtafiti alisoma tamthilia husika kwa kina, majarida na magazeti mbalimbali, tasnifu na vitabu vingine vya ziada ili kupata data iliyohitajika. Data hiyo ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti pamoja na nadharia zilizotajwa hapo juu. Uchanganuzi ulifanywa kwa njia ya maelezo.

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuonyesha mbinu mbalimbali zinazotumiwa na mataifa yaliyoendelea katika kutawala na kudhibiti mataifa yanayoendelea; kubainisha athari za ukoloni mamboleo kama zinavyojitokeza katika tamthilia teule; kuonyesha mchango wa baadhi ya vipengele vya fani katika kufanikisha maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia teule na mwisho tulikusudia kubainisha aina ya uhusiano uliopo kati ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea. Kutokana na utafiti huu, ilibainika kwamba mataifa yaliyoendelea hutumia mbinu fiche mbalimbali katika kuzidhibiti nchi zinazoendelea. Njia hizo zimeacha athari hasi nyingi kwa uchumi wa mataifa machanga. Athari hizo zimesababisha kuwepo kwa uhusiano wa kidhalimu baina ya mataifa.

YALIYOMO

Mada	Ukurasa
Ungamo.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Fasili za Istilahi Muhimu Zilizotumiwa katika Uchunguzi.....	v
Vifupisho.....	v
Ikisiri.....	vi
Yaliyomo.....	vii

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo La Utafiti.....	2
1.3 Maswali ya Utafiti.....	3
1.4 Madhumuni ya utafiti.....	3
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	4
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	5
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada Hii.....	5
1.8 Msingi wa Kinadharia.....	10
1.8.1 Ubaada-ukoloni.....	10
1.8.2 Elimumitindo na Nguzo zake.....	14
1.9 Mbinu za utafiti.....	16
1.10 Hitimisho.....	17

SURA YA PILI

MAANA YA UKOLONI

2.1 Utangulizi.....	18
2.2 Ukoloni Mkongwe.....	18
2.3 Ukoloni Mamboleo.....	28
2.4 Hitimisho.....	35

SURA YA TATU

NAFASI YA UTEGEMEZI WA KIUCHUMI NA TAASISI ZA KIMATAIFA KATIKA KUENDELEZA UKOLONI MAMBOLEO

3.1 Utangulizi.....	37
3.2. Utegemezi wa Kiuchumi.....	37
3.3 Sera za Taasisi za Kimataifa.....	44
3.3.1 Mpango wa kutoajiri na ustaafishaji mapema wa wafanyikazi.....	45
3.3.2. Sera ya Kugawanya Gharama	49
3.3.3 Malengo ya Kimaendeleo ya Milenia	50
3.4 Hitimisho.....	52

SURA YA NNE

UBEBERU WA KITAMADUNI NA MATUMIZI YA MBINU ZA KIUTAWALA ZA KIKOLONI KATIKA UENDELEZAJI WA UKOLONI MAMBOLEO

4.1 Utangulizi.....	53
4.2 Ubeberu wa Kiutamaduni	53
4.2.1 Elimu ya Kigeni	54
4.2.2 Huduma za Afya za Kigeni	61
4.3 Matumizi ya Mbinu za Kiutawala za Kikoloni.....	64
4.3.1Tenga Utawale.....	64
4.3.2 Dhuluma dhidi ya Wafanyaikazi	67
4.3.3 Matumizi Yasiyofaa ya Polisi	70
4.3.4 Unyakuzi wa Maliasili	72
4.4 Mbinu za Lugha Zilizofanikisha Maudhui Katika Kazi Hii	74
4.5 Hitimisho.....	78

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi.....	80
5.2 Muhtasari	80
5.3 Hitimisho.....	83
5.4 Mapendekezo	85
MAREJELEO	86

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi

Kazi hii ilidhamiria kutalii maudhui ya ukoloni mamboleo kama yalivyojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili na jinsi maudhui hayo yalivyowasilishwa. Mwandishi wa kazi ya kifasihi hupata kariha ya uandishi wake kutoka kwa mazingira ya jamii yake. Kwa sababu hii, tunaamini kwamba mtunzi anapoandika kuhusu suala kama hili la ukoloni mamboleo, huwa amechochewa na athari zinazoonekana za suala hilo. Kwa hivyo, ni sahihi kuchukulia kuwa bara la Afrika limeathiriwa na tatizo la ukoloni mamboleo na ndio sababu waandishi wa Kiafrika wanalizungumzia katika kazi zao.

Dhana ya ukoloni mamboleo imetolewa fafanuzi mbalimbali na waandishi tofauti tofauti. Kwa mfano, ukoloni mamboleo unaelezwa na “*The Online Thesauras*” kama sera ya nchi yenye nguvu ya kuendeleza utawala na udhibiti wa nchi nyingine huru au eneo fulani la kijiografia bila kufanya nchi au eneo hilo koloni kirasmi (T.Y). Jambo la kimsingi linalojitokeza katika fasili hii ni kuwa ukoloni mamboleo huhusisha utawala na udhibiti wa nchi zilizokuwa chini ya mkoloni. Pia ni wazi kuwa ukoloni mamboleo uhusisha ukandamizwaji wa watu na nchi zisizo na nguvu za kiuchumi. Ukoloni mamboleo unachukua sura mbalimbali kama vile unyamazishwaji wa lugha asili na unyakuzi wa maliasili ya nchi changa.

Padley (2006) anaeleza kwamba suala la nchi chache zenye nguvu zaidi za kiuchumi na kisiasa kuzitawala nchi zisizo na nguvu hizo limekuwepo tangu enzi za kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Kwa mfano, anadai kuwa kufikia mwisho mwa karne ya kumi na tano mataifa ya Ulaya kama vile Ufaransa, Uingereza, Uhispania, Ureno na Uholanzi yalikuwa yameanza kuvamia maliasili ya ulimwengu mzima. Kwa mfano, nchi tulizozitaja hapo juu zilishiriki biashara ya utumwa ambayo iliwadhulumu sana watu weusi. Kufikia kipindi cha ukoloni, yaani kufikia karne ya kumi na tisa, Uingereza ilikuwa imetawala na kudhibiti robo nzima ya ulimwengu. Kwa mfano, ilikuwa inadhibiti India, Australia, Canada, Newzealand, Ireland, Marekani Kusini, Mashariki ya Kati na sehemu kubwa ya bara la Afrika na West Indies.

Udhibiti na utawala wa mataifa machanga haukukoma baada ya uhuru kupatikana na mkoloni kuondoka katika mataifa na maeneo tuliyoyataja hapo juu. Utawala wa mataifa yenye nguvu za kiuchumi kwa mataifa machanga uliendelezwa kwa kutumia mbinu mpya (ukoloni mamboleo).

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza njia na mbinu hizo mpya zinazotumiwa na nchi zilizoendelea katika kuzitawala na kuzidhibiti nchi zinazoendelea. Tamthilia za Kiswahili tulizozichunguza (*Mstahiki Meya na Kijiba cha Moyo*) zimeangazia baadhi ya mbinu hizo. Kama tulivyoona katika uchunguzi wa tamthilia hizo, mbinu hizo ni kama vile: utoaji wa mikopo na misaada pamoja na biashara ya kimataifa. Mkakati mwingine unahusu matumizi ya sera kandamizi za mashirika ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani. Mbinu nyingine zinazoashiria ukoloni mamboleo katika tamthilia tulizohakiki ni kama vile mfumo wa kugawana gharama katika sekta za elimu na afya, mipango ya kupunguza idadi ya wafanyikazi na mipango ya maendeleo ya millenia (MDGs). Kwa kuwa fani na maudhui ni viambajengo vya fasihi visivyoweza kutenganishwa, kazi hii ilichunguza vipengele vya fani, hasa matumizi ya lugha na uhusika, vinavyokuza maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia za *Mstahiki Meya na Kijiba cha Moyo* (za Arege). Katika kuchunguza mbinu za uwasilishaji, tulijikita katika ukiushi wa kisemantiki na wa kileksika na kuonyesha mchango wake katika kuendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo.

Tamthilia za mwandishi huyu zimezungumzia maudhui ya ukoloni mamboleo kwa kina na zinaweza kutumiwa kama vichocheo vya kuwazindua viongozi wa Kiafrika kuanza kuzikabili athari hasi za ukoloni mamboleo. Tamthilia hizi zimetungwa kwa ufundi mkubwa unaodhihirika kupitia matumizi pevu ya fani, hasa matumizi ya lugha.

1.2 Tatizo La Utafiti

Utafiti huu ulichunguza maudhui ya ukoloni mamboleo na uwasilishaji wake katika tamthilia mbili za Timothy Arege ambazo ni *Mstahiki Meya na Kijiba cha Moyo*. Tulikusudia kuonyesha jinsi mwandishi huyu alivyolitalii suala la ukoloni mamboleo kisanii ili kukuza dhamira yake. Ili kufanikisha haya, tulihakiki pia vipengele vya fani vilivyofanikisha uwasilishaji wa maudhui haya. Tulikusudia kuonyesha namna tungo hizi zinavyolidhihirisha suala la ukoloni mamboleo pamoja na athari zake. Kwa mfano, utafiti huu ulichunguza njia mbalimbali zinazotumiwa na

nchi zenye nguvu za kiutawala na kiuchumi katika kuzidhibiti na kuzikandamiza nchi changa, kama ilivyoonyeshwa katika tamthilia zilizotajwa hapo juu.

Ukoloni mamboleo ni tatizo linalolemaza maendeleo katika nchi nyingi hasa zile zisizo na nguvu za kiuchumi. Hii ni kwa sababu nchi zilizoendelea hupania kuzitawala nchi changa kwa njia fiche ili kutimiza maslahi yao. Matokeo ya kutawaliwa huku ni kuibuka kwa athari hasi za ukoloni mamboleo hasa unyonywaji wa kiuchumi. Uhusiano unaojengeka baina ya mataifa haya unakuwa wa kinyemela na uliojaa unafiki. Mwishowe, mataifa haya machanga yanakosa kujitambua na kujinazua kutoka kwa athari hasi za ukoloni mamboleo. Ni wazi kwamba hili ni suala nyeti kwa wananchi wa mataifa machanga kote duniani kwa sababu linaathiri si tu maendeleo bali pia hali za maisha ya wanajamii wa nchi hizo. Hata hivyo, tatizo hili halijatafitiwa kwa kina kinachostahiki hasa na wasomi wa Kiswahili. Kwa hivyo kuna umuhimu wa kuchunguza ni vipi maudhui ya ukoloni mamboleo yalivyojitokeza katika tamthilia za Kiswahili. Hili ndilo pengo tulilokusudia kuliziba.

1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

- (i) Je, ukoloni mamboleo umeacha athari hasi zipi za kimaendeleo katika mataifa machanga kama inavyodhihirika katika tamthilia teule?
- (ii) Je, ni mbinu zipi zinazotumiwa katika kuendeleza ukoloni mamboleo na zinatambulikana wazi wazi na wananchi wa nchi zinazoendelea?
- (iii) Mataifa machanga yamechukua mikakati madhubuti ya kujikomboa kutokana na athari hasi za ukoloni mamboleo?
- iv) Je, uhusiano baina ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea unafaidi pande zote mbili kiuchumi?

1.4 Madhumuni ya utafiti

Malengo ya utafiti wetu yalikuwa:

- (i) Kuonyesha mbinu mbalimbali zinazotumiwa na mataifa yaliyoendelea katika kudhibiti na kutawala mataifa yanayoendelea.

- (ii) Kubainisha athari za ukoloni mamboleo kama zilivyowasilishwa katika tamthilia teule na jinsi athari hizi zinavyolemaza maendeleo katika nchi changa.
- (iii) Kuonyesha mchango wa baadhi ya vipengele vya fani katika kufanikisha maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia teule.
- (iv) Kubainisha uhusiano uliopo kati ya nchi zinazoendelea na zile zilizoendelea.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Sura mpya za ukoloni mamboleo zinazidi kujitokeza kadri ulimwengu unavyobadilika. Kwa mfano, kuna tofauti kuhusu jinsi ukoloni mamboleo ulivyokuwa miaka ya sabini, themanini, tisini na sasa. Tamthilia za Kiswahili nazo zinaendelea kudhihirisha mabadiliko haya. Kwa hivyo, tumeteua mada hii ili kuonyesha sura mpya za ukoloni mamboleo.

Wahakiki wengi wa tamthilia za Kiswahili waliowahi kuliangalia swala la ukoloni mamboleo katika tamthilia za Kiswahili, hawajaonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyoathiri maendeleo katika mataifa machanga. Kwa hivyo, tunakusudia kuliziba pengo hili kwa kuzijadili athari hizi kama zinavyojitokeza katika tamthilia teule za Kiswahili.

Vile vile, maarifa yanayohusu mada hii yamejikita mno katika masomo ya uchumi na yale ya uhusiano wa kimataifa, somo la biashara au historia. Sisi tulitarajia kuwa utafiti huu ungeyalingiza maarifa haya kutoka kwa masomo ya biashara na uchumi hadi kwa somo la Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, tulikusudia kuzua maarifa mapya ili kuwafaidi wasomi wa fasihi ya Kiswahili.

Zaidi ya hayo, tamthilia za *Kijiba cha Moyo na Mstahiki Meya* hazijahakikiwa kwa lengo la kuonyesha maudhui ya ukoloni mamboleo na uwasilishaji wake. Kwa misingi hii basi, hakuna uhakiki uliopo wa tamthilia hizi unaotumia nadharia ya ubaada-ubaada ukoloni. Kwa hivyo, utafiti huu unakusudia kuliziba pengo hili la kiakademia.

Mwisho, tamthilia hizi zimeteuliwa kimakusudi ili kuwakilisha kipindi cha karne ya ishirini na moja. Kwa sababu hii tamthilia zote zilizoteuliwa ni za miaka ya 2000, kipindi ambacho kimeshuhudia ongezeko kubwa la unyanyasaji wa kiuchumi wa mataifa ya Kiafrika si tu kutoka nchi za Kimagharibi bali pia kutoka Mashariki (haswa Uchina)

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti wetu unahusu tamthilia mbili za mwandishi Timothy Arege. Mwandishi huyu ameandika tamthilia tatu ambazo ni *Mstahiki Meya* (2009), *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Chamchela* (2007), lakini tumeteua tamthilia mbili zake kimaksudi kwa kuwa sio tamthilia zake zote zimegusia mada yetu. Kwa sababu hii, tumehakiki tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kijiba Cha Moyo* kwa sababu zimeliangazia suala letu la utafiti kwa kina.

Vilevile kwa sababu swala la ukoloni mamboleo ni pana mno, sisi tumechunguza tu njia zinazotumiwa na nchi zilizoendelea katika kudhibiti uhuru, uongozi na maendeleo ya nchi zinazoendelea. Kwa kuwa yaliyomo katika kazi ya kifasihi na jinsi yanavyowasilishwa ni mambo yasiyotenganishika wazi wazi, tumechunguza pia baadhi ya vipengele vya kimtindo vinavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui. Vipengele hivyo ni matumizi ya lugha na uhusika. Pia uhakiki huu umetumia nadharia ya ubaada ukoloni ili kuweza kushughulikia kikamilifu maudhui ya ukoloni mamboleo. Pia, tumetumia baadhi ya vipengele vya elimumitindo ili tuweze kufafanua njia za uwasilishaji huo.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada Hii

Fanon (1963) akigusia suala la uhusiano wa kimataifa uliopo haswa kati ya Afrika na Uropa, anadai kuwa utajiri lililona bar la Ulaya pia ni utajiri wa Waafrika. Anasisitiza kwamba:

Bara la Ulaya limejilimbikizia dhahabu na aina nyingine za maliasili kutoka kwa nchi zilizotawaliwa za Afrika, China na Marekani ya Kusini. kwa kila dalili ya utajiri iliyopo Ulaya, ni ishara ya utolewaji nje wa maliasili ya mabara hayo mengine-dhahabu, mafuta, pamba, almasi na aina nyingine za mali .
Bara la Ulaya kimsingi limeumbwa kutokana na nchi za ulimwengu wa tatu (81- 83) (T.Y)

Maoni ya Fanon ni muhimu kwetu kwa sababu yanadokeza baadhi ya mbinu zinazotumiwa na mataifa ya ulimwengu wa kwanza katika kuyakandamiza mataifa ya ulimwengu wa tatu hasa kiuchumi. Mbinu ambazo Fanon anadokeza ni kama vile ; wizi wa maliasili ya Kiafrika ulioendelezwa na mkoloni pamoja na ukoloni mamboleo hasa kupitia utoaji wa misaada na mikopo. Anadai kuwa bandari za Uholanzi, Bourdeaux na Liverpool zimejengeka na kukomaa kwa sababu ya biashara ya utumwa. Kwa sababu hiyo basi, Fanon anakiri kuwa bara la Ulaya

linapotoa misaada kwa mataifa machanga, mataifa hayo machanga yanapaswa kusema, 'Hii ni haki yetu na tayari tushailipia...ni malipo ya tulichopokonywa.' T.Y

Kwame Nkrumah (1965) anasema kwamba ukoloni mamboleo upo katika awamu zake za mwisho lakini awamu hizo ndizo hatari zaidi. Anadai kuwa nchi za Kiafrika kinadharia zina uhuru unaotambulikana na jamii ya kimataifa lakini katika hali halisi, mifumo ya kiuchumi na kisiasa yao inaongozwa kutoka nje. Maoni haya ya Nkrumah yatatufaa katika kuhakiki tamthilia tulizoteua kwa kuonyesha athari za sera za Kimagharibi katika maendeleo ya nchi changa.

Rodney (1973) anasema kuwa njia moja kuu iliyotumiwa na mataifa ya Magharibi katika kujenga Ulaya ni aina mbili za biashara. Biashara ya utumwa ya kabla ya ukoloni na biashara ya kisasa ya kimataifa ambayo sheria zake zinatungwa bila kulihusisha bara la Afrika. Rodney anasema kuwa Ulaya ndilo bara lililohodhi vyombo vya kusafiria majini na usafiri huu ulisaidia ukuaji wa haraka wa Ulaya kwani meli zao zilihakikisha utoshelevu wa malighafi ya viwanda. Anasema kuwa biashara hii inaendeleza unyanyasaji kwa nchi changa. Kando na biashara kama njia ya kuendeleza ukoloni-mamboleo, Rodney pia anachukulia kuwa makampuni ya kimataifa yameendeleza ukoloni mamboleo katika bara la Afrika na kwingineko. Kwa mfano, analaumu taasisi kama vile benki za Ulaya, Mashirika yanayomiliki meli, makampuni kama vile yale ya uchimbaji madini na mengineyo. Anazishutumu kampuni za kimataifa (Sunlight, Unilever, Lifebuoy, Lux na Vim) kwa kutegemea maliasili ya Afrika Magharibi ili kujiendeleza huku yakiwadhulumu wakulima. Masuala anayoibua mwandishi huyu yana uzito sana katika uhakiki wetu kwani yeye anatambua njia za kisasa zinazoendeleza ukoloni mamboleo ambazo ni: biashara ya kimataifa, makampuni na benki za Ulaya na unyanyasaji wa wafanyikazi. Sisi tumechunguza mbinu hizi na nyinginezo kama zinavyojitokeza katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo na Mstahiki Meya*.

Encyclopedia Britanica, (1988) inafafanua kuwa ukoloni mamboleo ulitumiwa mwanzo kwa kuhusishwa na sera za Kiulaya ambazo zilionekana kama njia za kidhibiti mataifa ya Kiafrika na mataifa mengine tegemezi. Inaendelea kusema kuwa kilichosababisha uibukaji wa isitilahi hii ni kongamano lililofanyika Paris mwaka wa 1957 ambapo mataifa sita ya yalikubaliana kuweka koloni zao katika mfumo wa "The European Common Market". Kitendo hiki kilikosolewa na

viongozi wa kitaifa na vikundi vingine mbalimbali kwa sababu hatua hii ilichukuliwa kama njia mpya ya unyanyasaji wa kiuchumi. Kwa upana zaidi, ukoloni mamboleo huchukuliwa kama udhibiti usiokuwa wa moja kwa moja unaoendelezwa kupitia sera za kibiashara, kampuni za kimataifa, sera za kifedha na taasisi za kifedha za kilimwengu. Maelezo haya ya Encyclopedia Britanica yanatusaidia kusesitiza tatizo la utafiti huu kwani haya ndiyo mambo tunayokusudia kuchambua kutoka katika tamthilia teule. Wakosoaji wa ukoloni mamboleo wanasema kuwa, mfumo huu huendelezwa kupitia uwekezaji wa kampuni za kimataifa katika nchi za ulimwengu wa tatu. Kulingana na Encyclopaedia Britanica, kampuni hizi hufaidi watu wachache katika nchi changa na kijumla huendeleza hali ya utegemezi. Inadai pia kuwa taasisi za kifedha za kimataifa kama vile Benki ya Dunia na Shirika la Kifedha la Dunia zimelaumiwa kwa kuendeleza ukoloni mamboleo kwa kutoa mikopo na misaada ya kiuchumi inayokuja na vikwazo vingi na kisha kuacha athari kubwa hasi kwa chumi changa.

Mkangi (1995) anaonyesha njia nyingine inayotumiwa kuendeleza ukoloni mamboleo kwa kuyadhibiti mataifa machanga ambayo ni matumizi ya taasisi za kimataifa, haswa sera za benki ya dunia. Sera moja anayokejeli Mkangi ni ile ya kuyalazimu mataifa machanga kupanda mazao ya kuleta fedha za kigeni ilhali nchi hizi pia hazijitoshelezi kichakula. Mazao haya yana jina maarufu la' *Kachatapami*', yaani, kahawa, chai, katani, pareto, pamba na miwa. Kwa mfano, katika riwaya hii ya *Walenisi*, kuna mazungumzo baina ya karani na Dzombo ambapo karani anamwambia Dzombo kuwa mahindi yake yalifyekwa kwa sababu 'Benki ya Dunia yenyewe ndiyo iliyotushauri kuwa sehemu hii inapaswa kupandwa mazao ya kutuletea fedha za kigeni'(uk. 18). Udhibiti huu unatiliwa nguvu zaidi wakati wa uuzwaji wa mazao haya katika soko la nje kwani mataifa haya ndiyo huamua bei. Mawazo haya ya Katama Mkangi yanashabihiana na yale ya Rodney (1973) kuhusu biashara ya kimataifa na jinsi inavyokandamiza nchi za ulimwengu wa tatu. Huu ni mchango muhimu sana kwa utafiti huu kwani kando na biashara ya kimataifa, tunakusudia kuonyesha mbinu nyingine zinazotumiwa na utawala wa kimataifa katika kuyadhibiti mataifa machanga. Mkangi analishughulikia suala hili katika utanzu wa riwaya huku nasi tukionyesha jinsi waandishi wa tamthilia walivyolishughulikia.

Wafula (1999) anaonyesha historia fupi ya tamthilia ya Kiswahili nchini Kenya na Tanzania haswa akichunguza mabadiliko ya kimaudhui na kimtindo. Uchanganuzi wake wa Tamthilia ya *Amezidi* (uk.78-79) umetufaa sana kwa sababu anadhihirisha jinsi nchi zilizoendelea zinavyolilemaza bara la Afrika hasa kupitia misaada na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya Afrika kiholela. Kando na hili, amezungumzia suala la uongozi katika mataifa ya Kiafrika kama linavyojitokeza katika tamthilia hii. Wafula anadai kuwa 'Mbali na viongozi kulifisidi bara lao, hawana ubunifu wa kimawazo kuwawezesha Waafrika kujitegemea. Wanastarehe kwa bidhaa ambazo hawafahamu asili wala chanzo chake. (uk.79). Mambo anayoyaibua mhakiki huyu ni muhimu kwetu kwa sababu suala analolizungumzia la misaada na uagizaji wa bidhaa, sisi pia tumeliangazia kama mojawapo ya baadhi ya njia zinazoendeleza ukoloni mamboleo na ambazo tumejadili kwa kina katika utafiti wetu.

Were (2012) alihakiki tamthilia za *Kilio cha Haki* na *Kijiba cha Moyo* kifani. Alichunguza mbinu za lugha (dayalojia na monolojia), wahusika na dhana ya ploti. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwani yeye anatumia tamthilia moja ya Timothy Arege huku sisi tukichunguza tamthilia mbili zake. Pia tunatofautiana kinadharia. Yeye anatumia nadharia ya umuundo huku nasi tukitumia nadharia ya ubaada ukoloni na vipengele vichache vya elimumitindo. Hata hivyo, utafiti wake umetufaa sana hasa uchanganuzi wake wa mbinu ya monolojia. Maelezo yake kuhusu mbinu hii yametusaiaid kuelewa vyema kinachowakilishwa na mhusika Sele katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. Pili, uhakiki wake wa ploti umetufaa hasa kuhusu suala la uhusiano wa kimataifa unaowakilishwa na jazanda za Madaktari, Sele, Vidagaa, Papa na Bahari (uk.99-103). Uchanganuzi wake wa jazanda umetuwezesha kubainisha kipengele cha fani kinavyofanikisha maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia mojawapo tuliyoichunguza ya *Kijiba cha Moyo*.

Magati (2013) amehakiki kuhusu ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia tatu za Timothy Arege. Alichunguza vipengele vya ploti, msuko, wahusika na mchango wake katika kuendeleza dhamira. Utafiti wake unatofautiana na wetu kwani sisi tumechunguza suala la ukoloni mamboleo katika tamthilia mbili za Arege. Pia yeye anatumia nadharia ya umuundo huku sisi tukitumia nadharia ya ubaada-ukoloni na vipengele vya elimumitindo. Hata hivyo, kazi yake imetufaa hasa uchanganuzi wake wa msuko umetusaiaid kuzielewa tamthilia za Arege vyema.

Magati ameliangalia swala la uongozi na utawala lakini akionyesha udhalimu wa viongozi wa Kiafrika dhidi ya wananchi wao huku sisi tukiangalia jinsi udhalimu unavyotekelezwa na mataifa yaliyoendelea kwa mataifa machanga.

Okwena (2013) ametafitia matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu za Timothy Arege, huku sisi tukichunguza tamthilia zake mbili. Pia mwelekeo wake unasisitiza fani huku sisi tukiegemea maudhui hasa swala la jinsi mataifa machanga yanavyozidi kukandamizwa na kudhibitiwa na mataifa yaliyoendelea. Yeye ametumia nadharia ya kimtindo ya Buffon (1930) na Crystal na Davy (1969). Hata hivyo, tumefaidika kutokana na kazi yake haswa ufafanuzi wa mafumbo yanayopatikana katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*.

Kairi (2014) alitafiti kuhusu swala la ukoloni mamboleo na utandawazi katika tamthilia mbili za *Sudana* (2006) ya Alamin Mazrui na Kimani Njogu na *Posa za Bikisiwa* (2008) ya S.A Mohamed na King'ei Kitula. Utafiti huu unatofautiana na wetu kimada na kiuteuzi wa tamthilia. Kwa mfano huku yeye akitumia tamthilia mbili za waandishi wawili tofauti, sisi tumetumia tamthilia za mwandishi mmoja. Pili, yeye anatilia mkazo kwenye uhusiano kati ya utandawazi na ukoloni mamboleo huku sisi tukichunguza uhusiano uliopo kati ya mataifa yaliyoendelea na yale yanayoendelea. Tumenufaika hata hivyo na kazi hii hasa kuhusiana na nadharia. Hii ni kwa sababu mhakiki ametumia nadharia ya ubaada-ukoloni ambayo pia sisi tunatumia.

Kilanga (2014) alichunguza matumizi ya ishara katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* (2009) ya Arege na *Kaptula la Marx* (2010) ya Kezilahabi. Amefafanua maana za ishara mbali mbali zinazojitokeza katika tamthilia hizo. Maelezo ya jazanda hizi yametusaikia katika kuelewa ploti ya tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* vyema. Hata hivyo, utafiti huu unatofautina na wetu kwa sababu sisi tunahakiki maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kijiba cha Moyo*.

Khamisi (2015) alichunguza usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* huku akitilia mkazo mbinu zinazofanikisha usimulizi katika tamthilia. Pia ameonyesha aina na daraja za usimulizi. Utafiti huu umetufaa hasa katika kuelewa msuko wa tamthilia hizi. Kazi hii inajikita katika mwelekeo wa kifani kinyume na uhakiki wetu ambao unalenga maudhui.

Matundura, Kobia na Ngesa (2015) katika *Swahili Forum* 22, wameangazia mwingilianomatini kati ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Kijiba cha Moyo* (2009). Wanaonyesha aina na viwango vya mwingilianomatini kati ya tamthilia hizi. Kwa mfano, wanafafanua mwingilianomatini wa kimaudhui na wa kijazanda. Baadhi ya maudhui wanayoangazia ni ukoloni mamboleo, elimu ya kigeni na suala la magonjwa na matibabu. Maelezo yake kuhusu ukoloni mamboleo yalitufaa kwani sisi pia tulichunguza jinsi ukoloni mamboleo unavyojidhihirisha katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Wao wanatumia nadharia ya mwingilianomatini huku sisi tukitumia nadharia ya ubaada ukoloni.

1.8 Msingi wa Kinadharia

Katika sehemu hii tunajadili nadharia za ubaada ukoloni na elimu mitindo. Kando na kuonyesha mawazo makuu ya waasisi wa nadharia hizi, tutaonyesha pia mihimili ya nadharia zote mbili iliyotumiwa kufanikisha uchunguzi huu.

1.8.1 Ubaada-ukoloni

Katika mwaka wa 1950, Frantz Fanon aliandika kitabu kiitwacho *Black Skins White Masks* ambako katika utangulizi wake alionyesha jinsi mtu mweusi amelazimika na kulazimishwa kubuia ujidunishaji na kujidharau hadi kufikia kiwango cha kujichukia na kutamani mtu mweupe. Baadaye katika mwaka wa 1963, aliandika kitabu kiitwacho *The Wretched of the Earth* ambako alionyesha jinsi mataifa ya Kimagharibi yanavyoyabagua mataifa yaliyotawaliwa. Kwa mfano, anaeleza kuwa Mfaransa alibuni nadharia za kusisitiza uovu wa Mwafrika, hasa Afrika Kaskazini kijumla na haswa Mwaaljeria. Nadharia hizi zilidai kuwa Mwaljeria ni mtu aliyezaliwa muongo, mwizi, asiyetii sheria na anayefurahia kuua bila sababu. Baadhi ya picha nyinginezo zilizoonyeshwa kumhusu Mwafrika kijumla ni kuwa hana hamu ya kujifunza mambo mapya kama inavyoonekana katika mtoto wa Kizungu. Mwafrika alisawiriwa kama mtu asiyeweza kuchanganua masuala ili kupata picha pana na kwamba hupenda kuzua ajali sana. Fanon alidai kuwa picha hizi hasi ziliaminiwa hata na wasomi kwa sababu zilipitishwa katika mfumo wa kielimu hasa vyiuni.

Maoni ya Fanon, yametufaa katika kazi hii kwa sababu kuwepo kwa picha hizi hasi kumezifanya nchi zilizoendelea kuchukulia mataifa machanga kama yasiyo na umuhimu mkubwa katika Ulimwengu. Kwa sababu hii, yanaendeleza unyonyaji wa kiuchumi na kisiasa dhidi ya mataifa

haya machanga. Kiini cha kazi yetu ni kuonyesha mbinu za unyonyaji huu ambao unaendeleza ukoloni mamboleo.

Said (1977) anasema kuwa nchi za Kimagharibi hazikutumia tu nguvu kuzimiliki koloni zao bali pia semi na kauli za kumdunisha mtawaliwa. Kwa mfano, anadai kuwa Mmagharibi alimchukulia Mmashariki kama mtu mzembe, asiyewajibika na mkosa maadili haswa katika masuala ya jinsia. Kulingana na Said, mataifa ya Kimagharibi yaliendeleza picha hizi ili kuendeleza kampeni za kijeshi au kama njia ya kutetea kukaa kwao katika nchi zilizotawaliwa.

Aidha, maovu ya watawala hayakuondoka hata baada ya uhuru kupatikana bali masalio ya utawala wa kikoloni yanajidhihirisha siku hizi kupitia mafarakano, ufisadi, vita vya wenyeji kwa wenyeji na mapinduzi ya serikali. Said pia analaumu vyombo vya habari vya Kimagharibi, siasa na wasomi wa Kimagharibi kwa kushadidia picha hizi hasi kumhusu Mmashariki. Anawalaumu pia wasomi wa nchi za kiarab waliozibuia picha hizi na kuyakubali mawazo ya Wamarekani na Waingereza kuhusu nchi za Kimashariki. Said (1993), hawalaumu tu wakandamizaji wa kikoloni bali pia viongozi wa nchi zilizotawaliwa. Kwa mfano, anadai kuwa ingefaa nchi za Asia, Afrika na Marekani ya Kusini kuwalaumu viongozi wao kwa kuuendeleza ukoloni mamboleo. Anadai kuwa viongozi hawa waliendeleza ukandamizaji na dhuluma kwa wananchi wenzao na kuwabagua kidini na kirangi (1993). Kama tutakavyoona katika tamthlia tulizoteua, viongozi wengi wa Kiafrika ni washirika wakuu katika kuendeleza ukoloni mamboleo. Katika kitabu hiki, Said anaonyesha pia kuwa picha hasi hazikuendelezwa kuhusu mmashariki pekee, bali pia kuwahusu Waafrika, Wahindi na Wamarekani wa Kusini.

Wamitila (2002) anasisitiza kuwa ingawa Said anazungumzia raia wa maeneo ya Mashariki, tunapaswa kuziangalia dhana hizi kwa upana, kwani picha hasi pia zimetumiwa na mataifa ya Ulaya kuwahusu Waafrika kwa kipindi kirefu. Mwelekeo huu utatufaa hasa katika kuonyesha uhusiano uliopo baina ya nchi za Kiafrika na mataifa ya Ulaya.

Mwandishi huyu anatambua kuwa mawazo ya Said ni msingi mkuu katika kuangalia ubeberu wa kibepari unaotawala ulimwengu siku hizi. Katika utafiti huu tumeonyesha jinsi mataifa kama vile

Marekani, Ulaya, Ujapani na Uchina (katika karne ya ishirini na moja) yanavyoendeleza ukoloni mamboleo kupitia ubepari wao.

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa uhakiki wa ubaada-ukoloni huchunguza uhusiano baina ya nchi tawala na nchi zilizotawaliwa, na kufichua unafiki uliopo. Waandishi hawa wanatambua mikondo miwili ya nadharia hii. Wanadai kwamba Kuna mkondo unaoendelezwa na Said , Bhabha na Spivak. Mkondo huu unawakilisha tahakiki ya kauli za kikoloni kutokana na msimamo usiokuwa wa nje wala ndani ya usomi wa kikoloni. Tahakiki hii hurejelea kauli za kiasili kwa njia isiyomakinika wala kujidhihirisha waziwazi. Tahakiki zao zinaonekana kudai kuwa juhudi za utandawazi na usomi wa Kimagharibi hazitafua dafu kwa sababu ndani mwa mataifa yaliyotawaliwa mna usomi wenye kina kisichoweza kueleweka na wasomi wa Kimagharibi. Mkondo huu unaonyesha namna udhibiti wa tamaduni wa nchi za Magharibi unavyovunjwa na miigo na takriri za nchi tawaliwa. Bhabha anasisitiza kuwa uwasilishaji wa kauli za kikoloni zenye nguvu si wa moja kwa moja kwa sababu unaingiliwa kati na kauli nyingine asili. Maingiliano haya yamesababisha kuwepo kwa utamaduni mseto.

Kulingana na Njogu na Chimera, mkondo wa pili ni wa moja kwa moja na wenye matumaini. Unadai kuwa watawaliwa walilazimishwa kujifunza lugha za kikoloni kwa sababu lugha za kienyeji zilinyimwa nafasi ya kukua na baadhi zikakufa (ukandamizwaji wa kitamaduni). Mkondo huu unasherehekea kurejea kwa kauli za watawaliwa. Yaani nchi zilizokuwa chini ya mkoloni zilionyeshwa zikiukabili utamaduni wa kigeni kwa kuutetea utamaduni wao asili. Hatimaye panatokea utamaduni mseto wenye sauti za kutoka nchi zilizotawaliwa. Kwa mujibu wa mkondo huu, nchi zilizotawaliwa zinatoa sauti zake imara. Sauti hizi zinawakilisha ujitambulishaji tofauti unaokinzana na ujitambulishaji uliolazimishwa na ukoloni.

Kutokana na mitazamo mbalimbali ya nadharia ya ubaada- ukoloni, mihimili ifuatayo inajitokeza:

Kwanza, lugha za Kimagharibi kwa nchi zilizotawaliwa ni juhudi za kutweza mchango wa nchi zilizotawaliwa katika kueleza mazingira yao. Ulazimishaji wa lugha za kigeni kwa watawaliwa uliwaelekeza katika ujifunzaji wa utamaduni wa kigeni. Hali hii, iliwakengeusha Waafrika wakawa wanaenzi lugha za ugenini na kuchukua zile zao. Ukoloni mkongwe ulihakikisha kuwa

lugha za kiasili hazipewi nafasi ya kukua. Kwa sababu hii, lugha nyingi zilififia. Kwa upande mwingine lugha za kikoloni ziliendelezwa kimatumizi hasa kupitia mfumo wa elimu. Mhimili huu umetusaidia kuchunguza ni kwa nini baadhi ya wahusika wanatumia lugha ya Kingereza katika mazungumzo yao (tamathali ya kuchanganya msimbo na kuhamisha msimbo) katika tamthilia tunazohakiki.

Pili, unyamazishwaji ni uti wa mgongo katika uhakiki wa ubaada-ukoloni. Hali hii hurejelea aina mbali mbali za ukandamizwaji wa watu waliotawaliwa. Kuna ukandamizwaji wa watu waliotawaliwa kokote walipo, wanaume kwa wanawake na ukandamizwaji wa wanawake unaoendelezwa na wanaume wenzao kando na kudhulumiwa na wakoloni. Hali hii huitwa “ukoloni maradufu”. Mhimili huu unatuwezesha kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo umekandamiza utamaduni wa Kiafrika hadi kufikia kiwango cha kumkosesha Mwafrika kitambulisho. Vile vile, tutachunguza mbinu zinazoendeleza ukandamizwaji (unyamazishwaji) wa mataifa machanga katika tamthilia teule za Kiswahili.

Tatu, Kuna utengano wa kimataifa kwa misingi ya ‘Sisi-waliostaarabika’ na ‘Wao-wengine/washenzi’ ambapo Wachina, Waarab na Waafrika husawiriwa kama waovu, wadanganyifu, wasioaminika, wazinifu na waliopotoka huku wananchi wa Kimagharibi nao wakijisawiri kama wenye huruma, wakamilifu, waaminifu na waadilifu. Hali hii huitwa ‘wingine’. Mhimili huu ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu hisia hizi zimeyafanya mataifa yaliyoendelea kujichukulia kuwa bora kuliko mataifa machanga. Tunachukulia kuwa hii ndio sababu yanaendeleza unyonywaji wa kiuchumi kwa mataifa machanga. Mwelekeo huu umetuwezesha kuchambua maudhui ya ukoloni mamboleo hasa utengano wa kimataifa na athari zake kama inavyoonekana katika tamthilia za Kiswahili.

Nne, kuna uibukaji wa utamaduni mseto/umahuluti - kutokana na masalio ya athari za ukoloni mkongwe, kunatokea mchanganyiko wa utamaduni asili wa mtawaliwa na utamaduni wa mtawala, mambo ambayo yamekuwa vigumu kutenganisha waziwazi. Padley (2006) anadai kuwa hii ni kwa sababu watawala hasa Waingereza waliweza kujikita katika maisha ya kila siku ya mtawaliwa kupitia elimu, utawala na kiutamaduni. Mhimili huu umetufaa katika kuchunguza hulka za wahusika na vichocheo vya hulka hizo katika tamthilia tunazohakiki. Pia tukitumia

mhimili huu tumeweza kuchambua jinsi wahusika wanavyotumia lugha na sababu za matumizi hayo katika tamthilia teule za Kiswahili.

1.8.2 Elimumitindo na Nguzo zake

Wamitila (2003) anaeleza kuwa elimumitindo ni dhana inayotumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi na uchanganuzi wa jinsi mbali mbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Elimumitindo huhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi za kifasihi na zinazomtambulisha mwandishi. Taaluma ya elimumitindo humsaidia mhakiki kuchunguza maudhui ya msanii na lugha ambayo huwasilisha maudhui hayo. Mawazo haya ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu kando na kuchunguza maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia teule, tumechunguza pia mchango wa lugha katika uwasilishaji huo.

Taaluma ya elimumitindo iliwekewa misingi yake na Buffon (1930) ambaye alidai kwamba mtindo ni mtu mwenyewe, yaani jinsi mtu anavyotumia lugha kupitisha ujumbe wake. Mawazo haya yaliendelezwa na Coombes (1953) ambaye alifafanua kwamba ili kuchanganua mtindo katika kazi ya kifasihi ni lazima kuchanganua vipengele vinavyoifanya kazi hiyo ivutie. Vipengele hivyo ni kama vile uteuzi wa maneno, matumizi ya taswira, urari wa vina na mahadhi ya mashairi. Utafiti wetu ulinufaika kutokana na mawazo ya Buffon kwani kwa kuchunguza matumizi ya lugha na uhusika katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* tumedhihirisha mtindo wa Timothy Arege.

Wazo kuu la taaluma hii ni kwamba kazi ya kifasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Jinsi mtunzi anavyoitumia lugha ndivyo anavyofaulu katika kutoa ujumbe wake kwa wasomaji. Kwa sababu hii, lugha ndiyo nyenzo kuu ya mawasiliano katika jamii zote za wanadamu (Leech, 1969). Wanamtindo husisitiza umuhimu wa lugha kama chombo kitekelezi kinachosaidia katika kuelewa maudhui yaliyokusudiwa. Wanasisitiza kuwa vipengele vya kiisimu hutumika kueleza jinsi lugha hutumika. Vipengele hivyo ni kama vile fonolojia, morfolojia, semantiki na sintaksia. Taaluma hii inachukulia kuwa unapobadili kipengee kimoja kama vile kile cha uteuzi wa maneno au muundo wa sarufi, mtindo nao unabadilika.

Elimumitindo husisitiza uwiano kati ya ujumbe na lugha kwa sababu lugha huchangia ufanisi wa kazi ya sanaa kwani hutumiwa katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi. Huu ndio msingi unaotuwezesha kuhakiki matumizi ya lugha katika tamthilia teule.

Leech (1969) anasema kuwa kazi ya fasihi hucusudia kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa wasomaji au wasikilizaji. Anadai pia kuwa, kazi za kisanaa huchambuliwa kwa kuangalia mitindo ya mwandishi. Alifafanua kwamba muundo wa kazi ya kifasihi ni muhimu katika kupitisha ujumbe. Kwa mfano, akirejelea mashairi, anasema kuwa ni vizuri kuchunguza jinsi msitari mmoja ulivyonganishwa na mwingine, ubeti na mwingine au wazo na lingine. Anaeleza kuwa lugha ya kifasihi nayo ina muundo wake uliosheheni vipengele kama vile usambamba, urudiaji, tanakali za sauti na ukiushi wa aina mbalimbali. Leech anatambua ukiushi wa kileksika, kifonolojia, kisemantiki kisintaksia na hata ukiushi wa kipindi cha kihistoria kiuandishi. Mawazo ya Leech yametufaa katika kuchunguza viwango mbali mbali vya ukiushi katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kijiba cha Moyo*.

Leech na Short (1981) wakimrejelea Aristotle na Plato wanaeleza kuwa yaliyomo na jinsi yanavyowasilishwa ni kama mwili na roho. Hii ina maana kuwa maudhui na namna yalivyowasilishwa ni mambo mawili yanayotegemeana na kuathiriana. Hii ndio sababu utafiti huu umekusudia kuchunguza vipengele vya fani vya uhusika na matumizi ya lugha na kuonyesha mchango wake katika kukuza maudhui ya ukoloni mamboleo. Vipengele vya kimtindo vya uhusika na matumizi ya lugha vitatufaa zaidi katika kuonyesha udhihirishaji wa maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kijiba cha Moyo*. Ifuatayo ni baadhi ya mihimili iliyofuatwa katika utafiti huu:

1) Kazi ya fasihi hueleweka kwa kuchunguza sifa za lugha aliyotumia mtunzi katika kuwasilisha maudhui yake. Mhimili huu utatufaa katika kuchunguza jinsi kipengele cha mtindo cha uhusika na wahusika kilivyotumika ili kufanikisha maudhui katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kijiba cha Moyo*.

2) Ukiushi hujitokeza katika viwango mbalimbali vya lugha. Kwa mfano kuna ukiushi wa kifonolojia, kisemantiki, kileksika na kisarufi. Kando na aina hizi, Leech (1969) anazungumzia pia ukiushi wa kipindi fulani cha kihistoria. Utafiti wetu unajikita katika kuchunguza ukiushi wa kisemantiki ambapo tutaonyesha tamathali za lugha zinazokuza maudhui ya ukoloni mamboleo

katika taamthilia teule za Kiswahili. Pia tutachunguza ukiushi wa kileksika unavyojitokeza katika tamthilia teule. Ukiushi wa kisemantiki huhusu matumizi ya lugha kwa njia inayoleta maana za ziada au zisizozoeleka. Ukiusha huu umejidhihirisha kupitia matumizi ya mbinu za lugha kama vile kinaya, sitiari, udamisi, tanakuzi, dhihaka na nyinginezo. Ukiushi wa kileksika huhusu matumizi ya maneno kwa njia inayokiuka ukawaida. Ukiushi huu ulizingatiwa katika kuchunguza uteuzi wa maneno ya mwandishi na matumizi ya uhamishaji msimbo.

Chapman (1973), akinukuliwa na Mbatiah (2012) anasema kuwa ukiushi ni matumizi ya kiisimu yanayochukuliwa kukosa ukawaida unaotarajiwa na watumizi lugha. Mbatiah katika makala iitwayo “*Deviation as a Communicative Strategy in Gamba la Nyoka*” katika Swahili Forum 19 (2012:117-126) anajadili aina nne za ukiushi ambazo ni: Ukiushi wa kisarufi, ukiushi wa kileksika, ukiushi wa kisemantiki na ukiushi wa kifonolojia. Henry Indangasi (1988:94) akinukuliwa na Mbatiah katika makala hii anasema kuwa ukiushi wa kisemantiki ndio hujitokeza mno katika kazi za kifasihi. Ukiushi huu hujitokeza kupitia mbinu kama vile sitiari, tashbihi, kwelikinzi, chuku, oksimora, metonimia, sinekidoki na tashhisi. Kwa muktadha huu, mawazo haya yametufaa katika kuchunguza baadhi ya tamathali hizi katika tamthilia teule. Ukiushi wa kileksika nao umetufaa kuchunguza matumizi ya maneno ya kigeni katika tamthilia tulizoziteua. Kwa hivyo, mhimili huu ni muhimu sana katika utafiti huu kwa sababu umetusaidia kuzungumzia ukiushi wa kisemantiki na wa kileksika (Tamathali za lugha kama vile kinaya, uzungumzi nafsi, kuchanganya ndimi, jazanda na nyiginezo)

1.9 Mbinu za utafiti

Kwa kiasi kikubwa utafiti wetu ni wa kimaktaba. Kwa sababu hii, sehemu kubwa ya utafiti huu ilifanyika maktabani. Tulisoma tamthilia zote mbili tukitilia maanani suala la ukoloni mamboleo huku tukiongozwa na maswali ya utafiti pamoja na malengo ya utafiti huu. Tulisoma tasnifu mbalimbali kuhusu tamthilia, vitabu mbalimbali vinavyozungumzia mada yetu, magazeti na majarida ya lugha na fasihi kama vile *Kiswahili Forum*, *Kiswahili*, *Mulika* na *Mwamko*.

Vile vile tumejadiliana na kuelekezwa kwa kina na wahadhiri wasimamizi wa kazi hii, wahadhiri wengine wa idara ya Kiswahili na wanafunzi wenzetu. Zaidi ya hayo, tumerejelea tovuti mbalimbali kama vile w.w.w.swahilihub.com. Uchanganuzi wa data ya utafiti huu ulifanywa

kimaelezo. Data iliyopatikana maktabani ilichanganuliwa kimaelezo kwa kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na nadharia ya ubaada-ukoloni.

1.10 Hitimisho

Sura hii imetoa utangulizi wa pendekezo la utafiti kwa kuanzia kwa kuliweka wazi suala la utafiti huu ambalo ni: Maudhui ya ukoloni Mamboleo katika tamthilia teule za Kiswahili na uwasilishaji wake. Jambo lingine tulilolishughulikia ni kubainisha sababu za kuchagua mada hii. Aidha, tumeonyesha upeo na mipaka ya utafiti wetu. Pamoja na hayo, tumejadili kwa kina misingi ya nadharia tulizozitumia kwa kuzingatia waasisi wa nadharia hizo na mihimili yake muhimu.

Mwishowe tumerejelea maandishi mbali mbali kama vile tasnifu za wasomi na wahakiki mbalimbali, vitabu vya fasihi, magazeti na majarida kadhaa ili kuonyesha ufaafu na udhaifu wa yale yaliyoandikwa kuhusu mada ya ukoloni mamboleo.

Mbinu za utafiti tulizozitumia kutafitia mada hii pia zimeonyeshwa. Tunasadiki kwamba sura hili imekuwa msingi thabiti kwa kazi nzima. Sura inayofuata inaangazia suala la ukoloni kwa kuoanisha ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Hapa, tumeonyesha jinsi waandishi wa fasihi ya kiasia na hasa wa Kiswahili walivyolizungumzia tatizo la ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo.

SURA YA PILI MAANA YA UKOLONI

2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tulitanguliza mada ya utafiti huu ambayo ni maudhui ya ukoloni mamboleo na uwasilishaji wake katika tamthilia za *Mstahiki Meyu* na *Kijiba cha Moyo*. Katika sura hii, tutashughulikia swala la ukoloni. Kwa kufanya hivi, tutakuwa tumeweka msingi thabiti wa uchunguzi huu kwa sababu unahusu ukoloni mamboleo katika tamthilia za Kiswahili.

Ukoloni ni tukio la kihistoria ambalo litakuwa vigumu kulifuta katika maisha ya Waafrika. Ni vigumu kwa hivyo, kuzungumzia historia ya bara la Afrika bila kurejelea mada ya ukoloni. Hii ni kwa sababu mkoloni aliathiri maisha ya Mwafrika kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata ikiwa fasihi za miaka ya awali kuhusu swala la ukoloni ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza, waandishi wa Kiswahili nao hawajaachwa nyuma katika kuliangazia tatizo hili. Kama anavyosema King’ei (1999), kuwepo kwa fasihi iliyohusu ukoloni kwa wingi kulichangiwa na kutukuzwa kwa lugha za kigeni na kutwezwa kwa Kiswahili na lugha nyinginezo za Kiafrika.

Kwa kuwa swala la ukoloni ni pana na lenye historia ndefu, tumelichunguza katika awamu mbili kuu ambazo ni ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Tumeonyesha sifa muhimu za kila awamu hasa zile tulizoweza kurejelea katika tamthilia *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meyu*.

2.2 Ukoloni Mkongwe

Sharma (2015) anafafanua kwamba kuna nadharia tatu zinazoeleza chimbuko la ukoloni. Kwanza, anataja nadharia ya kiuchumi inayosema kuwa mataifa ya Kimagharibi yalikuwa na msukumo wa kuvamia mataifa mengine kwa kuvutiwa na rasilimali za kiasili za maeneo hayo. Kwa sababu hii kuanzia karne ya kumi na tano mataifa ya Kimagharibi yalianza kunyemelea maliasili ya mataifa machanga ili kujifaidi kiuchumi. Nadharia ya pili inahusu maadili. Msingi mkuu wa nadharia hii ni dhana ya Kipling iliyojulikana kama “mzigo wa mtu mweupe”. Mwelekeo huu unadai kuwa mtu mweupe alijihisi kuwa yeye ni bora kimaadili na mwenye nguvu na uwezo kuliko watu wengine duniani na kwa sababu hii akachukulia kuwa ni jukumu lake kueneza maadili hayo kwa watu wengine ili kuwastaarabisha. Sharma anasema kuwa mtu mweupe alichukulia kuwa mtu wa rangi nyingine isiyokuwa nyeupe ni kama mnyama na

kuwadhibiti wanyama ni lazima nguvu zitumike. Vivyo hivyo, kumdhibiti mtu wa rangi nyingine isiyokuwa nyeupe ilibidi kutumia nguvu hasa dhuluma za kichapo.

Nadharia ya tatu inatokana na mawazo ya Mohandas Gandhi. Nayo inahusu usambazaji wa maarifa. Katika mkakati huu watu weupe walikusudia kuleta mifumo yao ya kielimu, kisheria na kisiasa kwa mataifa yaliyokosa vitu hivyo. Huu ndio msingi mkuu unaotumiwa na baadhi ya wahakiki wanaosisitiza kuwa ukoloni ulilifaa bara la Afrika kwa kuwaletea Waafrika maendeleo ya kiteknolojia na kielimu. Wahakiki hao hudai kuwa ukoloni kwa mfano umewakwamua Waafrika kutokana na giza la imani na itikadi potovu.

Wageni kama vile Wagiriki, Wachina, Waroma, Wareno, Waingereza na Wafaransa walianza kulitembelea bara la Afrika katika karne ya kwanza (Kiruthu, Kapiyo na Kimori, 2011). Kulingana na waandishi hawa, wageni hawa walijia biashara, ingawa baadaye walianza kuja kwa sababu za kitalii, kueneza dini ya Kikristo na kuwastaarabisha watu wa bara la Afrika. Hata hivyo ni katika kipindi cha mwisho wa karne ya kumi na tisa ambapo Wazungu walifika kwa wingi barani Afrika. Wakati huu mataifa ya Kimagharibi yalianza kushindania bara la Afrika kwa sababu za kiuchumi (ubepari wa kiviwanda) na kisiasa. Wanafafanua kwamba kuligawa bara la Afrika kirasmi kulifanyika katika mkutano wa Berlin mwaka wa 1884.

Lengo kuu la kuligawa bara la Afrika miongoni mwa Wazungu hao lilikuwa ni kupata malighafi ya viwanda vyao. Katika kusaka malighafi hayo, Wazungu waliishia kunyakua maliasili ya Kafrika kwa nguvu au kwa njia za kijanja. Harakati hizo ziliendeleza dhuluma na ukandamizaji kwa wenyeji. Ukandamizwaji huu uliwapa Waafrika kariha ya kubuni fasihi iliyoonyesha maovu hayo. Hata hivyo, ilichukua muda mrefu kwa Mwafrika kuanza kukosoa uovu huo kimaandishi kwani hakuwa na elimu. King'ei (1999) anasema kuwa baadaye katika miaka ya 1950, waandishi wa Kiafrika kama vile Shaaban Robert na Ibrahim Hussein walianza kutunga fasihi ya kufurahisha na kuasa wasomi, waliojipatia elimu ya kigeni. Wasomi wengi nyakati hizo walikuwa wamisheni, watawala na watumishi wa kiserikali.

Kulingana na maoni ya mwandishi huyu, fasihi za mwanzo mwanzo hata kama ziliandikwa wakati wa ukoloni hazikupinga ukoloni moja kwa moja. Anatoa mfano wa kazi kama vile *Adili*

na *Nduguze* (1952) ambayo imefanikiwa zaidi katika kuburudisha. Kazi hii hata hivyo haikuzungumzia burudani tu bali pia ilizungumzia masuala mazito kuhusu uongozi. Hata hivyo, kazi hii haikuzungumzia suala la ukoloni ilhali iliandikwa wakati wa ukoloni.

Nchini Kenya tamthilia za mwanzo mwanzo zilijitokeza kwanzia miaka ya 1950 ingawa nazo pia zililenga kuburudisha tu. Kwa mfano, Graham Hyslop aliandika michezo miwili ya kuigiza ambayo ni *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu* mwaka wa 1957 huku Mwafrika aliyekuwa mwanafunzi wake, Henry Kuria, akiandika na kuchapisha tamthilia yake mwaka wa 1957 iitwayo *Nakupenda Lakini*. Hata baada ya ongezeko hili la kimaandishi, pingamizi dhidi ya ukoloni bado hazikujitokeza wazi wazi. Jambo hili laweza kuwa lilitokana na ukweli kuwa hakukuwa na wasomi wengi wa Kiswahili na wachache waliokuwepo nao wakakumbwa na matatizo ya kuwapata wachapishaji ambao wangekubali kazi kama hizo. Hata hivyo kipindi cha ukoloni mkongwe kilishuhudia baadhi ya kazi za kifasihi zilizokosoa ukoloni. Baadhi ya kazi hizo ni:

Utenzi wa Maji Maji. Kazi hii inaonyesha jinsi Vita vya Maji Maji vilivyowaathiri Waafrika wakati wa vita kati ya Wajerumani na Watanganyika baina ya miaka 1905-1907. Waafrika walipowavamia Wajerumani mwaka wa 1905 walishindwa kufanikiwa kwani maji ya kiongozi wao Kinjekitile hayakuwakinga dhidi ya risasi za Wajerumani. Utenzi huu unaangazia dhuluma za wakoloni dhidi ya Waafrika ambazo ni kama vile mauaji, ulipaji wa kodi na ajira ya kulazimishwa kama vile kuwajengea barabara Wazungu na kuwalimia pamba.

Kazi nyingine inayoonyesha jinsi wakoloni wa Kijerumani walivyowatesa Waafrika ni tamthilia ya Ebrahim Hussein ya *Kinjekitile*. Katika tamthilia hii, Kinjekitile anawaunganisha watu wa makabila mbalimbali kama vile Wazaramo, Wamatumbi, Wamakonde, na Wangoni katika vita dhidi ya Mjerumani. Dhuluma za kikoloni wanazolalamikia Wafrika katika tamthilia hii ni kama vile kufanyishwa kazi za sulubu bila malipo, kunyang'anywa mabinti na wake zao, kunyakuliwa kwa mashamba na kutozwa kodi na mkoloni. Kwa mfano, mazungumzo yafuatayo baina ya Mkichi na Mgindo yanaonyesha hali hii:

Mkichi: Kuliko kukaa hivi tunatawaliwa, tunalimishwa kama wanyama.
Njaa moja kwa moja kwa maana hatuwezi kulima. Tunamlimia
Bwana Kinoo tu. Afazali kufa kama maisha haya. Udongo

Mwekundu bado yupo nchini kwetu. Bado zaidi amechukua nchi yetu. Anatulimisha kwa nguvu sisi tunatazama tu. Anatudai kodi. Sisi tunatazama tu. Ilikuwa sisi tudai yeye kodi, lakini apana. Sisi kama wanawake tumekaa tumetazama. Kumtazama huku mpaka lini?

Mgindo: Tumuondoe.....tukate shauli sasa hivi...vita. Akuna jingine (uk.7)

Tukichunguza malalamiko ya wahusika hawa, ni wazi kwamba Mzungu ameichukua ardhi yao na kuwaacha baadhi wakiwa maskwota katika nchi yao. Pili, Mjerumani amewadhulumu wafanyikazi ili kujinufaisha yeye binafsi na nchi yake. Mbatiah (2016) anasema kwamba baadhi ya mambo yaliyowaudhi Waafrika zaidi ni kilimo cha pamba ambacho kilikusudiwa kuimarisha uchumi wa utawala wa Kijerumani. Vilevile Waafrika hawakupenda kuongozwa na maakida na majumbe walioteuliwa na Mjerumani. Mwandishi huyu anasema hii ni kwa sababu maofisa hawa aghalabu walikuwa Waarab na uhusiano baina ya Waarab na Waafrika katika sehemu nyingi ulikuwa mbaya tangu enzi ya biashara ya utumwa. Mkoloni popote alipoenda alihakikisha kwanza amemiliki mbinu za kimsingi za uzalishaji mali zikiwemo ardhi na umiliki wa wafanyikazi. Hii ndio misingi ya kibepari iliyowasukuma Wazungu kuja barani Afrika ili kuhakikisha ufanisi wa chumi zao. Dhuluma za ubepari huu zinawakosesha baadhi ya wananchi matumaini katika maisha. Hii ndio sababu Mkichi katika nukuu la hapo juu anasema, “Afazali kufa”

Kuhusu tatizo la ulipaji kodi, mwandishi anawakejeli wakoloni kwa kuendeleza dhuluma hii akionyesha kuwa mkoloni ndiye kwa hakika aliyestahili kumlipa Mwafrika kodi kwa kutumia shamba lake kujitajirisha. Hali hii inaonekana katika maneno ya Mkichi anaposema...“Ilikuwa sisi tudai yeye kodi lakini hapana”(uk.4). Kutokana na muktadha huu, ni dhahiri kuwa njia moja iliyotumiwa na mkoloni kuendeleza utawala wake barani Afrika ni unyakuzi wa ardhi na unyanyasaji wa wafanyikazi. Hii ni mbinu mojawapo iliyotumiwa na wakoloni ili kuendeleza utawala wao barani Afrika. Mbatiah (2016) anaonyesha kuwa njia na mbinu mbalimbali zilitumika katika kuendeleza ukoloni na kuwadhibiti Waafrika. Mbinu anazofafanua ni kama vile matumizi ya sheria kandamizi kama vile kodi ya kichwa, ubebaji wa kipande, unyakuzi wa ardhi na unyanyasaji wa wafanyikazi. Anasema:

Ili kuhakikisha kwamba mashamba ya Wazungu hayakukosa wahudumu, kodi mpya ilianzishwa ili kuwalazimisha Waafrika kufanya kazi katika mashamba hayo. Hii ilijulikana kama kodi ya kichwa. Waafrika ambao sasa hawakuwa na ardhi walikatiwa viwanja katika mashamba ya Wazungu

ili waweze kulima na kupanda mimea ya chakula. (uk.19)

Kama tutakavyoonyesha katika sura ya nne, hizi ni njia kuu zinazotumiwa na viongozi wa nchi huru za Kiafrika katika kuwadhulumu wananchi wao. Kwa hivyo wanatumia mbinu za kikoloni katika kutawala mataifa yao. Kwa kufanya hivyo wanaendeleza ukoloni mpya (ukoloni mamboleo).

Kulingana na tamthlia hii, mbinu nyingine iliyotumiwa na mkoloni katika kuendeleza utawala wake barani Afrika kwa muda mrefu ni ile ya ubarakala pamoja na sera ya tenga utawale. Kuna Waafrika ambao kwa sababu ya umaskini au tamaa na njaa waliwasaliti wenzao. Pia kuna baadhi ya jumuiia za Kiafrika ambazo zilikataa kuunga jumuiia nyingine mkono katika kumpinga mkoloni kwa sababu ya uadui wao wa kiasili. Njia za usaliti huo zinajitokeza wakati baadhi ya wananchi wanapoamua kuwapelekea Wazungu habari kuhusu mikutano ya wanaopanga vita dhidi ya mkoloni. Kwa mfano tunaona Kitunda akiwaonya wenzake hivi:

Kitunda: Sote sisi tunataka Njelumani aondoke. La kufanya ni kuanza kukusanya silaha-kuiba bunduki za askali, kufanya chini juu ili tupate silaha. Hili haliwezi kufanyika mala moja. Tena itakuwa ngumu maana sasa hivi kuna vibalaka chungu nzima. Utakachofanya akina askali au mnyampala keshasikia. Njaa inatufanya tuuzane. (uk.10)

Mzungu anawanasa baadhi ya Waafrika kwa hela ili watumike kama vibaraka wake. Kuna wale wanaompelekea habari kisiri hasa zile zinazohusiana na mipango ya vita. Tatizo hili la usaliti linazua hali ya kutoaminiana baina ya makabila mbali mbali na hiki kinakuwa kikwazo kikubwa katika vita vya ukombozi. Hali ya kutoaminiana inajengeka pia baina ya watu wa kabila moja. Mkoloni alifahamu kuwa Waafrika wakikosa umoja ingekuwa rahisi sana kwao kuendelea kuwataala. Wazungu walitumia mbinu ya tenga-tawale ili kupunguza upinzani kutoka kwa Waafrika. Mbinu hii ilihusu kuwapendelea baadhi ya Waafrika na kuwatumia katika harakati za kiutawala dhidi ya Waafrika wenzao. Huku baadhi wakipewa nyadhifa kama vile uchifu wengine walitumika kukusanya habari kuhusu harakati za ukombozi na kumpelekea mkoloni. Jambo hili lilikwamiza juhudi za kuungana kwa makabila mengi ili kumkabili adui ambaye alikuwa mkoloni. Hii ndio sababu tunaona Mngindo akisema kuwa mtu akipeleka habari Kilwa anapewa pesa kutoka kwa Udongo Mwekundu (Mkoloni).

Katika *Mukwava wa Uhehe*, mwandishi anaangazia jinsi jamii ya Uhehe ilvyoathiriwa na ukoloni. Kwa mfano, anasema kwamba uharibifu wa mali uliosababishwa na wakoloni ulizidi ule uliokuwa ukisababishwa na vita baina ya makabila. Hii ndio sababu mhusika Semulia anaviita vita vya kikabila, “Msugvano tu baina ya ndugu”. Vita vya Wazungu dhidi ya Waafrika vilipita mipaka na ndio sababu Mukwava anaomba usaidizi wa majirani ili kuweza kumkabili Udongo Mwekundu. Pia anakataa kutafuta suhulu na Udongo Mwekundu kama walivyofanya viongozi waliomtangulia. Aneleza:

Mukwava : Sote tunapenda amani na utulivu, lakini vita ni vita.
Hatutaki kupigana, lakini tunalazimishwa kupigana.
Hatumvamii mtu, sisi ndio tunaovamiwa kila vita vya kivamizi.
Kiini chake ni dhuluma.(uk.31)

Kulingana na nadharia ya ubaada-ukoloni na ambayo unaongoza utafiti huu, watu wa mataifa ya Kimagharibi huchukulia kuwa wao ni bora kuliko wale wa Mashariki na Afrika. Hiki ni kisingizio tu ambacho wakoloni walitumia ili kutetea kuja kwao barani Afrika. Walidai kuwa wangeleta ustaarabu wa Kimagharibi ili kumboresha Mwafrika kimaadili. Vile vile, picha hizi hasi walizo nazo Wazungu dhidi ya Mwafrika, ziliupa nguvu msingi wa ubaguzi wa rangi ulioendelezwa na mkoloni. Katika tamthilia hii, tunaona gavana mmoja wa Kijerumani akionyesha ubaguzi wa rangi wazi wazi kwa maneno yafuatayo:

Gavana: Imekwisha thibitishwa kuwa ustaarabu wetu wa Kizungu, hasa Kijerumani ni bora kuliko jadi zote duniani. Kwa hiyo Sisi Wazungu tunalo jukumu la kuyastaarabisha mataifa mengine ambayo bado yanatawaliwa na nguvu za giza yapate kuona mwangaza. Huu ndio mzigo wa mtu mweupe. (uk.34)

Wafula (1999) anakiri kwamba Wazungu walikuwa na imani na falsafa kama hizi walizotumia kama nguzo ya kuanzisha ukoloni katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa. Curtin (1964) akinukuliwa na Wafula (1999) anasema kuwa Wazungu kama vile David Hume waliamini kwamba binadamu wa rangi mbalimbali walizalika kutoka kwa wazazi wenye asili tofauti. Dai hili ndilo linaloeleza tofauti za kisayansi na kiteknolojia katika jamii mbalimbali. Wafula pia anailaumu Bibilia kwa kuhalalisha ubaguzi wa kikoloni. Kwa mfano, anasema katika Kitabu cha Mwanzo sura ya tisa, kuna kisa cha Nuhu. Nuhu anamlaani mtoto wake aliyemchekelea alipokuwa mlevi. Inasemekana kuwa adhabu aliyopata mtoto huyu ni kupata nywele ngumu na kuwa mweusi.

Tathmini ya mawazo ya mwandishi huyu inadhihirisha kuwa mkoloni alitumia dini katika kuelekeza utawala wake na kumdhibiti mtawaliwa kiakili. Biblia kwa hivyo ikawa chombo cha ukandamizaji hasa wa mtu mweusi. Tamthilia hii inaonyesha ukandamizwaji huo ulivyomkumba Mwafrika kupitia uvamizi wa Kijerumani hasa mauaji ya Waafrika waliojaribu kupinga utawala wa mkoloni pamoja na viongozi wao.

Ingawa tamthilia hizi zote ziliandikwa baada ya uhuru nchini Tanzania, zilijaribu kuchambua historia ya mataifa huru kwa kuonyesha mapambano ya Waafrika dhidi ya wakoloni. Zilionyesha ushujaa wa viongozi wa Kiafrika waliojitolea kuzikomboa nchi zao. Hii ni kinyume na jinsi wakoloni walivyojaribu kuonyesha kwani wengi wao waliwachora Waafrika waliopigania uhuru kama magaidi. Vile vile kazi hizi zinafafanua dhuluma zilizoendelezwa na mkoloni.

Waandishi wa Kenya nao pia hawakubaki nyuma katika kufafanua historia ya kikoloni na jinsi ilivyoathiri jamii zao. Mifano mizuri ni *Mzalendo Kimathi* ya Ngugi wa Thiong'o na Micere Mugo pamoja na riwaya ya P.M. Kareithi, *Kaburi Bila Msalaba* (1968). Tamthilia ya *Mzalendo Kimathi* inamulika mateso waliyopitia wapiganiaji wa uhuru na aliyekuwa kiongozi wa Mau Mau, Dedan Kimathi. Inafichua maovu ya nguvu za kikoloni zilizojidhihirisha kupitia polisi, wanajeshi, mahakama na vibarakala waliowaosaliti Waafrika wenzao kwa kujiunga na mkoloni. Kwa mfano, tamthilia hii inaonyesha jinsi mkoloni alivyowatuma watu mbali mbali kumshawishi Kimathi kuwachana na vita vya ukombozi. Kwanza kundi la Wahindi na Waafrika linamsihi akubali makosa, awaambie watu wake watoke msituni ili kuwe na amani na maendeleo. Badaye, kasisi, mwanasiasa na mfanyibiashara pia wanamwendea Kimathi kumshawishi zaidi.

Mfanyibiashara anapozungumza na Kimathi, anafichua kuwa serikali ya kikoloni imekuwa ikiendeleza ubaguzi wa rangi dhidi ya Mwafrika hasa katika maeneo ya umma. Hata hivyo, ili kumshawishi Kimathi kuwacha kupigania uhuru, wakoloni wanatumia propaganda kuwa kuna sera mpya ya ushirikiano katika maendeleo. Hii ilikuwa njia ya kumrai Kimathi kujiunga na watawala wa kikoloni na kuwasaliti Waafrika. Baadhi ya Waafrika walipotajiwa kuwa wangenunua mashamba yaliyokuwa ya Wazungu, walifurahia pasi kukumbuka kwamba mashamba hayo yalikuwa yao.

Kulingana na mazungumzo haya tunaweza kuona matatizo yaliyoletwa na wakoloni nchini Kenya ambayo ni kama vile unyakuzi wa ardhi, usaliti na ubaguzi wa rangi. Pia inadhihirika kwamba mbinu za hila, udanganyifu na tenga-utawale zilitumika sana katika utawala wa kikoloni. Katika tamthilia tunazozichunguza pia tutaonyesha ikiwa mbinu hizi bado zinatumiwa na mataifa ya Kimagharibi kuyadhibiti mataifa machanga au la.

Kareithi (1968) anafafanua harakati ya ukombozi dhidi ya mbeberu kupitia hadithi ya Mau Mau ambayo ni ya kwanza kuandikwa katika lugha ya Kiswahili. Anaonyesha gharama kubwa iliyolipwa na wapiganiaji wa uhuru nchini Kenya. Kwa mfano anaonyesha matatizo yaliyowakumba wapiganiaji wa uhuru kama vile kuishi katika makazi duni ya msituni, usaliti wa baadhi ya Waafrika hasa machifu na pia dhuluma za polisi kama vile kusakwa kwa wapiganiaji uhuru hasa nyumbani kwao. Hali hii ilisababisha hofu kuu katika maisha yao. Mwandishi akiliangazia suala la usaliti, anatoa mfano wa mhusika Karani ambaye alikuwa mweka hazina wa Mau Mau lakini akajigeuza kuwa jasusi wa mkoloni kwa sababu ya tamaa ya pesa.

Kando na matatizo kama haya ya usaliti, mwandishi anaonyesha dhuluma nyingizo zilizoendelezwa na mkoloni kama vile ubaguzi wa rangi katika uajiri wa wafanyikazi katika ngazi za utawala. Anaonyesha jinsi vyeo vya juu vyote vilivyomilikiwa na Wazungu huku Waafrika wakipewa vyeo vya ngazi za chini kama vile uchifu. Mzungu aliyekuwa wa ngazi ya chini kikazi ni mkuu wa taarafa (D.O). Katika nadharia ya ubaada-ukoloni kuna msisitizo mkubwa kuhusu ubaguzi unaoendelezwa na mataifa ya Kimagharibi dhidi ya watu wa maeneo ya Mashariki na Waafrika. Wakati wa ukoloni ubaguzi huu ulionekana katika utoaji wa ajira hasa vyeo vikubwa serikalini. Kwa sababu hii watu weusi hawakuaminiwa na vyeo vya juu kama vile vilivyoshikiliwa na Wazungu. Hii ndio sababu katika riwaya hii, tunaona mkoloni hamwamini Mwafrika na cheo kikubwa. Kwa mfano hakuna Mwafrika hata mmoja aliyepewa cheo cha mkuu wa taarafa.

Riwaya ya Kareithi inaonyesha ukweli wa mhimili wa nadharia ya ubaada-ukoloni unaohusu utengwaji kwa misingi ya ‘wao’ na ‘sisi’, ‘wao’ ikiwa ni wananchi wa mataifa machanga waliodhulumiwa na wliokosa ustaarabu huku ‘sisi’ ikiwa ni Wazungu waliojichukulia kuwa wao ni bora na waliostaarabika. Kama inavyoonekana katika dondoo za hapo juu, wakoloni

waliwazuga Waafrika akili wakachora picha ya mtu mweupe akiwa kama nusu-mungu katika akili zao. Hii ndiyo sababu mtu mweusi anamvulia kofia na kutubu mbele zake kama tunavyoona Karani akifanya katika riwaya hii...”Nataka kutubu na kusema kwa hakika mbele ya mungu sitahusiana na Mau Mau tena...”(uk. 71).

Athari za ukoloni pamoja na njia zilizotumiwa na wakoloni kujipenyeza katika mataifa ya Kiafrika yameangaziwa pia na Ngugi wa Thiong’o kwa kina. Historia kuhusiana na upiganiaji uhuru nchini Kenya inajitokeza wazi wazi katika riwaya ya *Usilie Mpenzi Wangu* (1964). Ngugi analisifu kundi la Mau Mau kwa kusema kuwa lilikuwa bora kuliko makundi yaliyowahi kupigania uhuru katika sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki. Njia moja iliyotumiwa na wakoloni kujipenyeza katika Nchi ya Kenya ni unyakuzi wa ardhi. Ngugi anaonyesha kuwa kitendo hiki kiliwachochea Waafrika kuanza kutumia nguvu kudai ardhi yao. Anatalia mkazo uhalisia wa kihistoria kuhusu ardhi ya Wagikuyu akisema kuwa ardhi hiyo ilikuwa na thamani ya kiuchumi na pia ya kidini (kiimani).

Dini ya Kimagharibi pia ni njia nyingine iliyotumiwa na wakoloni wakongwe katika kupenya na kufanikisha utawala wao barani Afrika. Hata ikiwa Waafrika walikuwa na dini zao za kiasili, dini hizo zilipuuzwa na wakoloni walipovamia Afrika kuzionyesha kama zilizojaa uovu huku wakisisitiza ubora wa dini ya Kikristo. Katika riwaya ya *Njia Panda* (1974), Ngugi anaonyesha mtanziko uliowapata baadhi ya Waafrika walipoletewa dini mpya na huku dini yao ya asili ikiwa bado na thamani kuu. Dini hii ngeni iliwigawana Waafrika kuwili kati ya walioupokea Ukristo na wale waliobaki na dini yao ya kitamaduni. Mhusika Waiyaki kwa mfano anajaribu kuziandama dini hizo mbili na kukosa kufanikiwa mwishoni. Kwa mfano, anapoenda kanisani watu walioshikilia utamaduni kikiki wanamshutumu wakidhani kuwa anashirikiana na maadui (Wakiristo). Kwa kuongozwa na mgawanyiko huu baina ya Waafrika ilikuwa rahisi kwa mkoloni kuongoza. Katika sura ya nne tutaonyesha jinsi mbinu hii ya tenga utawale ilivyotumika katika tamtulia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*.

Mbatiah (2016) ni mwandishi mwingine aliyetoa mchango wake kuhusu historia ya ukoloni nchini Kenya. Anaonyesha jinsi uvamizi wa Uingereza ulivyoanza na baadaye kupingwa na Waafrika. Anadhihirisha kwamba wakoloni walitumia mabavu kutawala na kuwanyang’anya

wenyeji mali yao. Baadhi ya makundi ya Kiafrika yaliyoanza kupinga utawala huo ni kama vile Wamazrui, Wanandi chini ya kiongozi wao Orkoiyot na kisha makabila mengine yakafuatia. Kama alivyoonyesha Kareithi, Mbatiah pia anathibitisha mchango mkubwa wa kundi la Mau Mau. Kwa mfano, mwandishi huyu anakiri kuwa wakoloni na hasa masetla walikuwa na nguvu nyingi sana kabla ya kuzaliwa kwa kundi la Mau Mau. Kufuatia shinikizo la kundi hili, wakoloni walianza kusikiliza maoni ya viongozi wa vyama vya kisiasa na baadhi yao wakateuliwa kujiunga na Bunge (LEGCO). Mtaalamu huyu anathibitisha ukatili wa wakoloni uliohusu matumizi ya nguvu za polisi na kijeshi dhidi ya Waafrika. Kwa mfano anaonyesha jinsi Wanandi walivyoadhibiwa vibaya na kikosi cha askari wa kikoloni. Katika utafiti wetu pia tunaonyesha jinsi polisi wanavyotumiwa na watawala kuwaadhibu Waafrika wenzao ili kumuepushia kiongozi upinzani na kudumisha utawala. Tunaonyesha kuwa kwa kufanya hivi wao ni vyombo vya uendelezaji ukoloni mamboleo.

Mhimili mwingine wa nadharia ya ubaada-ukoloni ni kuwa utamaduni mseto huibuka katika mataifa machanga kutokana na maingiliano baina yao na mataifa ya Kimagharibi. Kigezo hiki cha uibukaji wa utamaduni mpya ndicho Achebe (1967) anachoangazia. Anaonyesha jinsi mkoloni alivyotumia dini katika kubadili mawazo ya watu wa kabila la Igbo ili iwe rahisi kwake kutawala. Mkoloni alileta kwanza dini ya Kikiristo kupitia wamisheni na kwa njia hii akawagawa watu kuwili: Wafuasi wa wamisheni na wafuasi wa utamauni wa Kiigbo. Kwa hivyo kukawa na utamaduni mseto. Wamisheni waliwafundisha Waafrika kuwa imani na itikadi zao zilikuwa zimejengeka katika misingi ya uongo. Jambo hili lilipelekea watu wengi wa Umuofia kuikubali dini mpya. Katika muktadha huu dini inakuwa ni chombo cha utengano badala ya kuwaunganisha watu. Katika riwaya hii kwa mfano, mhusika mkuu Okonkwo anatengana na mtoto wake kwa sababu ya dini; mtoto anakubali dini ya kikoloni huku babake akibaki katika utamaduni wa kijadi.

Katika *Shujaa Okonkwo*, Achebe anaonyesha madhara mengine ya ukoloni kama vile unyakuzi wa ardhi, ulipaji wa kodi, mauaji na mafarakano ya kifamilia. Kwa mfano anatoa kisa ambapo Waingereza walilipisha kisasi kwa kuwaua watu wa kijiji kizima katika eneo la Abame. Hii ni baada ya Waafrika wa eneo hilo kumuua Mzungu mmoja aliyefika huko akiwa na baiskeli ambayo pia iliharibiwa. Hata hivyo, Achebe anaonyesha kuwa kuna baadhi ya watu waliofurahia

kuja kwa ukoloni. Kwa mfano, anasema kwamba biashara ya kisasa ilipoanzishwa katika Umuofia, baadhi ya watu walifurahia faida walizopata.

Katika Afrika Kusini, mkoloni pia aliendeleza udhalimu kwa miaka mingi dhidi ya Waafrika. Ubaguzi wa rangi ulionekana katika utoaji wa huduma za kijamii kama vile shuleni, hospitalini, sokoni, viwandani na katika uajiri wa wafanyikazi. Kwa sababu hii, mtu mweusi hakukubaliwa kutangamana na watu weupe atakavyo katika shule, kazini au mikutanoni. Wafanyikazi wa Kiafrika kwa mfano walidhulumiwa kwa kupewa kazi za sulubu za kuchimba madini na kulipwa malipo duni. Katika riwaya ya *Mchimba Madini* ya Peter Abrahams, tunaona mhusika Xuma akishangaa sana alipotembea mjini na kuwaona watu weusi wakikimbia mara wawaonapo watu weupe. Yeye anapokataa kutoroka anazuiliwa na askari mweupe. Askari anamchapa Xuma vibaya. Katika kisa kingine katika riwaya hii, mtu mweusi anakatazwa kupika pombe lakini mtu mweupe anakubaliwa. Ubaguzi kama huu unathibitisha mawazo ya msingi ya nadharia ya ubaada-ukoloni kwamba Mwafrika anachukuliwa kuwa mtu wa tabaka la chini na aliyenyuma kimaendeleo. Hii ndio misingi ya ubaguzi huu. Abrahams hata hivyo, anaonyesha kukerwa na mtindo huu na hii ndio maana anatoa kauli hii: “Binadamu ni binadamu tu na rangi haifai kuwa sababu za kubaguana”.

Kufuatia ukweli kwamba ukoloni ni tukio la kihistoria lililoathiri maeneo mengi ya bara la Afrika, pamekuwepo na waandishi wa kutoka sehemu mbali mbali za Afrika na nje ya Afrika, waliowahi kuandika kuhusu ukoloni. Hii ndio sababu utafiti huu umetoa mifano ya waandishi wa kutoka Afrika Magharibi (Achebe), Afrika Mashariki (Ngugi, Mulokozi na Kareithi) na Afrika Kusini (Abrahams).

2.3 Ukoloni Mamboleo

Ukoloni mamboleo ni namna nchi za Kimagharibi zinavyoendeleza utawala wa kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa mataifa machanga kwa lengo la kujinufaisha. Waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili wameonyesha kuwa mataifa mengi ya Kiafrika yangali yanadhibitiwa kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja na mataifa yaliyoyatawala. Hii ina maana kuwa mataifa hayo ya Kiafrika yalipata uhuru wa bendera pekee lakini uhuru wa kiuchumi, kisiasa na kijamii ukabakia mikononi mwa nchi za Kimagharibi. King’ei (1987) anadai kuwa kabla ya mkoloni kuondoka,

alihakikisha kuwa amejitua tabaka la wenyeji lililokuwa na mwelekeo na tabia kama zake (Mzungu) ili liendeleze ukoloni mpya. Kwa hivyo, dini na elimu vikawa vyombo vilivyotumika kulitimiza jambo hilo. Jambo hili lilizua tabaka la Waafrika lililojitenga na wengine waliokosa elimu na dini. Utengano huu ulisababishwa na mgongano wa kiutamaduni uliojitokeza kwa sababu ya uigaji wa mitindo ya kimaisha ya Kimagharibi. Kulingana na Mazrui (1979), hali hii imezua mtanziko kwa Waafrika ambapo baadhi wanajaribu kuuasi utamaduni wa Kimagharibi huku wengine waking'ang'ana kuuiga utamaduni huo.

Tukiangalia tamthilia ya *Mashetani* (1971) kwa mfano, tunaona matabaka mawili makuu yanayowakilishwa na familia za Kitaru na Juma. Familia ya Juma inawakilisha tabaka lililokuwa na utajiri wa kiukoo lililorithi kutoka kwa wazazi wao. Lile la Kitaru ni tabaka lililopokea elimu ya Kizungu na ndilo lililoshika hatamu za uongozi baada ya uhuru. Tabaka hili lilirithi vyeo, nyumba na mienendo ya kimaisha iliyokuwa ya Wazungu. Kama anavyosema Hussein, tabaka hili baadaye lilikuja kuitwa “Wazungu weusi.”(utangulizi wa *Mashetani*, uk.vii).

Mwandishi wa *Mashetani* anatumia jazanda mbalimbali katika kulimulika suala la ukoloni mamboleo. Kwa mfano Kitaru na Juma wakiongea kuhusu kwenda kutazama sinema wanasema:

Juma :Tuende sinema basi itatusaidia

Kitaru : Hakuna sinema nzuri

Juma : Iko cowboy moja.Tikiti juu yangu

Kitaru : Sinema yenyewe ninajua hata kabla sijaiona.

Cowboy atawaua *Red Indians* wote peke yake. Mimi mchezo unaoonyesha ugomvi au mgongano baina ya mwenye nguvu na asiye na nguvu sipendi. (uk.20)

Mazungumzo haya yanaashiria mivutano ya kimataifa inayotiliwa nguvu na dhuluma za kiuchumi na kisiasa kutoka kwa nchi zilizostawi kiuchumi dhidi ya nchi maskini. Ukoloni mkongwe hasa uliwekewa misingi yake kupitia dhuluma za aina mbali mbali. Kwa muktadha huu, “cow boy” ni ishara ya mataifa yenye nguvu na “Red Indians” ni kiwakilishi cha mataifa yaliyobaki nyuma kiuchumi. Kifungu hiki kijazanda kinaonyesha hali ya uhusiano uliopo baina ya mataifa machanga na yale yenye uwezo mkubwa wa kiuchumi; kwamba ni uhusiano wa maonevu na dhuluma.

Hussein (1971) anaonyesha mtanziko unaozikumba nchi changa kwa sababu ya mivutano ya kiuchumi na kisiasa kuhusu ubepari wa Kimagharibi. Baadhi ya nchi zilishindwa kuamua ni mfumo upi bora wa kiuchumi, kijamii na kisiasa wa kuongoza mataifa yao. Mataifa yaliyoendelea yaliyang'ang'ania mataifa machanga ili kudumisha aidha ubepari au ujamaa huko. Kwa hivyo nchi hizo ziliongozwa na nguvu za kutoka nje ya bara lao. Hivi ndivyo Kitaru anasema:

Kitaru: Toka tumepata uhuru, sisi Waafrika hapa imekuwa tumeingia...ehe, mfano mzuri...imekuwa kama tumeingia katika jahazi moja zuri na jina letu limeandikwa..lakini nahodha... nahodha nani? Je ikiwa mkondo unavuta upande mwingine na nahodha anataka kupeleka jahazi upande mwingine? (Uk.21)

Taswira ya jahazi na nahodha imetumiwa kueleza hali ya kuchanganyikiwa waliokuwa nayo baadhi ya viongozi wa Kiafrika baada ya uhuru kufuatia nguvu za kutoka nje ya mataifa hayo. Baadhi yao walilazimishwa kuandama mfumo wa kiuchumi na kisiasa wa kiubepari au kisosholisti kutoka mataifa ya nje bila kuwa na uhuru wa kujiamulia mfumo faafu katika mazingira yao.

Mazrui (1982) ameonyesha jinsi tatizo la ukoloni mamboleo lilivyoziathiri nchi za Kiafrika. Njia moja inayodhihirisha ukoloni mamboleo anayoonyesha ni dhuluma dhidi ya wafanyakazi hasa wale walioajiriwa katika mashamba ya Wazungu. Katika tamthilia hii, Mazrui anaonyesha kuwa hata baada ya uhuru wafanyakazi wanazidi kunyimwa haki zao kupitia unyanyasaji wa kibepari. Hii ni ishara ya ukoloni mamboleo kwani hivi ndivyo pia walivyofanya wakoloni. Katika tamthilia hii, tunaona migomo kadhaa ya wafanyakazi wakilalamika kuwa wanakandamizwa na mwajiri wao, bwana Delamon.

Kulingana na mwandishi huyu, njia nyingine inayoendeleza ukoloni mamboleo na iliyorithiwa kutoka kwa ukoloni mkongwe ni tenga-utawale. Stewart (1951) anasema kuwa huu ni mkakati uliotumiwa na Uingereza kutawala India. Ulihusu kuwatenganisha watu kwa misingi ya kikabila na kidini. Kwa mfano, Wahindu walipendelewa nao Waislamu wakabaguliwa. Vivyo hivyo, katika *Kilio cha Haki*, Delamon anawatenganisha wafanyakazi kwa kuwaongezea baadhi yao mishahara na kuwanyima wengine. Mbinu hii inamwezesha kukomesha migomo ya mara kwa

mara shambani mwake. Wale wanaokubali nyongeza hizi (Matovu, Tereki na Pelekha) wanawasaliti wenzao na kusambaratisha juhudi za kujikomboa.

Tamthlia hii pia inaunga mkono mawazo makuu ya nadharia tunayoitumia katika utafiti huu ya ubaada-ukoloni, kwamba Wazungu waliamini kuwa mtu wa Mashariki na Mwafrika walikosa historia, utamaduni na ustaarabu. Wafula (1999) anasema kwamba Wazungu kwa kufanya hivi walikuwa wakiendeleza dhana potovu zilizokuwa zikienezwa na Joseph Conrad katika *The Heart of Darkness*. Mtazamo huu hasi ndio msingi wa ubaguzi wa rangi unaondelezwa na wakoloni na baadaye wakoloni mamboleo dhidi ya watu wa Kiafrika. Kwa sababu hii Mzungu hakumthamini Mwafrika wala kumheshimu. Delamon kwa mfano anawatusi wafanyikazi mara kadhaa kwa njia inayoonyesha ubaguzi wa rangi:

Delamon: (Akiwageukia Zani na Shindo) Kwa nini hamnitafutii maboi wenye akili zaidi? *Foolish baboons*. (uk.9-10)

Hii ni ishara tosha kuwa Mwafrika huonekana kama mtu mwenye akili duni na aliyekosa maadili kama Mzungu na hii ndio sababu Wazungu wanawadharau na kuwatusi. Hali hii pia ni ishara ya jinsi mataifa ya Kimagharibi yanavyodumisha uhusiano wa kinafiki na mataifa ya Kiafrika. Tunamsikia Delamon akiwatusi waajiriwa wake mara nyingine lakini kwa sababu ya uhitaji wao hawajali:

Delamon : Pumbavu, hata mambo rahisi yanawashinda...(akipiga ngumi meza) Huyu mwanamke ni punda, hana fadhila, hana shukrani kama hayawani...naapa kwa bendera yetu leo atanitambua...(uk.67)

Tatizo la utegemezi wa kiuchumi kama njia moja inayoendeleza ukoloni mamboleo pia limeangaziwa na waandishi wa fasihi ya Kiswahili. Mohamed (1995) anaonyesha jinsi mataifa ya Kiafrika yalivyoathiriwa na utegemaji wa misaada ya kutoka ng'ambo hasa misaada ya kutoka Ulaya. Anadai kuwa utegemezi unalemaza uvumbuzi wa aina yoyote. Hii ndio sababu anatashtiti mfumo wa elimu kwa kuendeleza ukariri wa dhana za kigeni bila kutumia dhana hizo kuboresha maisha. Kwa mfano katika tamthlia hii, mwandishi anamkejeli mwalimu na wanafunzi wake kwa kukariri "Archimedes Principle" bila kuonyesha maatumizi ya kanuni hii katika hali halisi.

Wafula (1999) akichangia katika mjadala wa *Amezidi*, anasema kuwa mwandishi anaamini kuwa maongozi ya nchi za Kiafrika ni potovu. Badala ya kuhimiza uvumbuzi, mataifa haya yanasisitiza uigaji na ununuzi wa bidhaa kutoka ng'ambo. Tamthlia hii pia inafichua matatizo mengine yanayoletwa na utegemezi wa misaada kama vile vifo na magonjwa. Ame na Zidi wanapopata msaada wa nyama ya ng'ombe kutoka EC, nyama hiyo ilikuwa imeoza. Kwa sababu hii ugonjwa unazuka na kumwamamiza Zidi. Mwandishi anatumia ugonjwa kijazanda kutuelimisha kuwa utegemezi wa misaada unaangamiza chumi za Kiafrika. Ni wazi pia kwamba misaada inayoingizwa barani Afrika huwa ni masalio ya vitu visivyohitajika katika mataifa yanayotoa misaada hiyo.

Njogu na Chimera (1999) wanakubaliana na Mohamed kwamba misaada inaleta athari nyingi hasi badala ya kumsaidia mlengwa wa misaada hiyo. Wanasema:

Misaada inayotolewa kwa nchi za Amezidi haifai. Kwa mfano, Ufaransa inatoa madawa yasiyohitajika huko kwao, Uingereza inatoa mitumba na nyama za kukausha na EC inatoa mizoga iliyoza na inukayo vibaya sana. (Uk.77)

Maoni ya wahakiki hawa yanashabihiana na yale ya Rodney (1976) kuhusu utegemezi. Rodney anasema kuwa ni vyema kila jamii iweze kutegemea mazingira yake kuboresha maisha yake:

Kila jamii imeonyesha uwezo wa kuyaendeleza maisha yake vizuri zaidi kwa kuzitegemea rasilimali ambazo imetunukiwa na mazingira asili (uk:11).

Tunaafikiana na wazo hili la Rodney, kwa kuwa utegemezi wa kila nchi unalemaza maendeleo katika nchi changa kwani nchi zinazotegemea zingine hushindwa kutumia mazingira yake kikamilifu kujikimu. Uhusiano kati ya mataifa unapozorota taifa lililokuwa tegemezi husababishia wananchi wake matatizo mengi yakiwemo ya njaa na uhaba wa huduma za kimsingi kama vile dawa, shule na maji. Katika *Amezidi*, utegemezi uliopita mipaka unawafanya Ame na Zidi kuagiza takribani kila kitu. Wanaagiza kwa mfano moto, kuni, mafuta na hata kisu. Hii ni kwa sababu utegemezi unaleta athari kubwa ya uvivu.

Okot p'Bitek (1972) analiangalia tatizo la ukoloni mamboleo katika muktadha wa utamaduni wa Kiafrika. Kwa mfano anaonyesha jinsi elimu ya Kimagharibi ilivyowakengeusha baadhi ya

wasomi wa Kiafrika. Anamtumia mhusika asiyekuwa na elimu hii ya kigeni (Lawino) kuonyesha athari za elimu hii. Kwa mfano, Lawino anakerwa na tabia nyingi za mumewe aliyesoma. Kwa mfano mumewe aliyesoma anamtusi Lawino kwa kutosoma na kukosa dini akimlinganisha na mama mkwe. Lawino analalamika hivi:

Lawino: Huwa ananitusi kwa Kiingereza, ana maringo sana, hanitaki tena,
Anasema kuwa siwezi kutamka hata neno moja la kigeni,
Ocol anasema kuwa yeye ni mwanamume wa kisasa. Aliyeendelea
na kustaarabika. Anasema sijui dini na kwamba ninazuia maendeleo
yake. Anasema watu weusi ni washenzi, na njia zao zimeoza, nyimbo
zao zimejaa uovu, ni wajinga, maskini na wenye magonjwa. (Uk.36) T.Y

Mawazo makuu katika shairi hili ni kwamba kuna mgongano wa kitamaduni kwani Ocol kinyume na Lawino ni msomi aliyebugia vipengele vya utamaduni wa Kimagharibi kama vile dini, elimu na hata mienendo yake. Mkinzano huu unamtenganisha na mkewe na wakwe zake. Hata hivyo, mwandishi anamkejeli Ocol ambaye ni mtu mweusi ilhali anapata ujasiri wa kuwatusi watu weusi anaposema kuwa wao ni wajinga, maskini na walioathiriwa na magonjwa. Hii ni ishara tosha kwamba elimu ya kigeni inawakengeusha wasomi sana mpaka kufikia kiwango cha kuwavunja familia zao. Kwa sababu ya usasa hasa elimu, Ocol anaamua kumuoa mke mwingine (Tina) aliyeelimika na anayezingatia mienendo ya Kizungu. Tina amekengeuka sana hivi kwamba anajinyima hata chakula ili asinone bali awe kama Mzungu kiumbo na kitabia. Katika muktadha huu Lawino hampingi mumewe kumuoa mke wa pili, na kwa sababu hii anakuwa kiwakilishi kizuri cha utamaduni wa Kiafrika unaoathiriwa na utamaduni wa Kimagharibi unaowakilishwa na Ocol na Tina. Kama nadharia ya ubaada-ukoloni inavyosisitiza utamaduni mseto ni tokeo la mtagusano wa utamaduni wa Kimagharibi na wa Kiafrika. Waafrika walioathiriwa na utamaduni wa kigeni kama vile Ocol na Tina wanakosa utamaduni asili.

Achebe (1967) pia anaonyesha kuathiriwa kwa Waafrika wengi na ukoloni mamboleo kupitia njia mbali mbali. Kwa mfano, anaonyesha jinsi Waafrika walivyoathiriwa na lugha ya Kiingereza hadi kufikia kiwango cha wale wasiokielewa Kingereza kukitumia kwa kukichanganya na lugha za Kienyeji na kupelekea kuibuka kwa pijini inayosemwa na baadhi ya watu wa Afrika Magharibi. Kuonyesha jinsi Waafrika walivyoathamini utamaduni wa kigeni hasa mavazi, baadhi yao hununua mavazi kutoka Uingereza na kujivunia hali hiyo. Achebe katika *Mwakilishi wa Watu* anasema:

Nilishangazwa na haja ya watu wetu kununua mavazi ya kigeni.
Kwa mfano kuna huyu mwenye nguo iliyo na maandishi: 100%
WOOL: MADE IN ENGLAND. (uk.64).

Katika muktadha huu, tunaona jinsi watu wa jamii hii walivyothamini utamaduni wa kigeni na hali hii inawafanya kupenda vifaa vya kigeni kama vile mavazi. Katika riwaya hii, Achebe pia anaonyesha jinsi mataifa ya Kimagharibi yanavyoingilia uongozi wa nchi za Kiafrika. Kwa mfano, anatoa kisa ambapo waziri mkuu anawashutumu viongozi wa upinzani kwa kujaribu kupindua serikali huku wakisaidiwa na maadui kutoka ng'ambo. Hii ni ishara kwamba mataifa ya Kimagharibi yanaendelea kuzidhibiti nchi changa kwa kuamua jinsi nchi hizo zitakavyoongozwa.

Ukoloni wa kitamaduni umezungumziwa vile vile na Okot p'Bitek kando na Achebe. Mwandishi kuyu anaangazia jinsi ukoloni mamboleo ulivyoza dhana ngeni na ambazo zilimtatiza Mwafrika kuzifahamu. Katika *Wimbo wa Lawino* kwa mfano, dhana ya kuhesabu wakati inakuwa kizungumkuti kwa Lawino kutatua. Mumewe Lawino, Ocol, aliyeelimika na kupata dini ya Kikristo, anamwambia Lawino kuwa kabla ya Yesu kuzaliwa Wazungu walihesabu miaka kutoka nyuma. Ocol anasema “Miaka ikawa elfu, mia, kumi na ilipofika moja Yesu akazaliwa.” (uk.254). Kwa muktadha huu, mwandishi anaonyesha athari ya ukoloni wa kimawazo kwa Waafrika iliyopitishwa katika mfumo wa elimu ya kigeni. Okot pia anaonyesha jinsi dini ya Kikristo ilivyowaathiri Waafrika kimawazo.

Ukoloni mamboleo unaonyeshwa kama chombo cha ukengeushi hasa kwa wasomi waliopokea elimu ya kigeni. Baadhi ya wasomi hao wanashindwa kuingiliana na wenzao wa vijijini vizuri kwa sababu za kitabaka zinazojengwa na elimu hiyo. Wao huishi mijini na kuandama hali za maisha za Kizungu. Ngugi wa Thiong'o anaangazia tatizo hili la ukoloni mamboleo katika tamthilia ya *Mtawa Mweusi* (1970). Katika tamthilia hii mhusika Remi anakatalia mjini na kumuoa bibi wa Kizungu kinyume na matakwa ya wazazi wake. Hii ni kwa sababu ana eimu ya kigeni na dini ya kigeni tofauti na wanakijiji. Kwa njia hii mwandishi anaangazia jinsi ukoloni mamboleo ulivyodhuru utamaduni wa kijadi wa Waafrika. Kisasi kilichofumbata dini na elimu ya Kimagharibi kinajitokeza kama kisicho na njia maalum ya ujitambulishaji. Ukosefu wa

kitambulisho maalum kwa wananchi wa mataifa yaliyotawaliwa ni mhimili mmoja unaoshikilia nadharia ya ubaada-ukoloni.

2.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumerejelea kazi mbalimbali za kifasihi ili kuonyesha jinsi suala la ukoloni na ukoloni mamboleo limeangaziwa na waandishi wa Kiswahili. Tumerejelea tamthilia na riwaya za waandishi wa kutoka Afrika Mashariki, Afrika Magharibi, na Kusini. Tumefanya hili kwa sababu ukoloni uliathiri pembe zote za Afrika na kwa sababu hii waandishi wa sehemu hizi wameandika kuhusu namna ukoloni na ukoloni mamboleo ulivyoziathiri jamii zao. Ukoloni mamboleo nao unazidi kujidhihirisha tangu nchi za Kiafrika kujinyakulia uhuru hadi sasa. Kwa maoni yetu mataifa machanga hayafanyi juhudi kubwa kujinasua kutokana na ukoloni mamboleo. Kwa hivyo, yamezidi kuendeleza ukoloni mamboleo ama kimakusudi au kwa kutojua.

Vilevile, tumeangazia suala la ukoloni kwa kutazama sifa mbali mbali za ukoloni kwa awamu mbili, yaani ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Tumezungumzia kwa kifupi historia ya ukoloni mkongwe, maendeleo yake hadi kufikia hali ya kisasa ya ukoloni mamboleo. Imebainika kwamba ukoloni mkongwe ulitumia mbinu kadhaa ili kujidumisha. Baadhi ya mbinu hizo ziliwasababishia watawaliwa madhila makubwa kama vile kunyang'anywa mashamba yao, kushinikizwa kulipa kodi, kunyimwa uhuru wa kutembea bila kitambulisho, uharibifu wa mali na hata vifo.

Kwa bahati mbaya athari za ukoloni mkongwe hazikuisha kufuatia kupatikana kwa uhuru kwani nchi nyingi zilijipata, kupitia viongozi wao, zikiendeleza ukoloni mpya. Fasihi ya Kiswahili imeyazungumzia masuala haya kwa kina na ndio sababu katika utafiti huu tumenukuu kazi za fasihi ya Kiswahili kama vile *Mashetani*, *Mzalendo Kimathi*, *Amezidi*, *Kilio cha Haki*, *Kaburi bila Msalaba*, *Mtawa Mweusi*, *Wimbo wa Lawino* na nyinginezo.

Waandishi wengi wametoa kazi kwa lugha ya Kiingereza zinazofichua madhara ya ukoloni na ukoloni mamboleo katika mataifa yaliyotawaliwa. Hii ni kwa sababu wasomi wengi wa Kiafrika walioelimika mapema, walipitia mfumo wa kielimu wa kokoloni ambapo umilisi wa lugha za

Kizungu ulisisitizwa. Nazareth (1976) anaunga jambo hili mkono akisema kwamba waandishi wa mataifa yaliyokuwa chini ya mkoloni wamekumbwa na tatizo la ukosefu wa lugha ya kuandikia. Hii ni kwa sababu waandishi hao wanapojaribu kulikosoa tatizo la ukoloni mamboleo na ukoloni, wanagundua kwamba hawana lugha ya kufanya hivyo ila ile ya kikoloni. Inakuwa kinaya kwa mhakiki kuonyesha maovu ya ukoloni na ukoloni mamboleo huku akitumia lugha ya kikoloni vile vile. Kwa hivyo, kuendelea kutoa kazi za kifasihi kwa lugha za kigeni ni kama kuendeleza ukoloni mamboleo.

Utafiti huu umegundua kuwa waandishi wengi wameangazia jinsi wananchi wa mataifa yaliyotawaliwa walivyodhulumiwa na wakoloni wakongwe na picha wanazochora kuwahusu wakoloni ni hasi. Wachache mno wameonyesha upande chanya wa ukoloni mkongwe. Hata hivyo, hivi si kumaanisha kuwa hakuna lolote zuri lililoletwa na wakoloni. Kwa mfano huduma za afya na kielimu ziliboreshwa nao na wamisheni. Hata hivyo, tabia, mienendo na taasisi za kikoloni zilibaki baada ya ukoloni kung'olewa na kuendelezwa na Waafrika pamoja na mataifa ya Kimagharibi kwa njia zisizo wazi.

SURA YA TATU

NAFASI YA UTEGEMEZI WA KIUCHUMI NA TAASISI ZA KIMATAIFA KATIKA KUENDELEZA UKOLONI MAMBOLEO

3.1 Utangulizi

Sura hii inachunguza baadhi ya vipengele vya ukoloni mamboleo vinavyopatikana katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Vipengele hivyo ni utegemezi wa kiuchumi na sera za taasisi za kimataifa. Sura hii inaangazia kwa kina ni vipi suala la utegemezi wa kiuchumi linavyoziathiri nchi changa hasa kwa kulazimika kufuata masharti ya mataifa yanayozipa mikopo na misaada.

Mchango wa taasisi za kimataifa kama vile Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani na Shirika la Biashara Duniani umeangaziwa ili kudhihirisha jinsi sera hizo zinavyopunguza kasi ya maendeleo katika mataifa machanga. Vilevile sura hii inaangazia baadhi ya vipengele vya kimtindo vinavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui ya ukoloni mambo leo.

3.2. Utegemezi wa Kiuchumi

Katika taaluma za kimaendeleo, utegemezi hurejelea hali ambapo nchi au eneo fulani hutegemea nchi au eneo lingine kimsaada, kimaisha au katika ukuaji wake (Ikechukwu, 2017). Kulingana na kazi hii, nchi za Ulimwengu wa Tatu hujumuisha nchi zilizo na maendeleo pungufu za Asia, Afrika na Marekani kusini na huwa na sifa zinazofanana. Sifa hizo ni umaskini, ongezeko kubwa la watu na utegemeaji mkubwa wa kiuchumi kwa nchi zilizoendelea. Ni wazi kwamba tatizo la utegemezi ni njia moja kuu ya kuyadhibiti maendeleo ya mataifa machanga na kwa kufanya hivi nchi hizi changa zinakosa uhuru wa kukuza chumi zao. Hii ni kwa sababu matukio ya kisiasa na kiuchumi yanayofanyika katika mataifa ya Ulimwengu wa Kwanza huwa na athari kubwa sana katika mataifa ya Ulimwengu wa Tatu. Kinyume na hili, matukio kama hayo kutoka mataifa ya Ulimwengu wa Tatu huwa na athari ndogo mno kwa nchi hizo zilizoendelea.

Tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Kijiba cha Moyo* zimeangazia tatizo la utegemezi katika mataifa machanga kwa mapana na marefu. Mwandishi vilevile ameonyesha athari za utegemezi katika kupunguza kasi ya maendeleo ya nchi hizo hasa kulemaa kwa Afrika kiuchumi. Suala la

utegemezi hujidhihirisha kupitia mikopo na misaada inayotolewa na nchi zilizoendelea kama vile Marekani, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Uchina na Japani. Vilevile kuna mashirika mbalimbali ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Dunia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Kibiashara la Dunia na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambayo hutoa mikopo na misaada. Kwa sababu ya ufadhili wa mashirika haya, mataifa huru hasa ya Kiafrika yanalazimika kufuata sheria na kanuni za kutoka nje katika utawala wa nchi zao.

Katika tamthlia ya *Mstahiki Meya*, kiongozi wa jiji la Cheneo anategemea msaada sana kufadhili shughuli muhimu za baraza mpaka anakuwa na woga mwingi kuhusu kuharibika kwa jina la mji wake machoni mwa wafadhili. Hii ndio maana kiongozi huyu anashtuka anaposikia kuwa huenda wafadhili wasizuru mji kufuatia mgomo wa wafanyikazi. Jambo hili linadhihirika kupitia mazungumzo yafuatayo:

Meya: Jina huko nje bwana. Jamii ya kimataifa ingesemaje?

Diwani II: Hata wangewashauri wageni wetu dhidi ya kuja hapa. Sura ya baraza letu ingeharibika huko nje. Hii ni hatari kwa misaada tunayotarajia baada ya ziara hii wanayoanza kesho.

Meya: Hayo tunayafahamu sote. La muhimu sasa ni kuamua jambo la kufanya. Taka zimejaa katika barabara zetu. Wanatawala nzi na harufu. Hali hii tutaiondoaje kabla ya kesho? (uk.73)

Tukichunguza mazungumzo haya, inabainika kuwa mataifa machanga huwa tayari kufanya lolote ili kuyafurahisha mataifa ya Kimagharibi ili yaendeleo kupata misaada yao. Hii ndio maana Meya na viongozi wengine wa jiji wanashikwa na kiwewe wakati wafanyikazi wanapogoma wakati ambapo wageni wafadhili wanatarajiwa kuuzuru mji wao. Woga huu unawazindua viongozi hawa kuanza kutafuta njia za dharura za kuunadhifisha mji. Huu ni ukoloni mamboleo kwa sababu ni wazi kwamba nchi za nje ndizo zinaelekeza mipango kadhaa ya nchi hizi changa.

Baadhi ya viongozi wa Kiafrika wanapomba misaada wanaielekeza katika miradi isiyozalisha faida kama vile ulipaji wa mishahara. Matumizi ya mikopo kwa njia hii hayafai kwani hulifunga taifa katika utumwa wa kulipa madeni kwa miaka mingi ilhali pesa hizo hazikuwekezwa kwenye miradi ya kuufaidi uchumi. Athari kubwa ya mikopo kwa uchumi wa aina hii huwa ni kwamba

vizazi vya baadaye hulazimika kulipia madeni ambayo hayakuvifaidi. Jambo hili linadhihirika katika mazungumzo yafuatayo baina ya Meya na Diwani III:

- Meya** : Hivi una habari kwamba hao wageni wanaokuja ni washirika wetu wa maendeleo? Wanatupa mikopo ya kulipia mishahara.
- Diwani III** : Kwa sasa hilo ni suluhisho zuri kwa matatizo yetu lakini ni mzigo tunaowaachia wajukuu na vitukuu ambao hawakufaidi mikopo hiyo.
- Meya** : Leo si kesho. Tuyashugulikie ya leo. Kesho, keshokutwa na mtondo hatutakuwepo. Wayatakiani ya mtondogoo? (uk.55)

Katika maongezi haya, ni wazi kwamba tamthlia hii inawatashtiti viongozi wa bara la Afrika wanaokimbilia madeni kutoka mataifa yaliyoendelea lakini bila kujali athari hasi za mikopo hiyo. Kwa mfano, kutokana na dondoo hilo hapo juu ni wazi kwamba baadhi ya viongozi hao hawajali maslahi ya vizazi vya kesho. Pia wengi wao huwapuuza wanauchumi pamoja na mawaidha yao kama tunavyoona Meya akipuuza wosia wa Diwani III. Utegemezi huu unailemaza nchi kwani inakwama katika ulipaji wa madeni na riba yake. Mutiga (2017) anasema kwamba utegemezi wa mikopo hukuza uvivu, hulemaza uvumbuzi na huendeleza uongozi usiofaa kwa sababu viongozi wasiostahili huendelea kushikilia hatamu za uongozi huku wakihungwa mkono na mataifa ya kifadhili. Anahitimisha kuwa ikiwa nchi za Kiafrika zitakomesha utegemezi wa misaada kutoka mataifa ya Kimagharibi, zitaweza kutumia maliasili yake kujikomboa. Anakiri kuwa Afrika inachohitaji si misaada bali ni ushirikiano wa kibiashara ulio na uwiano sawa.

Uongozi unaotegemea msaada katika kutimiza mahitaji ya kimsingi humtia kiongozi husika kiburi na mara nyingi huzua uongozi wa kiimla. Hali hii hupelekea viongozi wa mataifa tegemezi kuwadharau raia wake hasa wale wanaowapinga. Katika tamthlia ya *Mstahiki Meya*, kiongozi wa Cheneo anajihusisha na maandalizi ya kuwapokea wageni wanaotarajiwa kutoka ng'ambo na kukataa kusuluhisha matatizo ya wafanyikazi. Kiburi na mapuuza haya yanajitokeza katika mazungumzo yafuatayo:

- Meya:** Basi mnafahamu sina muda mwingi wa kupoteza.
- Medi:** Kupoteza?
- Beka:** Una maana kuwa kilichotuleta hapa hakina maana?
- Meya:** Wageni ni muhimu zaidi.
- Beka:** Wageni wa siku moja? (uk.67)

Katika mazungumzo haya, tamthilia inawakejeli baadhi ya viongozi wa Kiafrika ambao wameathiriwa na kasumba ya ukoloni mamboleo sana hivi kwamba wanashindwa kutatua matatizo ya nchi zao, wakitegemea nchi zilizoendelea kwa kila kitu. Hii ndio maana Meya anaona kuwa kuzungumza na wafanyikazi waliogoma ni kupoteza wakati kwani kwake wageni ambao huleta misaada ndio bora kuliko wananchi wake.

Tamthilia hii pia inaonyesha kuwa tatizo kubwa la mikopo na misaada ni kwamba mikopo hiyo inaelekezwa kwenye miradi isiyofaa kama vile inapotumika katika kulipia mishahara. Msimamizi wa masuala ya kiuchumi na kazi katika jiji la Cheneo, kwa mfano anamkanya Meya dhidi ya kuomba mikopo ya kulipia mishahara. Anamwambia kuwa mikopo inayotumiwa kulipia mishahara ni matumizi yasiyofaa ya pesa za umma. Hii ni kwa sababu kufanya hivyo ni kutatua matatizo ya baraza kijuujuu tu.

Hali hii inaongeza viwango vya umaskini na kuzidisha ufisadi wa viongozi hasa ikiwa nchi inayopokea misaada hiyo haina misingi bora ya kidemokrasia ya kuhakikisha matumizi bora ya hela hizo. Djankov, Montalvo na Reynal-Querol (2005) wanasema kuwa utegemezi wa misaada na mikopo ni laana kubwa kuliko ile laana ya mafuta katika mataifa yanayoendelea. Wanafafanua kuwa sababu ya kuwepo kwa laana hiyo ni kwamba utegemezi huzalisha miundo isiyo dhabiti ya taasisi za utawala. Wanamnukuu Easterly aliyedai kuwa kati ya miaka 1950-2001 mataifa yaliyopokea misaada na mikopo mingi na yale yaliyopokea mikopo michache hayakuwa na tofaouti katika ukuaji wa kiuchumi. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, tunaona kuwa utegemezi wa kiuchumi haujaondoa umaskini wala kuboresha miundo misingi. Mji wa Cheneo, tukiuchukua kama kiwakilishi cha mataifa mengi yanayoendelea, una huduma mbovu za afya, migomo isiyokwisha ya wafanyikazi, umaskini uliokithiri (ukosefu wa maji, chakula, makaa, mafuta ya taa n.k), elimu duni na uharibifu mkubwa wa mazingira. Easterly aliongeza kuwa mikopo mingi hutolewa kama zawadi kwa baadhi ya serikali kwa kukubali masharti ya mataifa yaliyoendelea.

Utegemezi wa kiuchumi ni njia inayotumiwa na mataifa yaliyoendelea ili kuyanasa na kisha kuyadhibiti mataifa yanayoendelea. Mwandishi analisisitiza jambo hili katika *Kijiba cha Moyo* kwa kutuchorea taswira ya maisha ya papa na vidagaa wakiwa baharini:

Aisha: Wala hausemi kuwa michafuko mikubwa inayoifanya bahari kunguruma huvitia kiwewe vidagaa ambavyo vikiona papa hupata utulivu kwa imani ya kusaidiwa. Lakini baadaye vidagaa huliwa na papa. Kwao heri zimwi ulijualo.
Sele: (Akitabasabu). Hewaa...Mwalimu hasa. Elimu hii yote umeipata wapi? (uk.36).

Katika picha hii papa ni kiwakilishi cha mataifa yenye nguvu za kiuchumi na vidagaa navyo ni viwakilishi vya mataifa machanga. Kulingana na dondoo hili, ni wazi kuwa mataifa machanga hupata utulivu yanapopata misaada kutoka kwa wafadhili wao. Hata hivyo, nchi hizo huathirika sana baadaye kupitia ufadhili huo. Athari kubwa kwao ni kwamba maeneo hayo tegemezi hushindwa kuvumbua mbinu na njia asilia za kutatua matatizo yao. Kama anavyosema Rodney (1976), taifa likiachwa pekee laweza kuvumbua mbinu za kujiendeleza na kufikia maendeleo ya kiwango cha juu kwa kutegemea rasilimali zake. Rodney anashikilia kuwa maendeleo ni sifa inayovihusu vizazi vyote vya binadamu popote vinapopatikana.

Wasomi wengi wanakubali kuwa mikopo kwa mataifa yanayoendelea huja na vikwazo vingi vilivyofichama na ndio maana athari zake hasi hazitambulikani mapema na nchi zinazokopa. Mwandishi wa masuala ya kiuchumi kutoka Uingereza, Graham Hancock (1991) anasema kuwa misaada na mikopo ya kigeni haiwasaidii wanaolengwa na mikopo hiyo bali inayafaa zaidi mataifa yanayotoa ufadhili huo. Anasema:

Misaada ya kigeni imeoza...imeoza hadi katikati. Inapaswa kukomeshwa kwa sababu haimsaidii maskini. Mara nyingi ina athari kubwa hasi kwa watu maskini (1991:99). T.Y

Hancock anadai kuwa asilimia 80% ya pesa zinazotolewa kama mikopo hutumiwa katika kuwanufaisha waajiriwa wa mashirika na nchi zinazotoa mikopo hiyo. Kwa mfano anasema kwamba waajiriwa hao hulipwa mishahara na marupurupu makubwa yanayotoka kwa mikopo hiyo, huandaa makongamano katika hoteli za kifahari, husafiri kwa ndege na njia nyingine za ubadhirifu. Kulingana na msomi huyu, wanaotoa mikopo hiyo pia hufanya kosa lingine kubwa ambalo ni kushinikiza aina fulani ya miradi kutekelezwa bila kuwahusisha walengwa wa miradi hiyo. Walengwa wa miradi hiyo huchukuliwa kama wasiokuwepo ilhali wao ndio hutoa ardhi ambamo baadhi ya miradi hutekelezewa. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, tunaona

mwandishi akikubaliana na wazo hili la Hancock kuhusu kushauriwa kwa Waafrika na wafadhili wa kimataifa:

- Musa** : Sisi tunaambiwa na kulikubali lao. Hatuna hiari. (kimya). Hata ukapinga na wao wameamua si kazi bure tu? Ni unyonge una mambo!
- Zainabu**: Pamoja na hayo, sisi vilevile ni washika dau. Ingefaaa kutushauri na mapema...inavunja moyo.Wao ndio watu na sisi sanamu tu. Wanatutikisa na kutuchezesha kama sanamu inavyovutwa kutoka mbali na kuwawinga ndege kutoka shamba la mawele.
- Musa** : Mhitaji! Mhitaji mke wangu siku zote ni mtumwa, na wao wanajua (uk.25)

Tukichunguza dondoo hili kwa undani, ni wazi kwamba ingawa nchi changa zina uhuru, viongozi wake si manahodha wa nchi zao bali mataifa ya mbali ndiyo huendesha mataifa hayo kwa njia za mikopo yao inayoambatana na masharti ya kulazimishwa kufuata sera fulani au mfumo fulani wa kiuchumi. Ukosefu wa mashauriano ya kina kuhusu miradi ya kufadhiliwa kunasababisha mikopo hiyo kushindwa kuimarisha maisha ya walengwa.

Mbinu ya ulaghai na udanganyifu ilitumiwa na wakoloni wakongwe katika kujipenyeza na kukalia baadhi ya sehemu za Afrika wakidai kuwa wamekuja kuwafaa Waafrika. Wakoloni mamboleo nao wanaitumia mbinu hii kujipenyeza kwa mataifa yanayoendelea kupitia utoaji wa mikopo na misaada. Jambo hili linadhihirika katika kauli ifuatayo iliyosemwa na daktari wa kigeni aliyeitwa kumtibu Sele:

Mimi niko hapa kukufaa. Ukitaka nirudi nitarudi. Maarifa nimekuja nayo.
Ala za kazi nimekuja nazo vilevile kutoka huko mbali.(uk.54).

Hancock anasema kuwa watoaji mikopo ndio huamua aina ya mradi, ujenzi utakavyotekelezwa na mahali pa kazi hiyo. Kando na hili, wanataaluma wa kigeni hutumiwa katika ujenzi na huja na vifaa vya kigeni ili vitumike katika ujenzi wa kazi hizo. Maneno ya Daktari katika dondoo hilo hapo juu, yanaunga mkono wazo hili la Hancock kuhusu wanataaluma wa kigeni na vifaa vya kigeni kutumika kama sehemu ya ufadhili na hivyo kuendeleza utegemezi. Kwa hivyo, asilimia kubwa ya mikopo hurudi kwa nchi iliyoutoa mkopo. Kwa misingi hii basi taifa litoalo mkopo ndilo hufaidika zaidi kwani wanataaluma wake hupata kandarasi katika mataifa machanga navyo vifaa kama vile mashine kutoka mataifa ya Kimagharibi hupata soko katika nchi zinazopokea mikopo.

Fanon (1963) anaonyesha msimamo sawa na ule wa Hancock kuhusu utegemezi. Anasema kuwa mataifa yaliyoendelea hutoa misaada na mikopo kwa masharti magumu kwa nchi changa. Kwa mfano anasema kuwa mataifa hayo husisitiza kiwango fulani cha mkopo kitumike kununua bidhaa fulani kama vile mashine kutoka kwao na pia yanasisitiza ujenzi wa vituo vya kijeshi katika nchi zinazopokea msaada ili kulinda kampuni za kimataifa katika mataifa machanga. Kwa njia hii mataifa ya Kimagharibi huendelea kuongoza nchi za Kiafrika. Huu ni ukoloni mamboleo. Mwandishi huyu anahitimisha kwa kusema kwamba mikopo ya kigeni ni biashara inayonufaisha wanakandarasi wa Kimagharibi na wanataaluma wachache kutoka nchi zinazofadhiliwa. Anadai kuwa kwa kila dola kumi zinazoletwa kama mkopo, dola saba hurudi kwa taifa lililotoa ufadhili huo kupitia kwa ununuzi wa bidhaa na uajiri wa wanataaluma wa kigeni.

Aidha, tamthilia za Arege zinaliangazia tatizo la utegemezi wa wanataaluma wa kutoka mataifa ya Kimagharibi kwa mataifa machanga. Anaonyesha kuwa mataifa machanga mengi huamini kwamba matatizo yao yanaweza kutatuliwa na wanataaluma hao wa kutoka nje. Hata hivyo inadhihirika kuwa wanataaluma hao hujia nchi changa huku wakiongozwa na ubinafsi na tamaa tu. Kwa mfano daktari wa kigeni anayemtibu mhusika Sele katika *Kijiba cha Moyo* haja yake ni pesa wala si maslahi ya mgonjwa. Hii ndio sababu daktari anakereka Sele anapomuuliza maswali kadhaa kabla ya kufanyiwa *plastic surgery*, oparesheni ambayo ingeleta madhara makubwa katika mwili wake. Daktari huyu anasawiriwa kama mtu asiyejali maslahi ya wagonjwa wake. Badala yake, anamkemea Sele jambo lililo kinyume na taaluma aliyoisomea. Ubinafsi wake unajitokeza wakati Daktari anapomwambia Sele kuwa gharama ingeongezeka kwa kila huduma ambayo angehitaji. Aidha tamaa yake inadhihirika anapomwambia Sele kuwa angemrudushia tu asilimia tano pekee ikiwa Sele hataki huduma. Mazungumzo yafuatayo yanadhihirisha jinsi Daktari alivyojaa tamaa na ubinafsi:

Sele : Hata sasa sina ugonjwa. Siumwi popote.

Daktari: Uaumwa!

Sele : Siumwi

Daktari: Najua unaumwa

Sele : Ikiwa ni hivyo sitaki mambo haya tena. Nirudishie *deposit* yangu niende.

Daktari: Uliyasoma maagano?

Sele : Kiasi. Sio yote.

Daktari: Tutakurudishia asilimia tano kwa kukiuka maagano.

Sele : Nilijua tangu hapo kwamba kipo kitu. Nilihisi kwamba utanichezea ila sikutaka kukushuku kabla ya kushuhudia. Sasa nimeshuhudia

... sasa najua hukuja kunijali. Umekuja kwa manufaa yako uliyoyaficha. (uk.55-56)

Utaalumu wa Daktari huyu unatiliwa shaka katika tamthilia hii. Daktari wa kigeni aliyetarajiwa kumtibu Sele ni dhahirisho kwamba suluhu ya matatizo ya mataifa maskini haimo kwa wageni bali kwa wenyeji. Kinachosisitizwa ni umuhumuwa kujitegemea. Tunapomlinganisha Daktari huyu wa kigeni na muuguzi wa kienyeji, Jamila, ambaye amehitimu na stahhada tu, inadhihirika kwamba yeye ni bora kuliko huyo mgeni. Kwa msingi huu ni wazi kwamba mwandishi anaonyesha kuwa matatizo ya Waafrika yanaweza kutatuliwa tu na Waafrika wenyewe wala si wageni. Hii ndio maana mwandishi anamtumia mhusika Jamila kugundua ugonjwa wa Sele na kuipa familia yake matumaini kwamba kuna dawa ingawa dawa hiyo inachukua muda na kwamba inahitaji uvumilivu. Katika mazungumzo yake na familia hii, inabainika kuwa ugonjwa huo huitwa *Body Dysmorphic Disorder*. Mazungumzo haya yanaahiria kuwepo kwa matumaini katika kuyakabili matatizo ya Kiafrika:

Bi.Rahma : (Kwa mshangao) Ushetani?

Jamila : Hata.

Bi.Rahma : Ushirikina?

Jamila : Hapana. Ni kutoridhika au kutoikubali nafsi yako mwenyewe. Unajiona dhaifu. Unajihisi unahitaji badiliko fulani. Lakini badiliko linalofanywa huwa si la nje. Wengi hawatambui kuwa tatizo limo ndani.

Zainabu : Katika fikira

Jamila : Hasa ni katika moyo. Moyo hauridhiki na siku zote kwa kuwa moyo ni mfalme, huamrisha fikira kutafuta suluhisho.

Bi,Rahma: Huo ugonjwa ni gani?

Jamila : Unajulikana katika lugha ya utabibu kama *Body Dysmorphic Disorder*. Yaani B.D.D. Ni hali ya mtu kujikuta kutopenda sehemu ya mwili wake na kuichukia

Zainabu: Ipo dawa ya kuurai moyo kujikubali?

Jamila : Ipo lakini inachukua muda. Hutaka kwanza kumrai mgonjwa. Akuamini wewe unayemtibu. (uk.91)

3.3 Sera za Taasisi za Kimataifa

Mashirika yanayoonekana yakiendeleza ukoloni mamboleo ni kama vile Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani na Shirika la Kibiashara la Dunia. Mashirika haya na mataifa yenye nguvu za kiuchumi yalibuni sheria iitwayo Mipango ya Usawazishaji Miundo kwa lengo la kufanikisha ulipwaji wa madeni kutoka kwa mataifa machanga. Hata hivyo mchakato wa utekelezaji wa sheria hii umeishia kusabababisha umaskini zaidi na ukosefu wa maendeleo kijumla kwa nchi hizi changa. Hii ni kwa sababu mpango huu ulizilazimisha nchi changa kupunguza bajeti zake

katika sekta kama vile elimu, afya na uimarishaji wa miundo misingi ili kiasi kikubwa cha bajeti hizo kitumike kulipia madeni. Hii ni njia ya mataifa ya Kimagharibi kujiendeleza kiuchumi. Utekelezaji wa sheria hii ulitekelezwa kupitia sera mbalimbali kama vile:

3.3.1 Mpango wa kutoajiri na ustaafishaji mapema wa wafanyikazi

Sera hii ilianzishwa na Benki ya Dunia pamoja na Shirika la Fedha la Dunia mwaka wa 1988 kwa lengo la kuzisaidia nchi changa kukabiliana na tatizo la ukosefu wa maendeleo. Mataifa yanayopokea ufadhili yalilazimika kupunguza idadi ya wafanyikazi pamoja na kusimamisha uajiri upya wa wafanyakazi katika sekta mbalimbali. Rodney (1976) anasema kuwa lengo lilikuwa ni kushinikiza mataifa machanga kupunguza utoajiwa huduma muhimu ili kupata pesa za kulipa madeni ya nchi zilizoendelea.

Katika tamthlia ya *Kijiba cha Moyo* tunaona kuwa sera hii ilizua athari hasi nyingi kwa wananchi wa mataifa haya kwa njia mbalimbali yakiwemo umaskini, mateso ya kisaikolojia, magonjwa na vifo kwa waasiriwa na hata ukosefu wa matumaini. Katika tamthlia hii kwa mfano, familia ya Sele inaathirika sana baada ya Sele kustaafishwa mapema kazini. Sele anasumbuka kiakili hadi kufikia kiwango cha kuwa na uchakaramu hasa kwa sababu ni jambo lililomjia bila kutarajiwa na pia kwa kuwa ana familia changa. Kifungu kifuatacho kinaliweka jambo hili wazi:

Musa: Wewe unavyoona ana shida gani?

Zainabu: Mimi sijui kwa kweli. Nasikia watu wameanza
Kumsema eti anatatizwa na hatua ya kuachishwa kazi

Musa: Kazi?

Zainabu: Kazi ndiyo. Wanasema watu. Wanasema kuwa hakuwa
hivi kabla ya kupoteza kazi.

Musa: Si kweli.

Zainabu : Hata kama si kweli maadam hili limetokea baada ya hali
hiyo watu wataamini hivyo..

Musa: Lakini si yeye tu aliyesimamishwa kazi. Tena wajua hakufutwa
ila kustaafishwa mapema ulivyostaafishwa wewe.

Zainabu : Yote yanategemea jinsi anavyoipokea hali hiyo. Ndoto na matumaini
ya mtu huzimwa ghafla akabaki kivuli tu. Hata mimi mwenyewe
nilijitahidi kuikubali hali hii ambayo sikuitarajia.(uk.24)

Kutokana na mazungumzo haya, suala la ukoloni mamboleo linadhihirika. Kwanza ni wazi kuwa mataifa machanga yanalazimika kustaafisha wafanyikazi wake mapema pasi kujali athari za kufanya hivyo kwa maisha yao. Hii ni thibitisho kuwa nchi za Kiafrika hata baada ya kupata

uhuru zinaongozwa na mataifa ya Kimagharibi upya. Wafanyikazi kama vile Sele waliostaafishwa mapema wanadhoofika kiafya na kiakili na kushindwa kuzidhibiti familia zao. Mamake Sele ingawa naye pia alikuwa amestaafishwa hakuathiriwa sana kama Sele. Hivi ni kumaanisha kuwa wafanyikazi waliowahi kuhudumu kwa muda mrefu hawakuhisi athari ya sera hii sana kama wafanyikazi wachanga maana wao hawakuwa na familia changa zilizowategemea. Mwandishi anaonyesha kuwa sera hii iliwahumiza vijana zaidi kuliko wazee. Hii ni kwa sababu kama anavyosema Zainabu matumaini na ndoto zao huzimwa ghafla. Sera hii pia inazua hali ya wasiwasi na kutamauka kwa waajiri kwani wao pia hujikuta katika njia panda wakishindwa kuboresha hali za kikazi. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, afisa anayesimamia masuala ya kazi na uchumi (**Diwani III**) analalamika kuhusu sera hii:

Mimi siuoni mpango wa kuwanufaisha watu wetu. Watu wengi hawana ajira. Walio nayo mishahara yao haitoshi wala hailipwi kwa wakati. Zaidi ya hilo, tumelazimishwa na kaka zetu kupunguza idadi ya wafanya kazi... Tunahhitaji kutafuta suluhisho la kudumu kwa dukuduku la watu wetu.(uk.20).

Tamthilia hii inadokeza kwamba ili mataifa ya Kiafrika yaweze kujikwamua kutokana na athari za sera hii ni sharti mataifa hayo yatafute njia mwafaka za kupunguza utegemezi uliokithiri. Kama anavyosema diwani huyu, hii ni sera ya kulazimishwa na hailengi kuwanufaisha Waafrika. Kulingana na nadharia ya ubaada-ukoloni, mhimili wa utengwaji wa kimataifa kwa misingi ya “Sisi” dhidi ya “Wao” ni muhimu sana. “Sisi” hapa ikimaanisha mataifa yenye nguvu na “Wao” ikiwakilisha mataifa yaliyobaki nyuma kimaendeleo. Hiki ni kigezo kikubwa kinachotumiwa na mataifa ya Kimagharibi kuyabagua mataifa ya Kiafrika kwa kupitia sera kandamizi kama hii ya ustaafishaji mapema. Sera hizi hubuniwa mbali lakini huishia kuyaathiri mataifa ya Kiafrika vibaya zaidi kuliko mataifa yaliyoendelea. Hii ndio sababu katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, tunaona Zainabu akilalamika kuhusu hali hii hivi:

Zainabu: Maamuzi yalikuwa yameishakufanywa mbali huko yakawa yaja kutekelezwa hapa.

Bi.Rahma : (Kwa upole) Maamuzi yakawa yamefanyiwa mbali huko?

Zainabu : Huko huko bibi. Vyombo hivi vyote vya huko ng’ambo lakini vina sauti. Wakubwa wanaviogopa. (uk.37)

Tunaona pia tamthilia hii inakejeli hali ambapo sera mbalimbali hutungiwa mbali hasa katika mataifa ya Kimagharibi na kulazimishwa kwa mataifa machanga. Kwa mfano sera ya

ustaafishaji wa wafanyikazi mapema haikutoka kwa mataifa machanga ya Kiafrika bali ya Kimagharibi. Wakati wa kubuniwa kwa baadhi ya sera hizi, Waafrika hawakushauriwa kuhusu ufaafu au ubaya wa sera hizo. Hii ni kwa sababu mataifa ya Kimagharibi hujiona bora kuliko mataifa machanga kwa misingi ya kiuchumi na kisiasa pamoja na kujawa na kasumba ya kikoloni. Hii ndio sababu nchi hizi hazioni haja ya kuyashauri mataifa haya machanga wakati wa kubuni kaida na kanuni zinazoongoza uhusiano wa kimataifa. Pia mataifa haya yaliyoendelea hayataathmini athari za sera kama hizo kwa familia na wafanyikazi. Hii ni njia maarufu ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Mazungumzo yafuatayo yanaonyesha tatizo hili:

Musa : Huu ulimwengu wa tupa chuma kumla chuma. Wenyewe Wana sababu zao. Sisi tunaambiwa na kulikubali lao. Hatuna hiari. (Kimya). Hata ukapinga na wao wameamua si kazi bure tu? Ni unyonge una mambo!

Zainabu : Pamoja na hayo, sisi vilevile ni washika dau. Ingefaa kutushauri na mapema.

Musa : (Anacheka) Wajua katika dau, kuna wenye kulishika na wenye kushikwa na dau. Na wakati mwingi tofauti si dhahiri.

Zainabu : Inavunja moyo. Wao ndio watu na sisi sanamu tu. (uk.24)

Kulingana na mazungumzo haya, inadhihirika kwamba mataifa machanga hulazimika kukubali hata sera wanazofahamu kuwa mbovu. Hata mataifa haya yakipinga ni kazi bure kama anavyosema mhusika Musa. Hali hii inaonyesha kutamauka kwa nchi zinazoendelea kufuatia ubaguzi wa mataifa yaliyoendelea. Maamuzi yanayoathiri ulimwengu mzima yanafanywa na nchi chache zenye nguvu nyingi za kiuchumi na kisiasa huku nchi zisizo na nguvu hizo zikilazimika kutekeleza maamuzi hayo tu.

Sera hii vilevile inasababisha kuongezeka kwa tatizo la ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana. Hii ni kwa sababu sera hii ya ustaafishaji pia ilisimamisha uajiri mpya suala ambalo lilikwamisha maendeleo na kuongeza viwango vya umaskini. Kwa sababu hii vijana wengi wanaomaliza masomo ya vyuo vikuu na kuhitimu na shahada hukosa kazi hata za viwango vya chini kama vile utopasi. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, suala la ukosefu wa kazi limekaririwa mara kadhaa. Kwa mfano katika kifungu kifuatacho, Meya anasisitiza kuwa wafanyikazi waliogoma wafutwe kisha vijana wasio na kazi waajiriwe:

Diwani I: Waache wagome, watajiponza wenyewe. Watakaogoma wafutwe mara moja na wengine waajiriwe.

Meya : Kuna vijana wengi wasio na kazi ilhali wamehitimu kutoka vyuo vikuu *fresh* kabisa. Wanaoleta siasa wapewe barua za kuwatimua na kuwakumbusha kuwa kazi wanazofanya si zao bali ni za Baraza la Cheneo.(uk.21).

Kutokana na mazungumzo haya, Meya anakiri kuwa mji wake ambao ni kiwakilishi cha miji mingine katika mataifa yanayoendelea, unakumbwa na ukosefu mkubwa wa ajira. Kwa sababu hii migomo ya wafanyikazi inakuwa jambo la kawaida. Haya ni matokeo ya utekelezaji wa sera baguzi zinazotokana na taasisi za Kimagharibi. Hii ni njia mpya ya kuzitawala nchi zilizotawaliwa awali na mkoloni na kwa hivyo kuendeleza ukoloni mamboleo. Migomo hii inapochacha, Diwani I anapendekeza pia vijana wengi wasio na kazi wajiriwe kuliziba pengo lililowachwa na wafanyikazi waliogoma:

Diwani 1: Tunaweza kutangaza katika vyombo vya habari. Pia tunaweza kutumia vipasaa sauti kuwatangazi vijana wasio na ajira. Watu wengi huko nje wana njaa. (uk.73)

Suala la migomo mingi ya wafanyikazi vilevile ni ishara kuwa mataifa machanga kushindwa kutimiza maslahi yao. Wanakumbwa na matatizo kama vile ukosefu wa mishahara, kuchelewa kwa mishahara yao, mishahara kulipwa nusu na mara nyingi kulipwa ikiwa imechelewa na ukosefu wa vifaa muhimu vya kazi kama vile glavu. Matatizo kama haya yanaweza kufasiriwa kama tokeo la sera hii ya ustaafishaji mapema na kutoajiri. Viongozi wa wafanyikazi wanapomtembelea Meya ili kushinikiza utatuzi wa matatizo yao, tunaona matatizo yanayowakumba yakiwemo mishahara duni na kupanda kwa gharama ya maisha. Wanateta hivi:

Tatu: Sisi wafanyikazi tuna matatizo mengi yanayotuzonga kwa muda mrefu. Kwanza, mishahara yetu ni midogo.

Ni lini mara ya mwisho sisi wafanyikazi wadogo tulipata nyongeza?

Beka: Hata hiyo zamani tulipata ilikuwa ni vipeni wiwili vitatu ilhali nyinyi mlipata nyongeza kubwa. Nyongeza hizo kubwa zinakuja baada ya vipindi vifupi ilhali sisi maskini wa mungu tuko pale pale chini. Sababu ya nyongeza yenu? Gharama ya maisha inapanda kila uchao, mara mfumko wa bei. Hiyo gharama inapanda kwenu tu? Huo mfumko unawafumukia nyinyi tu? (Uk.68)

3.3.2. Sera ya Kugawanya Gharama

Hii ni sera nyingine iliyoanzishwa na Benki ya Dunia katika mwaka wa 1988. Obamba (2006) anasema kuwa sera hii iliilazimisha Kenya kugawa gharama na wananchi wake katika sekta za elimu na afya. Anadai kuwa hali hii ilienda kinyume na mapendekezo ya tume ya Ominde (1964) yaliyoamuru serikali kusimamia gharama yote ya elimu. Hata hivyo sera hii haikuathiri nchi ya Kenya tu bali mataifa kadhaa ya Afrika katika miaka ya themanini. Obamba anasema kuwa kufikia mwaka wa 1991, sera hii ilisababisha migomo mingi miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu wakipinga kulazimishwa kutoa sehemu ya gharama ya elimu yao. Hii ni ishara kwamba sera hii haikupokelewa vyema.

Sera hii ilihitaji mataifa ya kusini mwa Jangwa la Sahara kugawana gharama na wananchi wake katika kutoa huduma za afya na za kielimu. Kujiiondoa kwa serikali kikamilifu katika utoaji wa huduma hizi kulichangia kudorora kwa viwango vya ubora vya afya na miundomsingi ya elimu hasa miundomsingi ya shule za umma (Pamba, 2012). Katika tamthlia ya *Mstahiki Meya* tunaona jinsi sekta ya afya ilivyoathiriwa na sera hii ya benki ya dunia. Tamthlia hii inaonyesha kuwa tangu mfumo huu kuanzishwa, serikali zililegea katika ununuzi wa dawa, vifaaa muhimu vya hospitali na uimarishaji wa miundomsingi ya hospitali. Hali hii ilichangia wananchi wengi wasiokuwa na mchango wao wa gharama kukosa huduma za kiafya. Katika tamthlia ya *Mstahiki Meya*, tunaona wananchi wengi wakilalamikia hali ya kuchanga gharama ya matibabu. Kwa mfano, mazungumzo baina ya nesi (Waridi) na daktari (Siki) yanaonyesha hali hii:

Waridi: Hawana hela za kulipia huduma wanazotaka. Wengine hawana hata karatasi za kunakilia udodosi wao.

Siki : Lakini hawa watu hawana pesa.

Waridi: Ni amri daktari. Kama wakubwa wenyewe wamekuishasema sisi tutafanya nini? Si basi tu? Bora kutazama tu. Nchi yenyewe ni changa kwa kila hali. Nao hao **Wazungu** wanahimiza mfumo wa kugawana gharama kutumika. Sisi tutafanya nini na nchi yenyewe maskini. Ombaomba? (uk.3)

Kwa sababu ya amri hii ya kugawana gharama, tunaona jinsi wananchi wengi wanavyoteseka kwa kukosa kuhudumiwa hospitalini kwani ni amri kuwa angalau wawe wanalipia baadhi ya huduma pamoja na kununua vijitabu vya kuandikiwa udodosi. Kwa sababu amri hii inatolewa na mashirika ya kimaatifa kama vile Benki ya Dunia, hii ni ishara tosha kuwa mataifa ya Kiafrika yanaongozwa kutoka mbali na hii ni njia ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Tamthlia inatashtiti

viongozi wa Kiafrika wanaotekeleza sera za kigeni kiholela bila kwanza kutathmini athari zake. Kuzorota kwa huduma za afya kunaashiriwa na ukosefu wa bidhaa muhimu kama vile maji, dawa, glavu na bidhaa nyinginezo za zahanatini. Kwa sababu ya ukosefu huu, daktari Siki akisema kwamba ili kuwapa wagonjwa matumaini, ni vyema baadhi yao hasa waliowezwa zaidi walazwe hata kama hamna dawa nao wengine wapewe mchanganyiko wa maji, sukari na chumvi.

Mfumo huu wa kugawana gharama unaposhindwa kuzikomboa nchi changa kutokana na umaskini na matatizo mengine, mashirika yaliyoibuni sera hiyo yakabuni sera nyingine ya kufanikisha malengo yao. Mkakati huo wa kimaendeleo uliitwa ‘Malengo ya Kimaendeleo ya Milenia’ (MDGs). Mataifa kadhaa ya Ulimwengu yalianza kutekeleza mkakati huu kwa awamu mbalimbali.

3.3.3 Malengo ya Kimaendeleo ya Milenia

Mwaka wa 2000, viongozi wa nchi 189 walikubaliana na pendekezo la Umoja wa Mataifa la kuwa na malengo manane ya kutimiza ifikapo mwaka wa 2015 (Ki-Moon). Malengo hayo yalikuwa:

Lengo 1: Kumaliza umaskini na njaa.

Lengo 2: Kufikia elimu ya msingi kwa kila mwananchi.

Lengo 3: Kuimarisha usawa wa kijinsia.

Lengo 4: Kupunguza vifo vya watoto.

Lengo 5: Kuboresha afya ya uzazi.

Lengo 6: Kuzuia ongezeko la ukimwi, malaria na magonjwa mengine.

Lengo 7: Kuboresha hali ya mazingira.

Lengo 8: Kuunda ushirikiano wa kiamendeleo duniani.

Ingawa malengo haya yalikusudiwa kuboresha hali ya maisha katika ulimwengu mzima hasa katika mataifa yaliyokuwa nyuma kimaendeleo, hayakufanikiwa kwa kiwango kilichotarajiwa. Hii ni kwa sababu mataifa mengi hasa ya Kiafrika yalitupilia mbali mipango yao ya kimaendeleo na kuanza kuitekeleza hii mipya kikasuku. Kila nchi hubuni mipango yake ya kimaendeleo ya miaka mitano au kumi kutegemea mazingira yake ya kihistoria, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mipango hii hutekelezwa kupitia taasisi mbalimbali kama vile mahakama, bunge, mabaraza ya miji pamoja na wizara mbalimbali. Katika tamthlia hii inaonekana wazi kwamba haikufaa kwa mataifa machanga kutupilia mbali mipango yao ya maendeleo kwa kuiga ile ya kutoka nje. Hii ni kwa sababu kila nchi ina mahitaji maalum kwa wananchi wake. Pia tamthlia hii inakashfu uzingatiaji wa sera zilizobuniwa bila kuwahusisha wananchi wa nchi husika. Mazungumzo yafuatayo baina ya Siki na Meya yanadhihirisha hali hii:

Siki: Tunatembea lakini hatuendi mbele. Kwenda tunaenda lakini kinyumenyume. Kwa nini tujidai kuwatibu watu ilhali dawa hamna na hata zikawepo hawawezi kuzimudu? Afya bora na ya lazima kwa kila mwananchi ni moja kati ya malengo ya mji katika **mpango wake wa maendeleo wa miaka kumi**. Hamwafikirii watu waliowachagua. Mnajifikiria tu. (Kimya). Kama huku si kuwatusi wananchi basi ndio kutembea nyuma ya punda aliyeudhika.

Meza: (Kwa ukali) Hapa ni kwangu Siki. Usinifuate kwangu kunitusi. Mipango ya miaka kumi ni upuuzi. (Kimya) Sisi tuna **mipango ya kimaendeleo ya milenia**. Huu ndio mwongozo na haya ndiyo muhimu. Tumeshaingia katika viwango vya kimataifa. Kupinga haya ni kama kumkama simba mwenye watoto.

Siki: Upendavyo Mstahiki Meza. Vizuri. Lakini kumbuka kuwa kufikia kumi ni sharti kuanza na moja. Kumi haifikiwi katika ombwe tupu. Kukubali kufuata waliyoamua watu wengine bila kuwashirikisha watu wetu ni hatari. Huu ni ukoloni mamboleo. Ni namna mpya ya kutawaliwa. Chunga. Unamkanyanga nyoka mkia! (uk.14-15).

Kuna mambo matatau kuu yanayoibuka kuokana na mazungumzo haya. Kwanza, mataifa mengi ya Kiafrika hayasongi mbele ingawa viongozi wake hawataki kuukubali ukweli huu. Wanadai kuwa kuna maendeleo ilhali hali za maisha ya wananchi haziboreki. Kwa mfano katika dondoo hili, tunaona Meza akisema kuwa wameingia katika viwango vya kimataifa. Yeye ni kiwakilishi cha viongozi wasio na ufahamu wa hali halisi ya maisha ya watu wao. Huduma za kimsingi kama vile za afya zinadorora na viwango vya umaskini kuongezeka lakini kiongozi wa Cheneo haoni ukweli huu.

Pili, mataifa mengi machanga yana mipango yao ya kimaendeleo lakini mipango hiyo haithaminiwi na viongozi wa mataifa hayo. Kwa mfano, jiji la Cheneo lina mpango wa maendeleo wa miaka kumi lakini Meza anautaja mpango huu kama “upuuzi.” Yeye anatambua tu malengo ya milenia kwa sababu yamependekezwa na mataifa ya Kimagharibi na kupuuza sera za kikwao zinazoambatana na mazingira yao. Mataifa haya ya Kimagharibi yanapobuni sera na

kuzishinikiza kwa mataifa machanga ni njia ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Tatu, kama anavyosema Siki, kukubali yaliyoamuliwa na wengine ni hatari. Kufanya hivi ni kuendeleza ukoloni mamboleo. Hatari inayodokezwa hapa ni maasi yanayoweza kuanzishwa na wananchi wakidai uongozi unaotambua uhalisia wa mazingira yao.

3.4 Hitimisho

Katika sura hii tumebainisha kuwa mataifa ya Kimagharibi hutumia unafiki mkubwa katika kuzilaghai nchi za Kiafrika kupitia suala la utegemezi wa kiuchumi. Kulingana na utafiti huu, ni wazi kuwa wanaotoa misaada hasa ndio hufaidika zaidi kuliko mataifa pokezi kwa sababu misaada hiyo huja kwa masharti magumu ambayo huumiza mataifa machanga. Kwa mfano tumeonyesha kuwa mikopo hulipwa kwa riba za juu na kwa muda mrefu jambo ambalo huathiri hata vizazi vya baadaye ambavyo havikufaidika kutokana na mikopo hiyo.

Taasisi za kiamtaifa pia zimeonekana kama zinazoendeleza ukoloni mamboleo hasa kupitia sera zake zinazoyabagua mataifa machanga. Kwa mfano imedhihirishwa kwamba baadhi ya sera hubuniwa bila majadiliano na mataifa ya Kiafrika ilhali ndiyo yanayoathiriwa zaidi na maamuzi ya kimataifa. Sera kandamizi kama vile ile ya ustaafishaji wa wafanyikazi mapema imeathiri familia nyingi za Kiafrika kiuchumi na hata kisaikolojia. Tumeonyesha pia kuwa sera ya ugawanaji gharama katika utoaji wa huduma muhimu imezidisha hali duni za maisha kwa wananchi wa ma

SURA YA NNE

UBEBERU WA KITAMADUNI NA MATUMIZI YA MBINU ZA KIUTAWALA ZA KIKOLONI KATIKA UENDELEZAJI WA UKOLONI MAMBOLEO

4.1 Utangulizi

Katika sura hii tunahakiki jinsi tamthlia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* zinavyoangazia kuathirika kwa utamaduni wa Kiafrika kwa sababau ya uigaji wa utamaduni wa Kimagharibi. Uigaji huu umesababisha kuwepo kwa utamaduni mahuluti miongoni mwa wananchi wa mataifa yaliyotawaliwa na mkoloni. Baadhi ya vipengele hivi vya utamaduni wa Kimagharibi ni lugha za kigeni, elimu ya kigeni, vyakula na vinywaji vya kigeni na utumizi wa huduma za afya kigeni. Sura hii pia inaonyesha baadhi ya mbinu za kiutawala zilizotumiwa na wakoloni na ambazo zingali zinatumiwa na viongozi wa Kiafrika katika utawala wa nchi zao. Mwisho, sura hii inaangazia baadhi ya mbinu za lugha zilizotumiwa kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

4.2 Ubeberu wa Kiutamaduni

Kama anavyosema Said (1977) mataifa ya Kimagharibi yalichukulia kuwa utamaduni wao ulikuwa bora kuliko ule wa mataifa ya Kimashariki na yale ya Kiafrika. Maoni haya ni msingi wa nadharia ya ubaada-ukoloni inayoongoza utafiti huu. Wazo hili lilienezwa hadi likashika nguvu na kuaminiwa na baadhi ya Waafrika kama ukweli. Fanon (1963) akiutetea utamaduni wa Kiafrika anawalaumu wasomi wa Kiafrika hasa nchini Aljeria kwa kuikubali dhana hii ya udhaifu wa utamaduni wa Kiafrika. Anasema kuwa hisia za udhaifu wa utamaduni wa Kiafrika zilizoenezwa na wakoloni zilishika nguvu kwa sababu zilipitishwa katika mfumo wa kielimu.

Wamisheni, ambao waliwatangulia wakoloni waliendeleza vita dhidi ya utamaduni wa Kiafrika huku wakishinikiza utamaduni wa Kimagharibi kuheshimika. Kwa kutekeleza jambo hili, walionyesha uovu wa utamaduni wa Kiafrika. Walipiga vita hali za maisha kama vile dini za kienyeji, mavazi ya kienyeji, lugha za kiasili, utabibu wa Kiafrika na hata nyimbo za Kiafrika. Kwa sababu hii, Waafrika wakaanza kuiga na kupendelea utamaduni wa Kimagharibi huku wakipuuza ule wao.

Kama inavyoonyesha nadharia ya ubaada-ukoloni, utamaduni mseto hujitokeza kama athari kuu ya ukoloni katika mataifa yaliyotawaliwa. Huu ni utamaduni unaobeba vipengele vya utamaduni wa watu waliotawaliwa na ule wa mkoloni kama vile matumizi ya lugha za kigeni pamoja na lugha za kiasili. Mataifa ya kikoloni hayakuendeleza tu dhuluma za kiuchumi na kisiasa bali pia za kiutamaduni. Kwa mfano nchi zilizotawaliwa na Uingereza zilibaki kuendeleza mifumo ya kiutamaduni ya Uingereza kama vile mavazi, dini, nyimbo na utumiaji wa lugha ya Kiingereza kama lugha rasmi. Katika sehemu ifuatayo tunachambua vipengele hivi kama vinavyojitokeza katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*:

4.2.1 Elimu ya Kigeni

Mkoloni mkongwe alileta elimu ya Kimagharibi hasa kupitia wamisheni ambao walifika kwanza Hii ni kutokana na imani kwamba bara la Afrika lilikosa ustaarabu na njia moja ya kuwastaarabisha Waafrika ilikuwa kupitia elimu ya Kimaghribi. Kwa kufanya hivi, walipuuzilia mbali elimu ya kiasili iliyokuwepo katika jamii nyingi za Kiafrika. Hata hivyo, elimu hii ya kigeni ilitolewa kiubaguzi ambapo watu weusi walipewa elimu duni huku Wazungu wakijipa elimu bora (Ngugi 1986)

Kulingana na Nyerere (1967) elimu hii ya kikoloni haikupangwa ili kuwatayarisha vijana kulitumikia taifa lao bali ilikuwa ya kutimiza haja ya kuingiza tamaduni za kikoloni katika bara la Afrika. Anaendelea kufafanua kuwa elimu hii ilikusudiwa kuwafunza watu waendeleo kuwatumikia wakoloni wakongwe. Baada ya uhuru, mataifa ya Kiafrika badala ya kubuni mifumo ya elimu inayooana na mazingira yao maalum yaliendeleza mifumo ya elimu ya kikoloni. Hali hii ilipelekea kuwepo kwa elimu ya kibwege ambayo haikuwasaidia vijana kupata kazi hata baada ya kuhitimu. Tamthilia hizi zinakosoa mitindo hii ya elimu katika mataifa yanayoendelea akionyesha kuwa elimu hii inatamausha mno hasa kwani haiboreshi maisha ya mtu anapohitimu. Kwa mfano Meya akizungumza na Gedi anasema:

Meya: Waambie kuwa ikiwa hawataki kuonyesha shukrani kwa wanayofanyiwa na baraza letu tukufu, nitawafuta kazi. Wafahamishe wazi wazi kuwa wapo vijana wengi huko nje waliohitimu kutoka vyuo vikuu na wameshindwa kupata hata utopasi. Unaelewa?

Gedi : (Anasimama na kujikaza kabisa) Ndiyo Mstahiki Meya. (Uk.32)

Katika muktadha huu Meya alikuwa akimkumbusha Gedi kuwa wafanyikazi waliogoma wakidai nyongeza ya mishahara anaweza kuwafuta kwa sababu kuna watu wengi waliosoma na kuhitimu lakini hawana kazi. Hii ni ishara kwamba elimu ya Cheneo haijaweza kufikia malengo yake. Ni elimu duni isiyomsaidia msomi kujitegemea kimaisha. Viongozi wa Kiafrika walioshika hatamu za uongozi baada ya mkoloni mkongwe kuondoka hawakuboresha miundo misingi na mifumo hiyo ya elimu ili iafikiane na mazingira ya Kiafrika. Rodney (1976) anaunga mkono wazo hili akisema kwamba nia ya mkoloni haikuwa kudumisha mfumo wa kijamaa uliokuwepo wala kuleta mabadiliko kwa Waafrika. Nia yao ilikuwa kuwatayarisha Waafrika wachache ambao wangeajiriwa kumsaidia Mzungu kutawala. Anafafanua kuwa kazi ambazo Mwafrika aliandaliwa kwazo ni ukarani na unyampala.

Elimu inapaswa kusawazisha tofauti za kitabaka miongoni mwa wanajamii kwa kuwapa watu wa tabaka la chini uwezo wa kiuchumi na kijamii. Uwezo huu hupunguza viwango vya umaskini na mwishowe mianya ya kitabaka huweza kuzibika. Hata hivyo, viongozi wa nchi huru za Kiafrika wanaendeleza tofauti hizo kwa kuitoa elimu hiyo kwa misingi ya kitabaka kama walivyofanya wakoloni. Watoto wa maskini wanaenda shule duni huku wale wa wazazi wa tabaka la juu hasa viongozi wakiwasomesha watoto wao katika shule za kifahari na baadhi yao wakiwapeleka watoto wao ng'ambo katika vyuo vikuu vya kifahari. Hii ni njia ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Kwa kufanya hivyo, viongozi hawa hawaoni haja ya kuboresha elimu ya umma kwa sababu watoto wao hawasomei nchini. Katika *Mstahiki Meya* tunaona Meya akikubali hali hii katika mazungumzo yake na Bili:

Bili: Mama anakupigia simu kutoka wapi tena? Au amesafiri kwenda nyumbani!

Meya: Hata kidogo. Amekwenda ng'ambo kuwaona watoto wake. Siku ile nilikuambia kuwa hawasomei hapa tena. Viwango viko chini kidogo.

Bili : Nakumbuka uliisha kunitajia kuwa wangeenda kusomea ng'ambo. Mpango mzuri.

Meya: Ndiyo hivyo bwana. Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno. Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali.

Bili: (Anatabasamu) Kweli bwana. Elimu ya kina yakhe hii. (Kimya). Vipi mama? (uk.26).

Tukitazama muktadha wa mazungumzo haya ni wazi kwamba wananchi wanaojiweza hupendelea elimu ya ng'ambo na kupuuzilia ya kikwao ambayo inasawiriwa kama duni na ambayo inaweza tu kuwafaa maskini. Hii ni ishara kwamba mataifa mengi ya Kiafrika hujidai tu

kuwa yana uhuru lakini ukweli ni kwamba yanatawaliwa na mataifa ya Kimagharibi. Huu ni ukoloni mamboleo.

Tamthilia hii inakosoa kukengeuka kwa baadhi ya viongozi wa Kiafrika. Wamesawiriwa kama watu walioshindwa kudhibiti uongozi wa nchi zao kwa kuzihakikishia huduma za kimsingi kama vile dawa, elimu bora na maji. Kwa mfano Meya anapozungumza na Bili anasema, “Siku ile nilikuambia hawasomei hapa tena. Viwango viko chini kidogo...Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno...Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali”. (uk.26). Tamthilia inamtashtiti Meya kwa udhaifu wake. Kama kiongozi wa jiji ni jukumu lake kuboresha elimu kwa wananchi wote. Mwandishi anaitumia mbinu hii kukebehi viongozi kama Meya ambao hupuza taasisi zao kwa kupendelea taasisi za kigeni. Kipengele cha fani cha uhusika pia kimekuzwa sana katika dondoo hili. Kwa mfano, kiongozi wa Cheneo Mstahiki Meya, anajitokeza kama aliyetamaushwa na utamaduni wa kigeni sana hadi anakosa kujali maslahi ya wananchi wake. Hii ni kwa sababu hatuoni akitia juhudi zozote kuimarisha elimu ya watu wa tabaka la chini. Pia anajitokeza kama kiongozi badhirifu kwani anatumia pesa za umma (Baraza la Cheneo) visivyo kama vile kuwasomesha watoto wake ng’ambo bila kuwajali watoto wa maskini. Mfanyikazi wa Baraza hili, Tatu analalamikia hali duni ya elimu kwa maskini akisema: “Kuna raha gani kutazama watoto wetu wanapofukuzwa shuleni kwa sababu hatuwezi kuwalipia karo?” (uk.70)

Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* vilevile inakosoa hali ambapo elimu ya kigeni inamtenganisha msomi na utamaduni wake asili na hasa jamii yake. Kazi hii inaonyesha kuwa elimu ya kiasili iliyokuwepo kabla ya ukoloni ilikuwa na mafunzo muhimu ya kimaadili kama vile heshima kwa wazee na wazazi. Katika tamthilia hii, tunaona jinsi elimu ya Kimagharibi inavyowakengeusha wasomi wa Kiafrika na kuwafanya kutoheshimu wazee wao. Kifungu kifuatacho kinadhihirisha jambo hili:

Bi.Rahma: Aisha desturi gani hii? Mtoto wa kike toke nje sisi wazee wako tuko hapa, kisha utupuuze na kuelekea kwenye vitabu? Ndivyo elimu yenu hii ya Kizungu inavyowatuma kufanya? Huu ndio ustaarabu kwenu?

Aisha: Si hivyo. Kuna jambo ambalo aliniambia Sele nami nikawa silielewi vizuri. Nikataka nifuatilie na kupata usuli wake kabla sijasahau.

Zainabu: (Kwa ukali) Jambo la kuambiwa tu ndilo linakufanya utuone sisi kama vitu tu! Linakufanya utuvunjie heshima sisi wazee wako. Eeh.

Bi.Rahma: (Kwa Zainabu) Jambo gani ambalo asingetuuliza sisi tukampa ufafanuzi. (Kwa Aisha) Elimu hiyo mnayoitafula vitabuni na kuilipia sisi mnaotudharau ndiyo tunayo hapa (Akishiria kichwa). Wameitoa kwetu wakaitia humo vitabuni.(uk.19).

Kulingana na mazungumzo haya, ni wazi kwamba elimu ya kiasili haifai kupuuzwa kwani ndio msingi wa elimu ya kisasa kama anavyosema Bi.Rahma ndiyo huchotwa na kuhifadhiwa vitabuni. Ni dhahiri kuwa elimu ya Kimagharibi haipaswi kutufanya tusahau elimu yetu ya kiasili. Mwandishi anaashiria kuwa elimu ya kigeni ina kasoro zake na kwamba haifai kwaminika kana kwamba imefikia upeo wa ustaarabu. Elimu ya kiasili pia ilifunza ustaarabu kwa njia yake. Ngugi (1981) Anaonyesha elimu ya kigeni kama iliyowabagua Waafrika kwani ilidhihirisha chuki dhidi ya majina ya Kiafrika, lugha zao, mazingira yao, umoja wao na uwezo wao wa kiakili na kimwili. Anaonyesha kuwa Waafrika walioelimika walijitenga na utamaduni wao na kutamani utamaduni wa Kimagharibi. Hii ndio kauli tunayoona ikaririwa na tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* hii katika dondoo hilo lililonukuliwa hapo juu.

Kwa kuhitimisha sehemu hii, inadhihirika kwamba elimu ya kigeni ilimwathiri Mwafrika kimaadili alipoiga tabia za Wazungu na kuacha kudhamini tabia zake asili. Rodney (1976) anasema kuwa elimu ya kigeni ilikuwa ya dhuluma, ujidunishaji, ya kujenga hali ya kuchanganyikiwa kiakili na kuzua maendeleo pungufu.

Elimu ya Kimagharibi inamkengeusha Mwafrika hadi anafikia kiwango cha kujidharau kimaumbile na kitabia. Kwa sababu hii, Waafrika wanawaiga Wazungu kwa kila njia. Mwafrika anasawiriwa kama kikaragozi cha Mzungu. Tunaona katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, mhusika Sele akijaribu kuabadili uso wake kupitia *plastic surgery* ili ufanane na ule wa Wazungu. Anasema: “Sipendi hili kovu.....uso kwa ujumla...Sipendi hii pua...Pua mbaya hii”. (uk.33-34).

Aidha, elimu ya kigeni iliambatana na usambazaji wa **lugha za kigeni**. Athari kubwa ya kitamaduni iliyowachwa na ukoloni mkongwe na ikabaki hadi leo katika maisha ya wenyeji hadi leo ni lugha za kikoloni. Lugha hizi ni kama vile Kiraransa, Kingereza, Kijerumani, Kiispania n.k. Nchi zilizotawaliwa na mataifa ya Kimagharibi zimeendelea kuzitumia lugha hizo hadi kufikia kiwango cha kuwa sehemu ya utamaduni wao. Katika mataifa mengi yaliyotawaliwa lugha hizo zimekuwa lugha rasmi. Kwa mfano, Kiingereza ni lugha rasmi nchini Kenya, Uganda na Tanzania. Kwa sababu hiyo, waandishi wa mataifa yaliyotawaliwa na mkoloni nao wameendelea kuandika kazi zao kwa lugha hizo ngeni kwani ndizo walizofundishwa shuleni.

Hata hivyo, wapo waandishi wachache walioandika kwa lugha zao za kienyeji. Ngugi (1986) anasema kuwa wapo waandishi walioandika kwa lugha za Kafrika kama vile Shaban Robert aliyeandika kazi zake kwa Kiswahili na Chifu Fagunwa aliyeandika kwa Kiyoruba. Ngugi anafafanua kuwa baadhi ya lugha za Kizungu zilitumika sana hadi baadhi ya wasomi wa Kiafrika kama vile Ezekiel Mphahlele wakapendekeza kuwa lugha za Kifaransa na Kingereza zitumike kuwaunganisha Waafrika waliozungumza lugha nyingi. Mphahlele aliona kuwa ingefaa hasa kwa wapiganaji wa uhuru kuzitumia lugha hizo ili kuwashirikisha Waafrika wengi katika mapambano yao dhidi wakoloni.

Hata hivyo, baadhi ya waandishi wa Kiafrika walichukia kuandika kazi zao kwa lugha za kigeni lakini ikawa hawana njia nyingine ya kuandika ila hii. Hii ni kwa sababu elimu ya kigeni waliyopata ilisisitiza umuhimu wa kuzifahamu lugha za Kimagharibi na kupuuza lugha za kikabila. Ngugi (1986) anaonyesha jinsi mtanziko huu ulivyomuathiri Achebe. Achebe katika mwaka wa 1964 katika hotuba iitwayo, “Mwandishi wa Kiafrika na Lugha ya Kiingereza”, alihoji:

Je ni haki kwa mtu kuitupilia mbali lugha yake ya kwanza na kufuatia ya mwingine?
Inaonekana kama usaliti mkubwa na huzalisha hisia za kihatia. Lakini kwangu hakuna uteuzi. Nimepewa lugha na nakusudia kuitumia. (uk.7).T.Y

Kipengele hiki cha utamaduni wa kigeni kimewaathiri Waafrika tangu enzi za Achebe hadi sasa kwani hata waandishi wa kisasa wanaonyesha athari hizi katika kazi zao. Tamthilia tunazohakiki zinawaonyesha wahusika walioathirika na lugha ya Kingereza hasa kwa sababu ya kupata elimu ya kigeni. Ifuatayo ni mifano kutoka kwa tamthilia ya *Mstahiki Meya*:

Daktari Siki akizungumza na Diwani III kuhusu ukosefu wa dawa na vifaa muhimu zahanatini anasema... “Dawa tulizo nazo ni *painkillers* tu”...(uk.6). Kauli hii inaashiria hali mbovu ya hospitali za umma ambapo mara nyingi dawa zinazopatikana ni za kiwango cha chini mno kiubora.

Meya akizungumza na Gedi kuhusu mgomo wa wafanyikazi wanaoandamana, anasema.... “Mwambie *chief security* awaite polisi mara moja”...(uk.32). Meya anatumia maneno haya kwa lengo la kusisitiza uzito wa hatua anayotaka kuchukua. Naye Tatu, ambaye ni kiongozi wa wafanyikazi anaripoti kwa Diwani III jinsi Meya anavyokataa kuzungumza na wawakilishi hao wa wafanyikazi. Anasema, “Tumeambiwa kuwa *diary* yake imejaa ilhali watu wanakufa”...(uk 32). Mwandishi ameteua maneno ya lugha hii ili kutilia mkazo ukatili wa Meya.

Diwani III akimweleza daktari Siki jinsi sheria za mji zinavyompa Meya nguvu nyingi, anataja baadhi ya kanuni kama vile *Collective Responsibility, Mayors’ Act* na *Riots Act* ambazo zinampa Meya mamalaka mengi. Inasemekana kuwa Meya akitumia sheria hizi anaweza kumchukulia hatua kali mtu yeyote anayempinga. Kuwepo kwa sheria hizi ni ishara kuwa ukoloni mamboleo unaendelezwa kupitia sheria za kikoloni. Baadhi ya sheria zinazotawala mataifa huru ya Kiafrika zingali zinatumia sheria zilizotungwa na wakoloni. Kwa mfano, taasisi ya umeya na sheria za miji nchini Kenya ziliaanzishwa na wakoloni.

Baadhi ya visababishi vya matumizi mapana ya mbinu hii ya kuchanganya ndimi ni kuwa wahusika hao wamepata elimu ya kigeni hasa katika muktadha huu elimu inayosisitiza umilisi wa Kiingereza uliosisitizwa na wakoloni. Sababu nyingine ni kwamba huenda ikawa wahusika hao wana msingi dhaifu wa lugha ya Kiswahili. Hii ni ithibati kuwa lugha za Kiafrika zilipuuzwa na mfumo wa elimu wa nyakati za kikoloni na athari hizi zikaendelea hadi sasa.

Katika *Kijiba cha Moyo*, tunaona mhusika Jamila ambaye ni muuguzi akitumia lugha ya Kiingereza kumweleza Sele hali yake yake ya kiafya:

Jamila: (Kwa Sele) Si mbaya.

Sele : Kwa vipi?

Jamila : 144 kwa 91

Sele : Hivyo ndio nini?

Jamila : *Pulses* zako si mbaya wala *pressure*. *Borderline*.
Sele : *Borderline?* (uk.42)

Sababu kuu ya wahusika hawa kuchanganya ndimi ni kuwa wapo katika muktadha maalum (Sajili ya hospitalini) na kwa sababu hii wanashindwa kujieleza vilivyo katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kushindwa huku ni ishara ya ukandamizwaji wa lugha za kienyeji na ukandamizwaji wa utamaduni wa Kiafrika kijumla. Ukandamizwaji wa utamaduni ni muhimili muhimu katika nadharia ya ubaada-ukoloni inayoongoza utafiti huu. Hata hivyo ni vyema kukuza lugha za Kiafrika kwa kuandika kwa lugha hizo na kuuasi ukoloni wa kilugha.

Ngugi (1986) anasema kuwa kwa kuandika kwa lugha za kigeni ni kama kuendeleza utumwa wa kikoloni. Anasema, “Nini tofauti kati ya mwanasiasa anayesema kuwa Afrika haiwezi kuendelea bila ukoloni mamboleo na mwandishi anayesema kuwa Afrika haiwezi kuendelea bila lugha za Kimagharibi. Anaonyesha jinsi Waingereza walivyolazimisha matumizi ya lugha ya Kiingereza katika mfumo wa shule na kuwanyima wenyeji ubora wa lugha ya kutoka mazingira yao. Lugha za kikabila kama vile Kikuyu hazikutumiwa shuleni na wanafunzi wangepadhikiwa kwa kuongea lugha hizo. Kwa sababu hii, Ngugi anakiri kuwa mwanafunzi alilazimika kuongea Kiingereza, kuandika Kingereza na kufikiria kwa Kingereza. Hali hii ilizua ukengeushi ambao pia ulitiliwa nguvu na masomo ya historia, jiografia na muziki ambayo yalihusu bara la Ulaya. Hali hizi zilimtoa msomaji na mtumiaji wa lugha ya Kiingereza kutoka ulimwengu wake halisi na kumpa ulimwengu mwingine asiuelewa. Kwa misingi hii basi tunaona kuwa lugha ya Kiingereza kwa kweli ni chombo cha kuendeleza ukoloni mamboleo.

Vyakula na vinywaji ni sehemu kubwa ya utamaduni wa watu. Watu wenye utamaduni maalum hujivunia mitindo yao ya vyakula na vinywaji. Wakoloni walipoingia katika bara la Kiafrika walileta mitindo mipya ya vyakula kwa Waafrika. Mitindo hiyo iliendelezwa na Waafrika baada ya Mzungu kuondoka. Hii ni kwa sababu Waafrika hao walikuwa wameukubali utamaduni huo mpya. Kwa sababu hii, Waafrika wengi wamebaki kuagiza vyakula hivyo kutoka kwa mataifa yaliyowatawala. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, tunaona kiongozi wa jiji la Cheneo akiwangoja wageni wanaotarajiwa kuzuru mji wake. Anaagiza mvinyo kutoka Urusi na divai kutoka kutoka Ufaransa. Anasema:

Meya: Nitawapa mapokezi ya kupigiwa mfano. Hoteli ya kifahari. Vyakula kutoka kila utamaduni duniani. Si sembe. La hasha. Mvinyo nitauagiza kutoka Urusi na divai kutoka Ufaransa, wale na kunywa wajue kuwa

Cheneo si mji hivi hivi. Wajue kuwa ufadhili wao kwa baraza unadhaminiwa. (uk.25)

Katika uzungumzi nafsi huu, tunaona kuwa baadhi ya Waafrika wanabagua vyakula vinavyotokana na utamaduni wao kama vile sembe na kupania vile vya kigeni. Hii ni ishara ya ukoloni mamboleo. Mbinu ya uzungumzi nafsi imetumika katika kifungu hiki hasa ili kuonyesha matamano ya Meya. Katika kisa hiki, Meya anazungumza peke yake akiwa katika ofisi yake huku akipitia pitia mafaili mbalimbali. Jambo hili linaashiria kuwa Waafrika wengi hasa watawala huthamini tu vitu vya Kimagharibi na kudunisha vya kwao. Kando na hili, nukuu hili pia linaonyesha hali ya ubadhirifu wa mali ya umma unaoendelezwa na viongozi wa Kiafrika. Meya kwa mfano anatumia pesa za mkopo kuagiza vinywaji kutoka Urusi na Ufaransa. Kwa njia hii mwandishi anaonyesha kuwa misaada inayoyafikia mataifa mengi haitekelezi yaliyokusudiwa kwani inaelekezwa kwa mambo yasiyofaa.

4.2.2 Huduma za Afya za Kigeni

Shirika la Umoja wa Kimataifa liliibuka na malengo ya kimaendeleo ya milenia ili kuboresha sekta mbalimbali za kiuchumi kwa mataifa ya ulimwengu. Kati ya malengo hayo manane, matatu yalihusu huduma za afya. Kwa mfano kuna yaliyohusu afya ya uzazi na upunguzaji wa vifo kwa watoto wachanga. Hata hivyo, mataifa mengi yanayoendelea hayakuweza kutimiza malengo haya kufikia mwaka 2015 kama ilivyoratibiwa. Kassaye (2016) anasema kuwa malengo haya yaliwekwa ili kushinikiza mataifa yaliyokuwa nyuma kimaendeleo kuboresha huduma za afya kwa wananchi wao.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, tunaona jinsi viongozi wa Kiafrika wanavyokataa kuboresha huduma za afya kwa sababu wao hutembelea mataifa ya kigeni kutafuta huduma za afya. Kwa mfano mazungumzo yafuatayo kati ya Bili na Meya yanathibitisha jambo hili:

Bili : (Anatabasamu) Vipi mama? Hivi alishapata mgeni au vipi?

Meya: Bado karibuni.

Bili : (Kwa bashasha) Mara ile ya mwisho tulipokuwa pamoja alionekana amechoka sana.

Meya: Ndiyo maana alisafiri ng'ambo. Madaktari wetu hawa wa kubabaisha tu. Kule ng'ambo ndiko kuliko na wakunga wenyewe. Sikutaka kubahatisha. Halafu tena mtoto akizaliwa huko anapata uraia wa huko tena.

Bili: Kweli?

Meya: Kweli kwani hujui?

Bili : Sikujua. Hata mimi sasa naona nitamtuma mke wangu kuko huko wakati wake ukitimia.(uk.26-27)

Uchambuzi wa kina wa mazungumzo haya unadhihirisha kwamba, viongozi wengi wa mataifa ya Kiafrika wanataka watoto wao wawe na uraia wa nchi za Kimagharibi kama wanavyopendekeza Bili na Meya. Hii ni ishara ya ukoloni mamboleo. Viongozi kama hao daima matamaniao yao yapo katika mienendo ya Kimagharibi. Pia ni wazi kwamba viongozi wengi hawana imani na taasisi zao kama vile hospitali zao na madaktari wao. Kwa sababu hii wanaona afadhali kuwapeleka watoto na wake zao ng'ambo ili wapate huduma za huko. Kwa sababu hii, hawaoni haja ya kuziboresha taasisi hizo. Matokeo ya mapuuzwa haya ni ukosefu wa dawa na vifaa muhimu hospitalini kama inavyoonekana katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

Huku kutopenda vya kwao kunasababisha viongozi wengi kuagiza dawa kutoka nje na hata madaktari wa kigeni kuitwa ili kuwahudumia baadhi ya wagonjwa wenye uwezo wa kifedha. Kwa mfano katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, Sele anaagiziwa daktari kutoka taifa moja la Kimagharibi. Daktari huyu wa Kizungu anaharakisha kutaka kumfanyia Sele '*plastic surgery*' bila kwanza kubaini chanzo cha Sele kuchukua ngozi yake na sura yake hasa pua. Daktari hata hivyo, anatumika kijazanda kuonyesha tamaa na ubinafsi wa mataifa ya Kimagharibi wakati yanapohusiana na mataifa machanga. Mazungumzo yafuatayo yanashadidia jambo hili:

Daktari: Unaumwa?

Sele: Siumwi

Daktari: Najua unaumwa.

Sele: Ikiwa ni hivyo sitaki mambo haya tena. Nirudishie *deposit* yangu niende.

Daktari: Uliyasoma maagano?

Sele: Nilijua tangu hapo kuwa kipo kitu. Nilihisi kwamba utanichezea ila sikutaka kukushuku kabla ya kushuhudia...Sasa najua hukuja kunijali. Umekuja kwa manufaa yako uliyoyaficha .(uk.55-60)

Mazungumzo haya yanaonyesha kuwa huku mataifa machanga yakiwathamini madaktari wa nchi za Kimagharibi, madaktari kwa upande wao hawawathamini wagonjwa hao na hulenga kuwapunja. Daktari katika muktadha huu ni kiwakilishi cha dhuluma za kiuchumi dhidi ya mataifa machanga zinazoendelezwa na mataifa yaliyoendelea. Kwa mfano anamlazimisha Sele kukubali kuwa anaumwa ilhali haumwi. Hii ndio maana Sele anamwambia kuwa alikuja kwa

maslahi yake wala si ya mgonjwa. Yeye ni ishara ya uroho wa ukoloni mkongwe ulioambukizwa kwa wakoloni mamboleo. Huu ni upeo wa ukoloni mamboleo. Matokeo ya kudhamini huduma za afya na taasisi za afya za kigeni ni kuwepo kwa zahanati na hospitali zisizokuwa na dawa, vifo vya watoto ambavyo vingezuilika, migomo ya wahudumu wa afya, kujiuzulu kwa wauguzi na ukosefu wa vifaa muhimu katika hospitali kama vile glavu na vinginevyo. Kushadidia ukweli kwamba mataifa ya Kiafrika yanaagiza huduma za madaktari kutoka nje, tunaona daktari anayemtibu Sele mwenyewe akikiri kuwa ametoka mbali na kwamba hata vifaa vya kazi navyo vimetoka huko huko atokako yeye:

Daktari: Mimi niko hapa kukufaa. Ukitaka nirudi nitarudi. Maarifa nimekuja nayo. Ala za kazi nimekuja nazo vile vile kutoka huko mbali.(uk.54).

Kama inavyoonekana katika sehemu hii, ni wazi kwamba mwandishi analenga kuutetea utamaduni wa Kiafrika ambao umeyumbishwa mno na maingiliano kati ya nchi za Kimagharibi na za Kiafrika. Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* imetumia fumbo la nyimbo tatu kuonyesha jinsi utamaduni wa Kiafrika unavyofifia kufuatia kupendelewa kwa utamaduni wa kigeni hasa na vijana. Kwa mfano Aisha anamchagulia Sele wimbo wa Kiafrika wa taarab akidhani kuwa angefurahia lakini Sele anawacha kucheza akisema kuwa wimbo huu ni taratibu mno na kwamba kila anapoucheza anajikwaa. Jambo hili linadhihirisha kwamba Mwafrika anazidi kuuasi utamaduni wake kwa kuiga ule wa Kimagharibi:

Aisha : Mbona hivyo tena? Au hukuupenda wimbo?

Sele : Hata. Wimbo mzuri

Aisha : Cha mno nini basi?

Sele : Mwili wangu haupatani na mahadhi ya wimbo. Taratibu mno!
Kila nikicheza muziki wa taarab najikwaa. Nimeshaizoea hii miziki yenye kasi. Naipenda taarab ila sipatani nayo ukumbini. Imeniasi. Au niseme mimi nimeiasi. (uk.7-8)

Sele anapowekewa wimbo wa pili wa aina ya ‘Rap’, anafurahia na kuucheza vizuri. Wimbo huu ni kiwakilishi cha utamaduni wa Kimagharibi unaowavutia Waafrika wengi. Anafurahia na kuanza kuucheza ingawa pia anawacha baada ya muda mfupi kwa madai kuwa amegundua kuwa wimbo huu ni kama unamuamrisha. Anapowekewa wimbo unaoesema “New Kid on the Block”, Sele amasema kuwa wimbo huo pia ni utumwa kwa sababu una matumizi ya maneno ya kigeni. Tunaona hali ya kinaya katika tabia ya Sele kwa sababu yeye anakataa wimbo wa taarab wenye

mizizi ya Kiafarika na wakati huo huo anaona kwamba kuimba wimbo uliotungwa kwa lugha ngeni ni utumwa. Hata hivyo, kupitia mbinu hii, mwandishi anafanikiwa kuonyesha hali halisi ya bara la Afrika kwamba Waafrika wanaelewa kuwa utamaduni wa Kimagharibi ni sawa na utumwa lakini wanashindwa kujitenga nao.

4.3 Matumizi ya Mbinu za Kiutawala za Kikoloni

Wakoloni walitumia njia mbalimbali katika kutawala sehemu mbalimbali za ulimwengu. Mbinu hizo zilitofautiana kutoka nchi moja ya kikoloni hadi nyingine. Hata hivyo, baada ya uhuru Waafrika nao waliiga mbinu hizo na kiziendeleza lakini kwa viwango tofauti tofauti. Kwa kufanya hivi, viongozi hao wameishia kukuza ukoloni mamboleo. Hii ndio sababu baadhi ya viongozi hao wapya waliitwa ‘Wazungu weusi’. Baadhi ya mbinu hizo ni:

4.3.1 Tenga Utawale

Tenga utawale ni njia ya kujiweka na kujiendeleza katika mamlaka kwa kuwafanya waliochini yako kufarakana ili washindwe kuungana kwa lengo la kukuondoa mamlakani (Stewart, 1951). Kitabu hiki kinaendelea kufafanua kuwa sera hii ilihusu utengwaji wa watu kwa misingi ya kikabila, kijinsia, kidini na kitabaka katika historia ya mataifa mbalimbali. Kinatoa mfano wa jinsi Uingereza ilivyowatenganisha Wahindu na Waislamu katika nchi ya India kwa kuwadhulumu Waislamu na kuwapendelea Wahindu. Pia Wahindi kijumla walitenganishwa na Wapakistani nchini India wakati wa utawala wa Uingereza huko.

Katika nchi ya Naijeria wakoloni waliyatenganisha makabila ya Ibo na Yoruba kwa misingi ya kidini. Kama anavyosema Arowolo (2010), mkoloni alitoa dini ya kikristo kwa kabila la Ibo pekee na kwa njia hii Wayoruba wakabaguliwa na kutengwa. Vilevile, anatoa mfano wa nchi ya Rwanda, ambapo Wabelgiji waliyatenganisha makabila ya Tutsi na Hutu kwa kuwapendelea Watutsi ambao walikubaliwa kufuga mifugo kama vile ng’ombe, wakapewa elimu bora na kazi nzuri. Wazungu hawa waliwalazimisha Wahutu na Watutsi kubeba vitambulisho vilivyoonyesha makabila yao. Makabila hayo hayakujitofautisha kikabila kabla ya mjo wa Wazungu. Tofauti hizi zilifikia kilele mwaka wa 1994 wakati vita vya wenyewe kwa wenyewe vilipolipuka.

Mbinu hii ya tenga utawale ilirithiwa na Waafrika baada ya uhuru ambapo baadhi ya viongozi waliochukua hatamu za uongozi waliwatenga wenzao hasa waliokuwa na maoni tofauti na yao kuhusu uongozi. Viongozi wa taasisi mbalimbali na walioshikilia vyeo vikuu serikalini pia nao walianza kuwatenga waliowapinga na kuwapendelea wale waliowaunga mkono katika utawala wao. Baadhi ya viongozi hao huwaona wenye maoni tofauti kama adui zao na kwa sababu hii hukataa kuwahusisha katika miradi ya kimaendeleo. Tamthilia tunazozichunguza zinaliangazia tatizo hili. Kwa mfano, Meya anawateua madiwani tu wale wenye ushawishi mkubwa wa kisiasa kwenye kamati za Baraza la Cheneo na kuwatenga wengine. Anapogundua kuwa diwani mmoja ana maoni tofauti tofauti na yake na kuwa na msimamo thabiti anaanza kumtenga katika mikutano maalum. Hii ni baada ya Meya kubaini kwamba diwani huyu (Diwani III) hawezi kutumika kama kikaragozi. Tunaona jambo hili katika mazungumzo yafuatayo:

Diwani I: Haswa! Wale wenye ushawishi zaidi wanaweza kuteuliwa kuongoza kamati hizo. Mstahiki Meya uwezo unao. Katiba ya Cheneo inakupa mamlaka tosha kubuni kamati nyingi upendavyo na kuteua viongozi wake. (Kwa upole) Kwa unyenyekevu tunakuomba kutumia mamlaka hayo.

Diwani III: Ni wazo zuri ila kamati hizo huenda zisiwe na umuhimu kwa Baraza la Cheneo

Meya : Sina shaka zitakuwa na umuhimu mkubwa...Sioni kwa nini zisizibuniwe na wanachama wake kulipwa vizuri kwa kuhudumu katika kamati hizo.(uk.21-22).

Kutokana na mazungumzo haya, tunaona kuwa Meya anakubali wosia wa Diwani I wa kubuni kamati nyingi na kuwaweka madiwani wenye ushawishi tu katika kamati hizo. Inaonekana pia kwamba kuunda kamati nyingi kuliko idadi ya kawaida hakutazua upinzani dhidi yake kulingana na maoni ya Diwani III.

Katika mazungumzo baina ya daktari Siki na Diwani III, diwani huyu analalamikia jinsi anavyotengwa katika mikutano ya kamati hizo:

Diwani III: Ikiwa una hulka ya kudadisidadi mambo yanavyoendeshwa barazani wanakutema katika vikao. Wataitwa wanaounga mikono kila atakacho Meya hata kama hakifai na wewe mwenye udadisi kuachwa nje hata kama jambo linalohusika linataka ushauri wako.

Siki: Ajabu hiyo. (Uk.48)

Ni wazi kwamba ili kuepuka upingwaji na kuhahikisha kuwa matamania ya Meya yanapitishwa kwa urahisi, mbinu ya tenga utawale ilimfaa sana kiongozi wa jiji la Cheneo kama

inavyoonekana katika dondoo hilo hapo juu. Matumizi ya mbinu ya tenga utawale iliendeleza uongozi mbaya kwani wale viongozi wazuri wanaopinga mipango ya wizi wa mali ya umma aidha hufutwa kazini ama hukataa kushauriwa mara nyingi kutokana na misimamo yao thabiti. Katika tamthlia ya *Mstahiki Meya*, hali hii inaendeleza tatizo la ufisadi. Bili, Meya, Diwani I na Diwani II wanapanga kuiba fimbo ya Meya na kuiuza katika nchi za ng'ambo kisha wanaahidiana kuwa Diwani III asiambiwe lolote. Hii ni kwa sababu yeye ni mtetezi wa umma na asiyependa ufisadi. Wahusika hawa wakiwa katika kikao cha kupanga wizi wa fimbo ya Meya na kuiuza ng'ambo, wanasema:

- Meya:** Bwana uchumi na kazi asipate habari hizi kamwe. Akilipata hili basi atakuwa amepata fursa ya kuwachochea watu kufanya maandamano. Lazima mnihakikishie kuwa huyu sumu hapati hata fununu ya jambo hili. Hii ni bomu inayoweza kutulipukia usoni.
- Diwani II:** Kweli kabisa ndugu Mstahiki Meya. Yule ni mtu mwenye wivu. Akijua tumekutana bila yeye kushirikishwa itakuwa balaa moja kwa moja
- Meya :** Ndiyo sababu sikuthubutu kumwalika hata leo. Mtu hata siri haijui kuitunza!
- Bili :** Anaropokwa tu.
- Diwani II:** Anajidai kuwa mkamilifu. Eti hana doa.(uk.34)

Katika mazungumzo haya, inadhahirika kwamba anayepinga njama ya uuzwaji wa fimbo ya Meya anatengwa na kukashfiwa hata na madiwani wenzake kwani yeye anaweza kujulisha umma kuhusu njama hiyo.

Kipengele cha fani cha uhusika pia kimejengeka mno katika kifungu hiki. Kwa mfano, Meya anajitokeza kama kiongozi fisadi, mwenye ubaguzi na asiye na msimamo dhabiti. Kwa mfano, anaingia kwa urahisi mno katika mtego wa Bili wa kuiuza fimbo ya Meya, kifaa ambacho ni iahara ya uongozi wa jiji. Lengo la Bili ni kupata pesa kutoka kwa Baraza ilhali yeye si mfanyikazi wa Baraza la Cheneo, naye Meya hatathmini matokeo ya kitendo chake. Diwani I na Diwani II nao wanajitokeza kama wenye tamaa, fisadi na wenye ubinafsi mwingi. Kwa mfano wao wanakiri kuwa wako tayari kufa na siri kuhusu kupotea kwa fimbo ya Meya. Kwa kuhitimisha sehemu hii, tunaona kuwa mbinu ya tenga utawale imetumika sana katika tamthlia ya *Mstahiki Meya* na kama tulivyodokeza mwanzo. Kwa sababu iliasisiwa na wakoloni na ingali inatumika, basi hii ni njia inayoendeleza ukoloni mamboleo.

4.3.2 Dhuluma dhidi ya Wafanyaikazi

Ukoloni ulipoanzishwa katika Afrika ulileta mifumo ya kibepari ya kiuchumi ambayo ilibadili njia ya uzalishaji mali katika Afrika. Ubepari ulileta mfumo wa ulipaji ujira kwa wafanyikazi, kwa mfano, masetla waliponyakua mashamba, waliwahitaji Waafrika kufanya kazi kwenye mashamba yao. Kwa hivyo, wakatafuta mbinu ya kupata ujira kutoka kwa Waafrika kama vile kumtosa ushuru na kumlipa Mwafrika malipo duni. Ochieng na Ogot (1996) wanasema kuwa wazungu walijilipa mishahara mizuri, wakifuatiwa na Wahindi na Waafrika wakifuatia kimalipo nchini Kenya. Sababu ya tofauti hizi kama wanavyosema Ogot na Ochieng ni kuwa wakoloni waliona kuwa mishahara mkubwa ulifaaa ili kumvutia mzungu kufanya kazi Afrika na pili kumwezesha kuwa na maisha mazuri kuliko yale ya wenyeji.

Waandishi hawa wanasema kuwa Mzungu aliongozwa na chukulizi kuwa mwafrika alikuwa mvivu kazini na hii ikawa misingi ya malipo duni. Wanaendelea kusema kuwa kwa sababu ya ubaguzi huu wa kimalipo na hali mbaya za mazingira ya kazi, wafanyikazi hawakuwa na jingine ila kuanzisha migomo ili kutetea hadhi zao. Wanatoa mifano ya migomo iliyotokea katika maeneo mengi ya Kiafrika kama vile mgomo wa wafanyikazi wa mji wa Lagos 1897 na 1945, migomo ya wachimba madini nchini Zimbabwe na Afrika kusini na migomo ya wafanyikazi wa reli nchini Ghana 1945. Wakoloni katika mataifa mengi ya Kiafrika walihodhi mashamba makubwa na makampuni mbalimbali ambapo waafrika walijajiriwa. Hata baada ya uhuru, kampuni hizo zilibaki na kuendeleza unyanyasaji huo wa wafanya kazi.

Viongozi wa Kiafrika waloshika hatamu za uongozi nao waliiga na kuendeleza dhuluma za unyanyasaji huo dhidi ya wafanyikazi ambao walikuwa Waafrika wenzao. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, wafanyakazi wa Baraza la Cheneo wanadhulumiwa kwa kulipwa mishahara duni inayocheleweshwa kando na kutozwa kodi. Kwa kufanya hivi, viongozi wapya wa kiafrika wanaendeleza ukoloni mambo leo kwa sababu wakoloni pia waliendeleza dhuluma hizi. Matokeo ya unyanyasaji wa wafanyikazi ni migomo ya mara kwa mara na hali hii inapozidi, baadhi yao hujiuzulu. Meya akionyesha kutojali kwake kuhusu maslahi ya wafanyikazi anasema:

Meya: Usitie shaka Kheri. Hilo lisikusumbue. Hao waliogoma mimi nawafahamu sana. Uongozi wa baraza la mji haukuanza jana. Kungekuwa na vyeo hii leo ningekuwa na Ph.D (kimya). Watu hao

watarudi kazini baada ya siku chache na siku hizo walizogoma hawatalipwa. Wewe hujajua kuwa mahitaji ya kila siku yatawalazimu kurudi? Mhitaji siku zote ni mtumwa. (Uk.54)

Kiongozi huyu wa jiji anaonyesha kuwa hana nia ya kushughulikia maslahi ya wafanyakazi bali anataka wasitishie mgomo na kurudi kazini kwa sababu wao ni wahitaji. Kisa hiki kinaonyesha sifa kuu ya Meya kama kiongozi katili na mwenye kiburi. Tamthilia hii aimetumia methali, “Mhitaji ni mtumwa” kusisitiza hali ya kukata tamaa ya wafanyakazi.

Matatizo yanayowakumba wafanyakazi yanadhihirika kupitia mazungumzo yanayofanyika baina ya Meya na wawakilishi wa wafanyakazi (Medi, Beka na Tatu). Matatizo hayo ni kama vile kucheleweshwa kwa mishahara yao, kulipwa nusu ya mishahara na kubaguliwa wakati madiwani wanapopata nyongeza ya mishahara. Ubaguzi huu unawaathiri tu wafanyakazi wa ngazi za chini kama vile wanaofanya kazi za ufagizi na utopasi. Wanaoshikilia nyadhifa za kisiasa kama vile madiwani hupata nyongeza kila wakati wanapohitaji tu. Tamthilia hii inakosoa hali hii hasa ikizingatiwa kwamba wafanyakazi na wanasiasa wote huathiriwa na gharama ya maisha na hasa mfumko wa bei. Matatizo mengine yanayowakumba wafanyakazi ni ukosefu wa hazina ya kuwasaidia wanapostaafu. Hata hivyo, juhudi zao za kuwasilisha malalamishi yao kwa kiongozi wa baraza zinagonga mwamba kwa sababu ya ukali na kiburi cha kiongozi huyo. Meya wa jiji kwa mfano anajiusisha tu na maandalizi ya wageni wanaotarajiwa kuzuru mji na kuwapuuza viongozi wa wafanyakazi. Mazungumzo yafuatayo yanabainisha baadhi ya hoja hizo:

Medi: Ujira na ajira si neno. Lakini ajira yafaa kuwa ya kujali .

Tatu: (Kwa Meya) Sisi wafanyakazi tuna matatizo mengi yaliyotuzonga kwa muda mrefu. Kwanza mishahara yetu ni midogo. Ni lini mara ya mwisho sisi wafanyakazi wadogo tulipata nyongeza!

Beka: Hata hiyo zamani tuliyopata ilikuwa ni vipeni viwili vitatu ilhali nyinyi mlipata nyongeza kubwa . Sababu ya nyongeza zenu? Gharama ya maisha inapanda kila uchao, mara mfumko wa bei. Hivyo gharama inapanda kwenu tu? Huo mfumko unawafumikia nyinyi tu ? (Uk. 67-68)

Unyanyasaji wa wafanyakazi kama ilivyokuwa katika zama za mkoloni unatumiwa na viongozi na waajiri wengi hadi sasa ili kujilimbikizia faida na kuwadhibiti wafanyakazi. Hii ni kwa sababu mashirika na makampuni ya kibepari huandama tu faida kwani wafanyakazi huchukuliwa kama bidhaa. Kwa sababu ya ubidhaaishaji huu wa wafanyakazi, mfanyakazi anachukuliwa kama

chombo cha kununuliwa au/na kuuzwa. Hii ni mbinu inayoendeleza ukoloni mamboleo kwa sababu kama tulivyoonyesha awali, wakoloni wakongwe waliitumia sana mbinu hii katika mahusiano yao na Waafrika. Akiliunga mkono swala hili, Mbatiah (2016:54) anasema kwamba mabepari huwaajiri watu wengine kuwafanyia kazi na kuwalipa ujira duni. Anaendelea kufafanua kwamba kwa kufanya hivi wao huendelea kutajirika huku wafanyakazi nao wakiendelea kudidimia katika umaskini. Kama asemavyo Rodney (Ameshatajwa), mabepari wa kikoloni walilenga kujifaidi zaidi kupita uhusiano wao na Waafrika, katika uwekezaji wao. Waliwekeza tu katika sekta zilizolenga faida kwao kwa haraka na zilizokuwa na hatari chache.

Unyanyasaji wa wafanyakazi pia unalazimishwa kwa mataifa yanayoendelea kutoka kwa mataifa ya Kimagharibi na taasisi za kimataifa kama vile Benki ya Dunia. Katika *kijiba cha Moyo*, tunaona jinsi baadhi ya watu waliteseka baada ya nchi zao kulazimishwa kuwafuta wafanyakazi kazi. Mhusika Sele kwa mfano, anapatwa na tatizo la kisaikolojia na kuwa na tabia za kiwendawazimu. Jambo hili linaisumbua familia yake sana kwani familia inafikiri kuwa ana ugonjwa usioeleweka. Mamake Sele, Zainabu, ambaye pia alistaafishwa, anaakiri kuwa kwa wafanyakazi wachanga kustaafishwa mapema ni jambo gumu kulikabili hasa ikiwa mtu ana familia changa.

Zainabu : Tulikuwa wa kwanza kustaafishwa kabla ya wakati kwa shinikizo lao. Tulijitoa kupinga lakini wapi? Maamuzi yalikuwa yameisha kufanywa mbali huko yakawa yaja kutekelezwa hapa.

Bi.Rahma: (kwa upole) Maamuzi yakawa yamefanyiwa mbali huko ?

Zainabu : Huko huko bibi. Vyombo hivi vyote vya huko ng'ambo lakini vina sauti. Wakubwa wanaviogopa. Hata wakikataa ndo itafaa nini? Ikiwa vidagaa huliwa na mikizi chambilecho papa? Siku zote vidagaa ni vidagaa tu japo katika vidagaa hao yupo kinara wao. Sisi tulifadhahika hasa tuliposimamishwa ingawa hatukuwa mbali kustaafu. Wao waliokuwa ndo wamezianza mbio? Akili zinaweza kumruka mtu! (Uk. 86-87).

Ni wazi kuwa kulingana na dondoo hili shinikisho la kuwadhulumu wafanyakazi kupitia kustaafishwa mapema lilitoka nje, hasa mataifa ya Kimagharibi na kulazimishwa kwa nchi changa. Tamthlia imetumia jazanda ya vidagaa, mikizi na papa ili kufanikisha maudhui ya ukoloni mamboleo. Papa ni samaki mkubwa ilhali kidagaa ni samaki mdogo. Mwandishi ameteua samaki hawa ambao hufahamika sana ili kuwasilisha ujumbe wake kwa njia yenye

mnato zaidi. Papa anawakilisha nchi tajiri za Kimagharibi nao vidagaa ni viwakilishi vya nchi changa za Kiafrika zinazopewa masharti kutoka nje na kufuata tu. Kutokana na mazungumzo haya, nchi zenye nguvu za kiuchumi pamoja na taasisi za kimataifa hulazimisha mataifa machanga kuwastaafisha wafanyakazi ili nchi hizo changa ziweze kuyalipa madeni zilizokopa kutoka kwa nchi zilizoendelea. Hii ni njia kuu inayoendeleza ukoloni mambo leo.

4.3.3 Matumizi Yasiyofaa ya Polisi

Mkoloni alipoingia barani Afrika alikuwa na picha hasi mno kumhusu mwafrika. Kama anavyosema Fanon (1963), Mwafrika alichukuliwa kuwa kiwakilishi cha uovu. Anasema kuwa machoni mwa mkoloni mtu asili alionekana kama mkosa maadili, asiyekuwa na hisia zozote za kimaadili na hata kiwakilishi cha ukosefu wa maadili. Anaendelea kufafanua kwamba, kwa kweli yeye huchukuliwa kama adui wa maadili na kwa muktadha huu ni upeo wa uovu. Hii ndio maana mkoloni aliidhinisha matumizi ya nguvu za polisi katika kumdhibiti mwafrika. Ili kufanikisha utawala wa kikoloni, maofisa wa polisi walitumia nguvu kupindukia katika kuwadhhibiti raia. Mfumo huu wa utumiaji nguvu za polisi kupindukia ungali ukitumiwa na watawala wapya wa Kiafrika. Hivyo wanaendeleza ukoloni mamboleo. Ogot na Ochieng (1996) wanasema kuwa nchini Kenya ukoloni ulitangulizwa kwa matumizi ya nguvu za kihuni na kuendelezwa kwa nguvu hizo. Wanafafanua kuwa wakoloni waliendeleza matumizi ya ghasia hizo hadi zikawa kama ugaidi dhidi ya Waafrika kupitia kufungwa bila sababu, kuzuiliwa kutembea na hata mauaji.

Watawala wa kikoloni waliteuliwa na serikali ya Uingereza na wala hawakuchaguliwa na Waafrika ilhali Waafrika hao walitarajiwa kuwakubali na kuwatumikia watawala hao. Kwa hivyo, watawala hao waliwatumikia Waingereza na taifa lao wala hawakujali kamwe kuboresha maisha ya Waafrika. Kwa sababu ya haya, wakoloni waliwateua magavana, wakuu wa wilaya, machifu na polisi kuwasaidia kutumia nguvu katika uongozi wao. Rodney (1976) anatilia mkazo dhana hii akisema kuwa ni wazi kuwa kila mtu anazifahamu mbinu zilizotumiwa na mkoloni kutawala Afrika. Anafafanua kwamba kulikuwa na magavana, maofisa wa kikoloni na askari polisi.

Baada ya mataifa mengi kupata uhuru, yaliridhi asasi za kiutawala zilizokuwa zikitumiwa na mkoloni, kwa mfano mfumo wa utawala wa kimikoa nchini Kenya ulidumishwa hadi mwaka wa 2010 ambapo katiba mpya ilipopunguza nguvu za mfumo huo kwa kuleta mfumo wa ugatuzi. Katika mfumo huo wa awali, vyombo vya kidola kama vile polisi na mahakama vilitumiwa kuwakanadamiza wapinzani na kuendeleza utawala wa kiimla. Vikosi vya polisi vilikuwa kipengele muhimu cha utawala na kudumisha uongozi. Tamthlia ya *Mstahiki Meya* inakashifu matumizi ya nguvu zaidi za askari polisi kwa kuonyesha kuwa wanatumiwa vibaya na viongozi wa jiji kama vile Mstahiki Meya. Kila mara panapotokea mkutano wa wafanyakazi kupanga mgomo, polisi wanaitwa na kuwatawanya. Katika kikao cha Meya na madiwani wenzake, diwani anayesimamia usalama anamhakikishia Meya kuwa polisi watatumia nguvu kuwanyamazisha wanaompinga. Kwa njia hii tunaona kuwa mfumo huu ni kama ule wa wakoloni:

Meya : Basi mmeyasikia! Tufanyeje Bwana Usalama?

Diwani I : Mstahiki Meya kitengo changu mimi hakina shida. Ni kuwaamrisha vijana wetu wa usalama kulinda Baraza.

Meya : Mara hii sitaki kusikia mtu amekufa. Mwaka wa kuomba kura utakapofika sitaki mizuka yao kuniandama. Itaniletea tatizo wakati wa uchaguzi.

Diwani I : Nitawaambia kutembeza virungu vyao kiasi cha kuwafanya kutulia nyumbani.(uk.19)

Kulingana na muktadha wa dondoo hili, ni dhahiri kuwa matumizi ya polisi ni njia moja anayoitumia Meya kujiendeleza uongozini kama walivyofanya wakoloni. Kwa mfano, diwani anayesimamia usalama anakiri kwamba polisi watatumia rungu kuwapiga waandamanaji. Vitendo kama hivi vinasababisha hofu kwa wananchi na hata vifo. Unafiki wa viongozi unadhihirika Meya anaposema kuwa watu wasiuawe kwani ni wakati wa uchaguzi. Kwa kuwanyamazisha wapinzani hasa wafanyakazi wanapogoma, Meya pia huita polisi ambao huja kwa ghasia na vitoa machozi ili kuwatawanya wafanyakazi wanapoandamana. Kwa mfano, Gedi anaporipoti kuwa wafanyakazi wamegoma, Meya anasema:

Gedi : Mstahiki Meya *Sir*, wanadai mishahara zaidi, wanadai dawa Hospitalini, wanadai kukuona, wanadai takribani kila kitu.

Meya : Mwambie *chief security* awaite polisi mara moja.

Gedi : *Yes sir* . Thank you *sir* (Anajikaza, anapiga saluti na kuondoka mbio) (uk. 32)

Katika mazungumzo haya, ukatili wa Meya unadhihirika kupitia jinsi anavyojibu madai ya wafanyakazi kwa vitisho na ghasia za polisi. Hali hii inaashiria kwamba polisi hutumiwa vibaya na baadhi ya viongozi dhaifu kuwakandamiza wapinzani wao. Pia katika dondoo hili, sifa kuu

za Gedi zinadhihirika. Kwa mfano, anajitokeza kama kibaraka cha Meya. Matumizi yake ya kuchanganya ndimi pia ni ishara ya athari ya ukoloni mamboleo hasa kwamba amepata elimu na lugha ya kigeni kupitia mfumo wa kielimu uliosisitiza ufahamu wa lugha za kigeni badala ya zile za kiafrika. Athari ya ukoloni mamboleo pia inaonekana kupitia jinsi Gedi anavyomuogopa Meya kivitendo na kiuzungumzi kama vile tabia ya kujikaza na kumpigia saluti Meya kila mara anapozungumza naye, jinsi mwafrika alivyomuogopa mkoloni mkongwe.

Matumizi mabaya ya maofisa wa polisi yanamshtua Diwani III ambaye analalamikia jinsi wanavyotumia nguvu nyingi katika kuwafurusha wafanyikazi wakati wa mgomo. Anasema:

Diwani III : Tamaa hatujakata. Hata hivyo inavunja moyo kuona mambo kama haya ya watu kuvurimizwa na askari wanapotaka kushtakia hali zao. Mji si mji tena askari wameutwaa. Hata mimi ninaona vigumu kuingia humo wakati wafanyakazi wetu wanafurushwa. Mji bila watu si mji. Ndiyo maana nikaamua afadhali kubaki nyumbani na kufuatilia matukio yanayojiri.(uk.47)

4.3.4 Unyakuzi wa Maliasili

Tabia ya unyakuzi wa ardhi iliambukizwai kutoka kwa wakoloni hadi kwa waafrika waliochukua hatamu za uongozi baada ya nchi zao kupata uhuru. Tunasema hivi kwa sababu Wazungu walipofika Afrika walijinyakulia mashamba makubwa katika sehemu zilizokuwa na rutuba nyingi, Waafrika nao wakasongeshwa kwenye sehemu zisizofaa kwa kilimo. Viongozi wapya waliochukua hatamu za uongozi nao walianza kunyakua mashamba yaliyokuwa ya wazungu na hata nyumba zilizokuwa zao. Viongozi wa kisasa wa nchi za kiafrika na viongozi wa taasisi mbalimbali pia wanaendeleza unyakuzi huu. Tamthilia ya *Mstahiki Meya*, inakosoa tabia hii kwa kumchora Mstahiki Meya kama kiongozi mwenye tabia ya kunyakua viwanja vya umma. Kwa mfano, Meya akizungumza na Bili anamringia jinsi alivyo na viwanja vingi. Ingawa hakiri kuwa viwanja hivyo alivinyakua, ni wazi kwamba vimepatikana kwa njia isiyo ya haki na ukweli.

Meza: Nisipokuwa nazo, nani atakuwa nazo? Mimi nimeuza vipande vyangu vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii. Nimebakisha vitano *incase*. Wewe nilikugawia vinne. Unaweza kuuza kimoja au viwili kwa ajili hiyo. Vingine viweke kwa ajili ya hao watoto unaowahangaikia, hasa ile *prime plot*.

Bili : Wazo zuri kweli (uk. 27)

Tunaona katika mazungumzo haya, Meya amesawiriwa kama kiwakilishi cha viongozi wa kiserikali wanaonyakua mali ya umma hasa ardhi kitendo ambacho asili yake ni ukoloni. Kwa sababu ya tabia hii anapata viwanja vingi hadi anawapa rafiki zake baadhi ya vipande hivyo vya ardhi. Hali hii inamwezesha Meya kuwasomesha watoto wake ng'ambo bila kutumia hela zake mwenyewe na kwa kufanya hivyo, anaendeleza ubadhirifu wa mali ya umma.

Tamthlia ya *Kijiba Cha Moyo*, imetumia jazanda mbalimbali (tunaonyesha jazanda hizo katika sehemu ijayo) kuonyesha jinsi mataifa yenye nguvu za kibepari, yanavyojiendeleza chini ya mwavuli wa kuyasaidia mataifa ya Kiafrika. Mataifa haya yanadhihirisha unafiki wao kwani hudai kwamba yanakuja katika bara la Afrika kuwasaidia watu wa bara hili. Hata hivyo kiini cha kuja kwao hubainika baadaye wanapoanza kunyakua malighafi ya mataifa machanga na kuyapeleka kwao ili kunawirisha viwanda vyao. Sele anapogundua unafiki huu wa kimataifa anasema:

Sele: Nilijua tangu hapo kuwa kipo kitu. Nilihisi kuwa utanichezea ila sikutaka kukushuku kabla ya kushuhudia. Sasa nimeshuhudia...Siku nyingi umenichezea lakini ukawa unaficha huku kunichezea kwako. Sasa najua kuwa hunijali. Umekuja kwa manufaa yako uliyoyaficha katika hoja yangu. (uk. 56)

Kutokana na dondoo hili, inabainika kuwa Wazungu wanapoingia katika nchi za Kiafrika, hutumia hila ili kujipenyeza na kukaribia maliasili ya mataifa hayo. Wao hujifanya kuwa wamekuja kwa ajili ya manufaa ya Waafrika lakini lengo lao ni kujitayirisha kama vile wakoloni wakongwe walivyojinufaisha kutokana na maliasili ya Bara la Afrika. Baadhi ya wakoloni hao wanya hulifilisi bara hili kupitia njia za kibiashara zinazowafaidi wao tu. Mwandishi anaashiria kuwa Waafrika wanapowaalika Wazungu kutekeleza jambo fulani humu barani, Wazungu hao huwatumia Waafrika vibaya. Kwa mfano, Sele anachukulia matibabu ya daktari wa kigeni anayemtibu kuwa biashara inayoendeleza dhuluma za kiuchumi dhidi ya Waafrika. Anatoa maelezo yafuatayo:

Sele: Si biashara hiyo? Watumie mwili wangu kujinufaisha! Zipo siku za nyuma niliposhawishika kuwaamini. Mwili wangu hawakuufanyia chochote kuuthamini. Wao ndio walinifanya niamini kuwa nina ugonjwa. Tena ugonjwa mbaya...Ugonjwa unaotaka msaada wao...mpaka leo wanataka niamini kuwa nina tatizo na kwamba wao tu ndio wawezao kulisuluhisha...Wanataka niamini nilivyoamini jana (kimya). Wote nawajua.(uk. 77-78).

Katika muktadha huu, ni wazi kwamba tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* inashadidia kuwa wakoloni mamboleo wanawafanya Waafrika waamini kuwa wana shida na kuwa suluhisho la shida hizo laweza tu kutoka kwao. Hii ni njia ya hila ya Wazungu kujileta Afrika tena kuendeleza ukoloni mamboleo. Wakishakubaliwa wanabadili nia na kuanza kunyakua rasilimali za kiafrika kama vile ardhi au madini hasa kupitia mikataba yenye udanganyifu.

4.4 Mbinu za Lugha Zilizofanikisha Maudhui Katika Kazi Hii

Tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* zimetumia mbinu za lugha mbalimbali ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui ya ukoloni mamboleo. Kwa mfano kuna **jazanda** mbalimbali zilizotumika kuonyesha hali ya uhusiano kati ya mataifa machanga na yale yenye nguvu za kiuchumi. Jazanda ni mbinu inyoeezea jambo fulani kwa kutumia lugha ya kimafumbo au lugha fiche (Njogu na Chimera, 1999). Baadhi ya jazanda hizo ni kama vile:

Uhusiano baina ya **Papa na vidagaa** umetumika kijazanda. Kwa mfano, Zainabu akizungumza na Bi.Rahma kuhusu jinsi Sele anavyokataa kula vyakula vya aina yoyote anasema hivi kumhusu Sele:

Zainabu: Anasema eti anawaonea vidagaa huruma kwa kuliwa na papa na yeye pia awale. (Kimya). Anasema huku ni kuonewa maradufu. Anasema ...Anasema...eti tena kuwa hapendi vinavyoliwa huku vinatazama tu. (Uk.15-16).

Papa anawakilisha nchi tajiri za Kimagharibi kama vile Marekani ambazo hudhulumu nchi changa maliasili yao kwa mfano kupitia uchimbaji wa mafuta na madini pamoja na maliasili nyingine huku wakizipeleka kwao. Vidagaa ni kiwakilishi cha mataifa ya Kiafrika yanayonyanyaswa kiuchumi kupitia ubepari wa Kimagharibi. Mwandishi anaonyesha kuwa mataifa hayo huzua rabsha katika mataifa ya kiafrika ili yaweze kuingia katika mataifa hayo na kuiba maliasili yao. Kwa sababu ya vitendo hivi, baadhi ya nchi za Kiafrika zenye maliasili nyingi kama vile Sudani, Angola na Kongo zimekosa utulivu kwa miaka mingi. Hali hii huzua umaskini na kupunguza kasi ya maendeleo katika mataifa ya Kiafrika. Hii ni kwa sababu utajiri wao hutumiwa kujenga mataifa ya Kimagharibi. Hii ndio maana mwandishi anasema kuwa vidagaa hutumiwa kama kitoweo kuonyesha jinsi mataifa machanga hudhulumiwa. Mazungumzo haya yanatilia mkazo jambo hili:

- Sele:** Hata hiyo zamani zilikewepo hadithi kuhusu papa kuwa na wivu kwa kuchelea wingi wa vidagaa. Ndio chanzo cha kuviwinda vidagaa na daima kuviwacha vinaangamia. Kazi rahisi kwa papa kuwafanya kitoweo na sasa vizazi vyake vimerithi
- Aisha:** Wivu hutoka wapi?
- Sele:** Ni zao la inda. Kiburi. Pupa. (kimya). Tamaa.
- Aisha:** Si moyoni?
- Sele:** Labda. Labda fikirani. (Anafikiri). Au labda imani. Mtazamo.
- Aisha:** Lakini papa naye ana fikra gani?
- Sele:** Anayo mimi ni juavyo. Zamani walisema papa hutumia ubongo kuwaza na vidagaa navyo huwaza kwa roho zao (kimya)...Nasikia wakati mwingine papa ndio huchafua bahari na kuzua zahama. (uk.38)

Katika mazungumzo haya, tunaona aina ya uhusiano uliopo kati ya mataifa ya Kimagharibi na yale ya Kiafrika ni ile ya kutoaminiana na kudharauliana. Kama anavyosema mhusika Sele kubaguana huku kunatokana na inda na kiburi na hata tamaa. Nadharia ya ubaada-ukoloni ambayo inaongoza utafiti huu inafumbata wazo hili la ubaguzi na maonevu kutoka mataifa ya Kimagharibi dhidi ya mataifa ya Kiafrika. Mmoja wa waasisi wa nadharia hii, Said (1977), anashikilia kuwa mataifa ya Kimagharibi hujiona kuwa bora kinasaba na kwa sababu hii huwachukulia watu wa Kimashariki na hata Waafrika kama waliokosa ustaarab. Hali hii inaonekana katika mawazo ya Sele anaposema kwamba zamani ilichukuliwa kuwa papa alifikiri kwa ubongo ilhali vidagaa nao wakifikiria kwa roho zao. Hii ni sifa moja hasi waliyokuwa nayo Wazungu kuwahusu Waafrika na Wamashariki na ikawaongoza katika mavamizi yao dhidi ya sehemu hizo.

Mwandishi wa tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ametumia neno **bahari** kijazanda kuashiria ulimwengu unaomilikiwa na mfumo wa kiuchumi wa kibepari. Anaonyesha kuwa kuna nyakati bahari huwa na raha zake linapokuwa tulivu. Pia anabainisha kuwa bahari ina hatari zake vile vile ambazo zinapaswa kuogopwa na binadamu. Mtunzi huyu, anatumia bahari kuonyesha aina ya uhusiano uliopo baina ya mataifa machanga na yale yaliyoendelea. Uwezo wa bahari hapa ni kiwakilishi cha uwezo zilizo nao nchi zilizoendelea na ambao hutumiwa na nchi hizo kuzidhulumu nchi maskini. Tunaona hali hii katika mazungumzo baina ya Aisha na Sele.

Aisha: Naona leo twende tukaogelea

Sele : (Ananywea kidogo) Wewe nenda. Mimi siendi baharini tena.

Aisha : Mbona usiende baharini?

Sele : Bahari ina mengi. Naiogopa. Naiambaa.

Aisha : (Anamtazama kwa mshangao) Unaigoepa nini? Si mahala pa kujipumbaza na kujistarehesha?

Sele : Siku hizi hata watu huangamia mumo humo baharini. Wanapigwa dafrao na maji kwa namna isiyoeleweka.(uk.2-3)

Aidha, kutokana na dondoo hili bahari ni kiwakilishi cha mataifa kama vile Marekani ambayo hukusanya watu kutoka mataifa mbalimbali na kuwadhulumu kikazi. Baadhi ya Waafrika wanaohamia huko hudhulumiwa kwa kufanya kazi ngumu na kwa masaa mengi kama vile mkoloni tu alivyowafanyiza kazi watawaliwa. Kwa njia hii mataifa haya tajiri hutumia mataifa maskini kujiendeleza. Mataifa haya yanatumia mbinu ya hila kujileta karibu na mataifa machanga ili yaweze kunyakua maliasili zao. Kwa mfano vivutio vinavyotumiwa ni kama vile ahadi za msaada pamoja na kuunda ushirikiano wa kibiashara na kijeshi lakini lengo likiwa kumfaidi mwenye nguvu zaidi. Jambo hili linadhihirika hapa chini:

Sele: Na ukiangalia kwa maakini utaona kuwa bahari inakuwa kama kibakuli kidogo kinachokusanya samaki wote pamoja. Kibakuli hiki huwa ni chombo tu cha kuvivuta vidagaa karibu na papa.

Aisha: Aaaaah!

Sele : Kama huamini hulizia. (uk.38-39)

Katika *Kijiba cha Moyo*, kuna nyimbo tatu zilizotumika kijazanda ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui ya ukoloni mamboleo. Sele anawekewa nyimbo mbalimbali na Aisha ili achangamke. Kuna wimbo wa Taarab, wa Rap na mwishowe kuna wimbo wa Kichina. Katika muktadha huu tutarejelea tu wimbo wa mwisho kwani hizo mbili za awali zimeangaziwa katika sehemu ya ubeberu wa kiutamaduni. Wimbo wa Kichina unaitwa, “Yini Yueni” ambao Sele anaufurahia sana kwa kudai kwamba hauna makeke na ni wenye kuridhisha nafsi. Mazungumzo yao yanaenda hivi:

Sele: Lakini sina shaka kuwa ni Yini Yueni. Ni ngoma ngeni hii lakini haina makeke. Ni kama yenye kuridhisha nafsi.

Aisha: Mbona basi ukaiacha kama ulivyofanya?

Sele : (Kwa upole) Aisha ni hatari kuicheza ngoma ya namna hii. Utaichezaje ngoma usiyoelewa asili yake? (uk.12)

Wimbo huu ni ishara ya jinsi nchi ya Uchina inavyozitawala upya nchi za Afrika kwa kisingizio cha kuleta suluhisho kwa matatizo yanayokumba nchi hizo. Nchi ya Uchina inayavutia mataifa ya Kiafrika kupitia mikopo (ikiashiriwa na Yueni) lakini haja yake huwa ni kufaidika na

maliasili yatokayo Afrika kama vile pembe za wanyama maarufu, uchimbaji wa madini na mafuta na maliasili nyingine.

Mbinu ya kinaya pia imetumika sana katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Wamitila (2003) anasema kwamba **kinaya** ni kinyume fulani katika usemi, hali au tukio. Tunaona hali hii ya kinyume katika maneno ya Meya anaposema, “Tumeishaingia katika viwango vya kimataifa.” (uk.14). Ingawa mji wa Cheneo una umaskini mwingi, kiongozi wake anaamini kuwa hali ya maisha katika nchi yake yaweza kufananishwa na ile ya mataifa yaliyoendelea. Mbinu hii pia inajitokeza pale Meya anapoandama sera ya kigeni na kuipuuza ile ya kwake. Mwandishi ametumia mbinu hii kukashfu viongozi wanaoiga kila kitu chenye asili ya ugeni ilhali wana vitu na hali zao nzuri kuliko hizo ngeni.

Pia kuna matumizi ya kinaya wakati Meya kama kiongozi wa Cheneo anaposema kuwa madaktari wa nchi yake ni wa kubabaisha tu na kwamba hospitali zenyewe ni duni. Ingetarajiwa kwamba yeye kama kiongozi wa eneo lake angeboresha huduma za afya badala ya kutazama tu hali hiyo ikizorota.

Vilevile kuna matumizi ya mbinu ya **tasfida**. Hii ni sifa inayotumiwa katika kazi za kifasihi ili kuficha hali fulani ambayo itahisika kuwa na athari fulani isiyokuwa nzuri kwa wasomaji au hadhira, Wamitila (2003). Tasfida inaonekana katika kauli ya Bili anaposema: “**Hivi mama ameshapata mgeni au vipi?**” (uk.25) Katika muktadha huu Bili anadumisha heshima ya mawasiliano kwa kuepuka kuuliza ikiwa mama amezaa au bado. Kisha baadaye anaongeza kauli nyingine ya kitasfida hivi... “**Mara ile ya mwisho tulipokuwa pamoja alionekana amechoka sana**”. (Uk.25). Katika muktadha huu pia Bili anatilia maanani miiko katika lugha kwa kuficha ukali wa lugha ya moja kwa moja.

Tashbihi kama tamathali ya usemi pia imetumika sana ili kujenga taswira mbalimbali. **Tashbihi** ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi (Wamitila, 2003). Mwandishi huyu anasema kuwa tamathali hii hutambulishwa na viungio kama vile, ‘mithili ya’, ‘kama’, ‘ja’, ‘kama vile’, ‘sawa na’. n.k. Meya anamtisha daktari Siki akimwambia, “**Kupinga haya ni sawa na kumkama simba mwenye watoto**” (uk.14). Usemi huu unakusudia kumuonya

Siki dhidi ya kupinga mwongozo mpya wa kuzingatia malengo ya milenia. Meya anaulinganisha ukali wake na ule wa simba mwenye watoto. Sifa kuu za Meya zinazojitokeza katika kifungu hiki ni kuwa ni mtu asiye na msimamo dhabiti kuhusu uongozi. Anajitokeza kama kibarakala cha mataifa yaliyoendelea na ambao hawana falsafa maalum inayoweka msingi wa uongozi wao. Siki anajitokeza kama kiongozi mwenye maono na jasiri. Kwa mfano yeye anaona ni bora kuzingatia sera ya maendeleo iliyobuniwa na Baraza la Cheneo badala ya kutumia sera za kutoka mbali.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* pia kuna matumizi mapana ya **sitiari**. Mbinu hii huhusisha ulinganisho wa vitu viwili kwa njia ya moja kwa moja. Baadhi ya sitiari hizo ni:

Meya akikubali wizi wa fimbo ya Meya anawaambia washirika wake...“**Lazima kwanza mnihakikishie kuwa huyo sumu hapati hata fununu ya jambo hili**”. (uk.62). Katika sitiari hii, Diwani III analinganishwa na sumu kuonyesha jinsi msimamo wake dhidi ya ufisadi ulivyo mkali. Yeye, kama sumu ni hatari kwa Meya, Bili, Diwani I na Diwani II. Meya anaendelea kuonyesha uzito wa kitendo hiki akitumia sitiari nyingine:

.....“**Hii ni bomu inayoweza kutulipukia usoni.**” (uk.63). Katika mfano huu, kitendo cha kiufisadi cha kuiuza fimbo ya Meya ughaibuni, kinafananishwa na bomu inayoweza kulipukia usoni mwa wanaoshiriki wizi huo. Hii ina maana kuwa siri hiyo ya wizi ikitoka nje kutakuwa na athari kubwa hasi kama vile maandamano dhidi ya uongozi wa Meya

4.5 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia vipengele muhimu vinavyonyesha ukoloni mamboleo katika tamthilia zote mbili. Tumejikita katika vipengele viwili ambavyo ni: ubeberu wa kiutamaduni na matumizi ya mbinu za kikoloni za kiutawala. Tumeonyesha jinsi utamaduni wa asili ya Kiafrika ulivyoingiliwa na ule wa Kimagharibi hadi kusababisha uibukaj wa utamaduni mseto kwa mataifa yaliyotawaliwa.

Tamthilia za Arege aidha zimefanikiwa kuonyesha jinsi utamaduni wa Mwafrika ulivyo hatarini ya kumezwa na utamaduni wa Kimagharibi. Zinaonyesha jinsi Waafrika wanavyofurahishwa na maisha ya Kimagharibi kwa njia kadhaa, si vyakula vya kigeni, si mavazi, si nyimbo, si elimu, itikadi na hata huduma za afya. Jambo hili linatoa picha ya bara lililojaa viraka vya kila aina hadi

kufikia kiwango cha kushindwa kujitambua. Kazi hizi zinatoa mwito wa Mwafrika kujisaili yeye ni nani, anatoka wapi na ni wapi anakoenda. Vilevile inadhihirika ya kwamba Afrika ina kijiba cha moyoni ambacho si rahisi kukitoka. Kwa mfano si rahisi kudumisha utamaduni asili wa Kiafrika katika enzi hizi za utandawazi. Kuubadili mfumo wa kielimu uliojengwa kwenye misingi ya Kimagharibi pia itakuwa vigumu. Hata hivyo pana haja ya kutilia umuhimu katika vipengele vinavyokuza utamaduni wa Kiafrika katika mifumo ya kielimu.

Tumeonyesha pia mchango wa baadhi ya vipengele vya kimtindo vilivyofanikisha uwasilishaji wa maudhui haya. Tumechunguza baadhi ya mbinu za lugha zilizojenga maudhui ya ukoloni mamboleo.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika tasnifu hii, tumeshughulikia maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* kwa kuongozwa na nadharia ya ubaada-ukoloni. Utafiti huu ulinua kuchunguza jinsi ukoloni mamboleo unavyoendelezwa katika mataifa machanga na athari zake katika mataifa hayo. Sura hii inashughulikia muhtasari wa kazi nzima na kisha kutoa mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye kuhusiana na suala la ukoloni mamboleo katika tamthilia za Kiswahili. Ili kufanikisha haya, tutatathmini ikiwa malengo ya utafiti wetu yameafikiwa kwa kuzingatia maswali ya utafiti.

5.2 Muhtasari

Tasnifu hii ina sura tano ambapo sura ya kwanza ni utangulizi wa kazi nzima. Katika sura ya kwanza tumefafanua tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti. Tumefafanua pia mbinu za utafiti zilizotumika pamoja na kurejelea maandishi ya awali kuhusiana na mada yetu. Nadharia ya ubaada-ukoloni inayoongoza uchunguzi huu pia imefafanuliwa.

Sura ya pili imeshughulikia maana ya ukoloni kijumla kwa kuchunguza awamu mbili za ukoloni ambazo ni ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Tumeonyesha historia ya ukoloni mkongwe na athari zake katika mataifa yaliyotawaliwa na mkoloni. Kutokana na msimamo huu wa kijumla tumeonyesha jinsi jamii pana ya waandishi wa Kiafrika wakiwemo waandishi wa Kiswahili walivyoliangazia tatizo la ukoloni. Mwishoni mwa sura hii tumeliangazia tatizo la ukoloni mamboleo kwa upana katika mataifa yaliyotawaliwa na mkoloni na hasa nchi za Afrika Mashariki. Kwa kufanya hivi tumeweka msingi mwafaka wa uchambuzi wa ukoloni mamboleo katika tamthilia za Kiswahili zilizoteuliwa.

Upeo wa kazi hii ni sura ya tatu na nne ambazo zimejikita katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* ili kudhihirisha jinsi kazi hizo zimelishughulikia tatizo la ukoloni mamboleo. Hapa, tumeonyesha njia mbalimbali zilizotumiwa kuendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo ambazo ni utegemezi wa kiuchumi, sera za taasisi za kimataifa, matumizi ya mbinu za kikoloni

katika utawala na ubeberu wa kitamaduni. Athari za ukoloni mamboleo vilevile zimeangaziwa wakati vipengele hivi vya ukoloni mamboleo vilivyotajwa hapo awali vilipokuwa vikichambuliwa. Tumedhihirisha baadhi ya vipengele vya kimtindo vilivyofanikisha uwasilishaji wa maudhui. Kwa sababu utafiti huu kijumla ni wa kimaudhui tumejibana tu katika vipengele vya fani vya matumizi ya lugha na uhusika vilivyofungamanishwa na maudhui. Hapa, tamathali za usemi chache za lugha zilichunguzwa pamoja na sifa kuu za wahusika wanaochangia ufanifu wa maudhui ya ukoloni mamboleo.

Mihimili mikuu ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu ni kama vile uibukaji wa utamaduni mseto katika mataifa yaliyokuwa chini ya mkoloni. Hali hii inachangiwa na uigaji wa hali za kimaisha za Kimagharibi unaoendelezwa na mataifa machanga. Pili, kuna utengano wa Kimataifa unaohusu ubaguzi na udunishaji wa mataifa ya Kimashariki na Kiafrika kutoka kwa mataifa ya Kimagharibi. Hali hii inadhihirika katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Mhimili mwingine uliotufaa katika kazi hii unahusu ukandamizwaji wa lugha za kienyeji na ulazimishaji wa lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa. Ukandamizwaji huu wa kilugha unadhihirika katika tamthilia tunazozichunguza kupitia mazungumzo ya wahusika hasa uhamishaji wa msimbo.

Tasnifu hii ilidhamiria kutekeleza madhumuni manne. Kwanza tulilenga kuonyesha mbinu mbalimbali zinazotumiwa na mataifa yaliyoendelea katika kuyadhibiti mataifa machanga. Dhamira hii ilitekelezwa katika sura ya tatu na nne ambapo imebainika kwamba baadhi ya mbinu hizo ni kama vile utegemezi wa kiuchumi. Kupitia njia hii mataifa maskini yanadhibitiwa na mataifa yenye nguvu za kiuchumi kupitia misaada na mikopo. Nchi hizo zinaishi kulipia madeni yenye riba za juu na kutumbukiza wananchi wake katika utumwa wa umaskini. Mbinu nyingine ni kama vile sheria za vyombo vya kimataifa kama vile Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Dunia na Shirika la Biashara la Dunia.

Lengo letu la pili lilihusu kubainisha athari za ukoloni mamboleo katika mataifa yanayoendelea. Baadhi ya matokeo yaliyobainishwa ni kwamba kuna athari nyingi hasi zinazotokana na ukoloni mamboleo kama vile ukengeushi, ufifaji wa utamaduni asili, ukosefu wa kitambulisho asili kwa watu waliotawaliwa, kuzidi kwa utegemezi wa kiuchumi na unyakuzi wa maliasili ya nchi

zilizokuwa chini ya mkoloni. Imebainika kwamba, uibukaji wa utamaduni mahuluti ni athari moja kuu ambayo imelikumba bara la Afrika kutokana na ukoloni mamboleo. Hali hii imesababisha Waafrika wengi kuupania utamaduni wa Kizungu huku wakishikilia pia baadhi ya elementi za uasili wao. Hii ni athari hasi kwa nchi za Kiafrika kwani utamaduni wake asilia unafifishwa.

Tatu tulilenga kuonyesha mchango wa fani katika kufanikisha maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Katika uchunguzi wetu imebainika kwamba matumizi ya mbinu za lugha kama vile jazanda, methali, tashbihi na kinaya zimefanikisha maudhui. Uhusika pia umechangia mno katika uwasilishaji wa maudhui. Mbinu kama vile jazanda imetumika kwingi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na kwamba ufasiri unaofaa wa mbinu hii umefanikisha udhihirishaji wa maudhui ya ukoloni mamboleo.

Lengo la mwisho la kazi hii lilihusu kuchunguza aina ya uhusiano uliopo baina mataifa yaliyoendelea na yale yanayoendelea kwa muktadha wa tamthilia zinazochunguzwa. Imebainishwa kwamba uhusiano huo ni wa kiunafiki kwani mataifa yaliyo na nguvu za kiuchumi ndiyo hutunga sheria zinazoongoza mahusiano ya kibiashara na kisiasa na kushinikiza mataifa mengine kutekeleza sheria hizo. Hili linadhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ambapo tamthilia inaishia kwa kauli kwamba nchi zote zipo katika jukwaani zikiucheza mchezo mmoja lakini kasoro ni kwamba mataifa ya Kimagharibi ndiyo yaliyoutunga na kuuelekeza mchezo huo. Yaani, Wanalazimisha mataifa machanga kuucheza watakavyo wao (Wamagharibi).

Utafiti wetu uliongozwa na maswali manne ya utafiti ambayo ni:

Je, ukoloni mamboleo umeacha athari hasi zipi za kimaendeleo katika mataifa machanga kama inavyodhihirika katika tamthilia teule? Katika uchunguzi wetu, imebainika kwamba athari hasi zinazotokana na ukoloni mamboleo ni nyingi na kwamba itakuwa vigumu kwa mataifa machanga kujiepusha na athari hizo. Athari hizo zimetokana na matatizo ya kiuchumi ya nchi zilizotawaliwa pamoja na udunishaji wa utamaduni wa mataifa yaliyokuwa chini ya utawala wa kikoloni. Swali la pili lilikuwa: Je, ni mbinu zipi zinazotumiwa kuendeleza ukoloni mamboleo katika mataifa machanga? Tulibainisha kwamba, mbinu hizo si wazi na kwa sababu hii viongozi wengi na wananchi wao hawafamu njia za kilaghai zinazotumiwa kuendeleza ukoloni

mamboleo. Imebainika kuwa baadhi ya mbinu hizo ni utoaji wa mikopo na misaada lakini utoaji huo ukiambatana na vikwazo na masharti fiche. Kwa mfano suala la mikopo na misaada linachangamkiwa mno pasi na kujiuliza ni kwa nini mataifa ya Kimagharibi hutoa mikopo na misaada hiyo. Utafiti huu umeonyesha kwamba nchi zinazotoa mikopo na misaada ndizo hufaidika zaidi kuliko zile zinazopokea.

Je, mataifa machanga yamechukua mikakati madhubuti ya kujikomboa kutokana na athari hasi za ukoloni mamboleo? Uchunguzi huu umebaini kwamba hakuna hatua zenye mashiko zinazoonekana zikitoka mataifa hayo zikilenga kuuasi ukoloni mamboleo, baadhi ya nchi zimebuni wizara za utamaduni pamoja na jitihada za kutambua lugha asili kwa ajili ya kuimarisha ujitambulishaji. Hata hivyo juhudi hizo hazijapewa umuhimu unaostahili pamoja na kutengewa hazina ya uimarishaji huo. Kwa mfano nchi nyingi za Afrika zimeidhinisha matumizi ya lugha za kigeni kama lugha rasmi badala ya lugha moja kati zile zinazozungumzwa na wananchi wake. Vilevile jududi za kufunga utegemezi wa misaada na mikopo hazijafua dafu na kwa sababu hii mataifa mengi hutegemea nchi za Ulaya zilizoitawala kuziauni kifedha, kijeshi na hata wakati wa mikasa mbali mbali.

Je, uhusiano wa kimataifa kati ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea unafaidi pande zote mbili kiuchumi? Kama tulivyoonyesha katika sehemu ya madhumuni hapo juu, uhusiano huu ni wa kinafiki na kidhalimu. Imeonyeshwa kwamba uhusiano huu ni wa mwenye nguvu mpishe ambapo nchi zenye misingi dhaifu ya kiuchumi na kisiasa huendelea kudhulumiwa. Hii ndio maana Fanon (1977) anadai kuwa miji mikuu karibu yote ya Ulaya imejengwa na maliasili ya kutoka Afrika. Ni wazi kuwa baadhi ya maswali ya utafiti yamethibitishwa na mengine kukanushwa. Kwa mfano maswali mawili ya mwisho yamekanushwa ilhali yale ya mwanzo mawili yamethibitishwa.

5.3 Hitimisho

Katika kazi hii tumehakiki maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Data ilikusanywa kwa njia ya usomaji wa kina katika maktaba na ikachanganuliwa kwa ufafanuzi. Suala la ukoni mamboleo limewekewa msingi kwa kurejelea

historia ya ukoloni kijumla na kisha kuonyesha jinsi tatizo hili lilivyoangaziwa na waandishi mbalimbali wa Kiafrika hasa wa Kiswahili.

Maudhui ya ukoloni mamboleo yameshughulikiwa na waandishi wafasihi ya Kiswahili katika tanzu mbalimbali. Sisi tumejikita katika utanzu wa tamthilia kwa kuzichambua tamthilia mbili za Timothy Arege. Tumeonyesha njia mbalimbali zinazoendeleza ukoloni mamboleo katika mataifa yaliyokuwa chini ya utawala wa kikoloni kama inavyodhihirika katika kazi hizi. Baadhi ya njia hizo ni utegemezi wa kiuchumi, ubeberu wa kitamaduni, sera za taasisi za kimataifa kama vile Benki ya Dunia na matumizi ya mbinu za kikoloni katika utawala.

Utegemezi wa kichumi kwa mfano unachangia kupungua kwa kasi ya maendeleo kwa njia kadhaa kulingana na tamthilia hizi. Kwanza, unapalilia upuuzwaji wa taasisi muhimu za kitaifa kama vile hospitali na shule kama inavyoonekana katika *Mstahiki Meya*. Hii ni kwa sababu watawala wengi hawatafuti huduma katika nchi zao bali husomesha watoto wao ng'ambo nazo huduma za afya huzipata huko vilevile. Utegemezi uliokithiri pia umeonyeshwa kuchangia umaskini na ufisadi hasa kwa sababu mikopo inalipwa kwa riba za juu kwa miaka mingi. Hali hii hutumbukiza nchi husika katika utumwa wa madeni. Pesa zinazokopwa pia zinaelekezwa kwa miradi isiyofaidi uchumi kama vile ulipaji wa mishahara.

Tamthilia tunazochunguza pia zimedhihirisha kuwa mataifa mengi huru yanaendelea kutawaliwa upya kwa njia zisizo wazi na mataifa yenye nguvu za kiuchumi. Mataifa haya yanatumia njia za kilaghai kama vile utoaji wa misaada na mikopo ili kuyanasa mataifa machanga kwa lengo la kunyonya maliasili zao. Kutokana na tamthilia hizi, inaonekana kuwa ingefaa mataifa machanga yachunguze upya uhusiano wao na mataifa yaliyoendelea. Kazi hizi zinakosoa hali ambapo mataifa ya Kimagharibi ndiyo hutoa maamuzi makuu hasa kuhusiana na uchumi na siasa na kulazimisha maamuzi hayo kwa nchi za Kiafrika.

Utafiti huu umekumbwa na matatizo kadhaa kama vile ukosefu wa muda wa kutosha kwa sababu umefanywa wakati mtafiti akiwa kazini. Kwa hivyo, ilikuwa changamoto kubwa kuwasiliana na wasimamizi ana kwa ana mara nyingi. Hata hivyo, matumizi ya mtandao yalisaidia kuliziba pengo hili kwani mtafiti aliweza kutumia mdahalishi kutuma kazi kwa wasimamizi na kupokea

majibu. Tatizo lingine lilihusu uhaba wa fedha hasa za kugharamia ununuzi wa vitabu na usafiri. Mara nyingi mtafiti alihitaji kusafiri jijini Nairobi kupata huduma za maktaba na kupata mawaidha kutoka kwa wasimamizi. Mwisho, vitabu vingi tulivyorejelea vimeandikwa kwa lugha ya Kingereza na hili likabidi matumizi ya muda mrefu katika kupata tafsiri zinazofaa kuhusu ya dhana mbalimbali.

Ingawa kazi hizi tulizozihakiki zimefanikiwa kwa kiasi fulani kuangazia maudhui ya ukoloni mamboleo, ni wazi kwamba kuna maudhui mengine yaliyochukua nafasi kubwa zaidi. Kwa mfano, tamthilia ya *Mstahiki Meyya* imefanikiwa zaidi katika kuzungumzia maudhui ya uongozi mbaya nayo ya *Kijiba cha Moyo* imejikita sana katika maudhui ya uhusiano wa kimataifa.

5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza maudhui ya ukoloni mamboleo katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meyya* kwa kutumia nadharia ya ubaada-ukoloni. Tunapendekeza kwamba tafiti za baadaye zichunguze maudhui haya katika tanzu nyingine hasa hadithi fupi na ushairi. Tamthilia hizi pia zinaweza kufanyiwa uhakiki wa kimtindo kwa kuangalia jinsi kazi hizo zilivyotumia tamathali za usemi mbalimbali katika kusuka kazi zake. Hii ni kwa sababu tulipokuwa tukichunguza tamthilia hizi tumegundua kwamba zimesheheni tamathali kama vile methali, nahau, tashbihi, taashira, taswira, kinaya na nyinginezo. Vilevile tamthilia hizi zimeshughulikia maudhui ya uongozi mbaya kwa kina. Tunapendekeza pia uhakiki zaidi ufanywe kuhusiana na hali hii kwa kurejelea masuala ya ufisadi, tamaa, dhuluma kwa wanyonge, ukabila na mengineyo.

Tunapendekeza pia utafiti zaidi kufanywa kuhusina na tamthilia hizi kwa kutumia nadharia nyingine kando na ile ya ubaada-ukoloni tuliyoitumia. Kwa mfano, nadharia ya uhalisia inaweza kutumiwa kuchunguza jinsi mataifa ya Kiafrika yanavyolemazwa na matatizo yanayohusiana na uongozi mbaya kama vile ufisadi. Nadharia ya umaksi vilevile inaweza kutumiwa kuchunguza jinsi tatizo la utabaka linavyojitokeza katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meyya*.

MAREJELEO

- Abrahams, P. (1946) *Mchimba Madini*: Nairobi. Heinemann Education Books.
- Achebe, C. (1973) *Shujaa Okonkwo* (Tafsiri ya Clement Ndulute): Nairobi. Heinemann Educational Books.
- _____ (1977) *Mwakilishi wa Watu* (Tafsiri ya Douglas F. Kavugha): Nairobi. Heinemann Educational Books.
- Arege, T. (2009) *Kijiba cha Moyo*: Nairobi. Longhorn Publishers.
- _____ (2009) *Mstahiki Meya*: Nairobi. Vide-Muwa Publishers.
- Arowolo, D. (2010) "Effects of Western Civilisation and Culture on Africa.", katika *Afro-Asian Journal of Social Sciences*, Vol 1.No.1 Quarter IV(pg 2-22)
- Buffon, G. (1930) *Buffon's Discourse on Style*. Paris: Librarie Hatier Publishers.
- Coombes, H. (1963) *Literature and Criticism*.New York: Charto and Windows.
- Encyclopaedia Britannica* (1988) Chicago: University of Chicago Press.
- Fanon, F.(1963) *The Wretched of The Earth*: Newyork. Grove Press Incl.
- _____ (1967) *Black Skins White Masks*. London: Grove Press.
- Hancock, G.(1991) *Lords of Poverty: The Power, Prestige and Corruption of The International Aid Business*: London. Atlantic Monthly Press.
- Hussein, E.N. (1969) *Kinjeketile*: Dar es Salaam. Oxford University Press.
- _____ (1971) *Mashetani*: Dar es Salaam. Oxford University Press.
- Ikechukwu, E.(2013) "Dependency Theory and Africa's Underdevelopment: A paradigm Shift from Pseudo-Intellectualism: The Nigerian Perspective." Katika *International Journal of African and Asian Studies*. Vol.1. (pg. 116-125)
- Kairi, M .(2014) "Ukoloni Mamboleo na Utandawazi Katika Tamthlia za Sudana na Posa za Bikisiwa". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

- Kareithi, P.M. (1968) *Kaburi Bila Msalaba: Hadithi ya vita vya Mau Mau*: Nairobi. Phoenix Publishers.
- Karim Abdul, B. J. (2006) *Utenzi wa Vita vya Maji Maji*: Dar es Salaam. TUKI.
- Keesy, D. (1998) *Contexts for Criticism*: California. Mayfield Publishing Company.
- Khamis, B.S. (2015) “Usimulizi katika Tamthlia za Mstahiki Meya na Kijiba cha Moyo”. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Kilanga, B.S. (2014) “Ishara katika Tamthlia ya Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo”. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Ki-Moon (2015) *Millinium Development Goals 2015 Report*: Newyork. UNDP.
- King’ei, K. (1999) “Historia na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili” katika *International Journal of Arts and Social Sciences*. Vol.1, Dec 1999. Pg 82-93.
- Kiruthu, Kapiyo & Kimori (2011) *The Evolving World: A History and Government Course for Form 3*: Nairobi. Oxford University Press.
- Leech, G. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Publishers.
- Leech, G.M. na Short, M. (1981) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. England: Longman Group Ltd.
- Magare, F.A. (2002) “Uhakiki wa Tamthlia ya Amezidi Kama Kazi ya Kibwege”.Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Magati, C. (2013) “Ukuaji wa Muundo na Mawazo katika Tamthlia za Timothy Arege”. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Matundura, E. na Ngesa, A. (2015) “Mwingilianomatini kati ya tamthlia ya Mashetani na Kijiba cha Moyo katika Swahili Forum 22.
- Mazrui, A. (1982) *Kilio cha Haki*: Nairobi. Longman Publishers.
- Mazrui Ali (1979) “The African Condition, Lecture 1: The Garden of Aden in Decay”. Lecture Delivered at Reith on 7th November, 1979.

Mbatiah, M.(2001) *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi. Standard Textbooks Graphics and Publishing.

_____ (2012) “*Deviation as a Communicative Strategy in Gamba La Nyoka*” Katika Swahili Forum 19.

_____ (2016) *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo Yake*: Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S.A. (1995) *Amezidi*: Nairobi. East Africa Education Publishers.

_____ (2001) *Mwongozo wa Kilio cha Haki*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mulokozi, M. (1979) *Mukwava wa Uhehe*: Nairobi. East African Education Publishers.

Mkangi, K. (1995) *Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mutiga, M.(2017) “*Trump Offers Africa A Chance to Kick out Aid Addiction and Chart its own Path*” katika Sunday Nation 22/01/2017. Nairobi: Nation Media Group Publication.

Nazareth, P. (1978) *The Third World Writer: His Social Responsibility*: Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Ngara, E. (1982) *Stylistics Criticism and the African Novel*. London. Heinemann Educational Books.

Njogu, K. na Chimera, R.(1999) *Ufundishaji wa Fasihi*: Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Nkrumah, K. (1965) *Neo-Colonialism, The Last Stage of Imperialism*. London. Thomas Nelson and Sons Ltd.

Nyerere, J (1967) *Education for Self Reliance* Retrieved from <http://www.swaraj.org/shikshantar/resources-nyerere.html>

Obamba, M. (2006) “Governance of Higher Education, Research and Innovation in Ghana, Kenya and Uganda” in African Network for Internationalisation of Education (ANIE).

Ogot, B.A and Ochieng, W.R. (1996) *Decolonisation and Independence in Kenya: 1944-1993*: Nairobi. East African Education Publishers.

- Okwena, S. (2013) “Matumizi ya Jazanda Katika Tamthilia Tatu za Timothy Arege.” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta .(Haijachapishwa)
- Pamba, S.E. (2012) “An Analysis of the Impacts of Structural Adjustment Programmes on Education in Sub-Sahara Africa: A Case Study of Kenya (1980-2010)”. M.A Thesis University of Nairobi.(Unpublished)
- Padley Steve (2006) *Key Concepts in Contemporary Literature*. Newyork: Palgrave Macmillan.
- P’Bitek, O. (1975) *Wimbo wa Lawino*: Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.
- Rodney, W. (1976) *How Europe Underdeveloped Africa*: Dar es Salaam.Tanzanian Publishing House.
- Said, E. (1977) *Orientalism*. New York: Pantheon Books Ppublishers.
- _____ (1993) *Culture and Imperialism*. New York: Vintage Publishers.
- Senkoro, F.E.M (1982) *Fasihi*: Dar es Salaam. Press and Publicity Centre.
- Sharma, A. (2015) “The Making of the Third World: The Impact of Colonization” katika The Research Journal of English Language and Literature (RJELAL) . Retrieved from <http://www.rjelal.com>.
- Stewart, N. (1951) *Divide and Rule: British Policy in Indian History*: London. Guilford Press.
- Wafula, R. M. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historian a Maendeleo Yake*: Nairobi. Jomo Kenyatta Foundational.
- Wamitila. K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi; Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- _____ (2003) *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*: Nairobi. Focus Publishers.
- Wa Thiong’o, N. (1964) *Usilie Mpenzi Wangu* (Tafsiri ya J.S. Ndeti): Nairobi. Heinemann Educational Books.
- _____ (1970) *Mtawa Mweusi* (Tafsiri): Nairobi. Heinemann Rducaional Books.

_____ (1974) *Njia Panda* (Tafsiri ya J.S. Ndeti): Nairobi: East African Publishing House.

_____ (1981) *Writers in Politics*: London. Heinemann Educational Books Ltd.

_____ (1986) *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature*: Nairobi. Heinemann Educational Books.

Wa Thiong'o, N. & Micere, M. (1978) *Mzalendo Kimathi*: Nairobi. Heinemann Educational Books.

Were, E. (2012) "Fani katika Tamthilia za Kiswahili; Uchanganuzi wa Kilio cha Haki na Kijiba cha Moyo". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)